Anthologie

aus der

Suaheli-Litteratur

(Gedichte und Geschichten der Suaheli)

gesammelt und übersetzt

von

Dr. C. G. Büttner,

Lehrer am Seminar für orientalische Sprachen in Berlin.

Erster Theil.

Texte.

Berlin.

Verlag von Emil Felber.

1894.

27254.50.2

HARVARD COLLEGE
NOV 7 1895
LIBRARY

Sainsbury fund.
I, II (in 1.)

Alle Rechte vorbehalten.

Inhaltsverzeichniss.

Seite

Vorwort vii
Utenzi wa shufaka 1
Utenzi wa mi'iraji 31
Utenzi wa kutawafu kwe Muhammadi 53
Hekaya na visa 77
  Hekaya ya nabii Musa na kipofu 79
  Asili ya vitu vya themani 80
  Kisa cha Alibegi Kashkashi 85
  Hekaya za Abunawasi 87
  Wanawake watu gani 92
  Kisa cha sungura na cheche 95
  Maneno matatu 97
  Kisa cha Mwarabu na Mgunya 102
  Mzee kipofu na bunduki yake 103
  Asili ya mgomba 104
  Kazi ya shamba 104
  Kisa cha binti Matlai Shems 106
  Nini bora, mbingu au ardhi 115
  Sababu ya maji yakiyaa yakipua 116
  Hadithi ya mpomboo 116
  Hadithi ya chewa 117
  Binti la ngombe mia 117
  Mutanebbi 123
  Maneno matatu kwa reale elfu tatu 125
Mazehebi ya watu wa Unguja 131
Khabari ya Amur bin Nasur 147
  Khabari ya wazee wangu 149
  Khabari yangu mtoto 150

Seite
Nilitiwa chuoni 152
Mimi kijana 154
Safari ya Berlin 156
Khabari ya katika Berlin 159
Khabari nyingine ya Berlin 166
Khabari ya Unguja 170
Mashairi madogo 177

Utenzi wa Shufaka

(Das Gedicht von der Barmherzigkeit.)

1. Akhi patia hiburi
na lahu ya mistari
na kalamu ya sifuri
ipendezao kwolea.

2. Tinde ya shaba kalamu
ipate kustakimu
na lahu twaa ya Shamu
ipendezao kuoea.

3. Kisa, uje ukaribu,
mbele i utakarabu,
tamukalo ukutubu;
ukihifadhi makaa.

4. Ambalo linanitoka
tenda hima kuliandika;
moyo hauwezi weka
kwa ghamu na mashangaa.

5. Tamukalo kwa lesani
litie karatasini
kwa khati ngema bayani
ambayo yatujibia.

6. Hati iwe maarufu
zilingane tu harufu,
nukuta ziwe tatufu
zisikutane pamoja.

7. Nukuta na zilingane
na harufu zifanane,
na erabu tuzione
tupate kufahamia.

8. Na ifunuke hatie
harufu fupi na nyie;
na zituo uzitie
tupate kupambanua.

9. Pa fataha pa eribu
na domma uzirakibu
na kesre na erabu
sisahau kuzitia.

10. Na kulla penyi sakana
erabu eribu sana;
na mada na tanwina
nayo na kuhekimia.

---

3. 1. kisa = kiisha, danach.
3. 2. mbelei = mbele yangu, vor mich; i ist das arabische Suffix.
8. 2. nyie = re, lang.

11. Laza ya mutu katibu
ni kusahihi erabu
na kutoa kukalibu
harufu kutanganua.

12. Khati ikiwa hiyari
husitawiza shairi;
na ambao wabusuri
humupendeza kuoa.

13. Kwamba nakuhikimiza,
nimezile kukueleza,
basi. Kalamu fuza,
andika, takutaya.

14. **Bism illahi!** Isimu
yake Muungu karimu
mwenyi kutunga nudhumu
kukadimisha makaa.

15. Andika: **bism Illahi**,
rabbi asiye shabihi;
wapate kutanabihi
waja wenyi kusikia.

16. Uoe na: **rahamani**
mwawazi dunyani,
insi na jinani
muslimu na asiya.

17. Uandike na: **rahimu**,
mwenyi pepo na jahimu,
mteuzi wa kaumu,
kesho takaye teua.

18. Baada ye ukutubu
sifa za tuma habibu
muungwana wa Arabu
asiye kombo na tua.

19. Ndiye mwenyi mamulaka
mbele za Mola rabbuka,
ndiye mutume hakika
wa kwanza kubuathiwa.

20. Suyu nabii amini,
ndiye tuma wa Mannani,
muhifadhi kuruani,
asipokuyua kuoa.

21. Muhammadi tahakiki,
ndiye mupanda Boraki
hatta mbele za khalaki
alipo kasikilia.

22. Akakaa na Mola we
kama ninga na utawi,
na kulla jambo ambiwe
ambalo lahitajia.

23. Huyu ndiye maarufu
si kauli adh'afu,
na katika musahafu
alikotubainia.

---

16. 3. insi, arab.: Menschen.
16. 4. asiya, Widerstreitende, Abtrünnige, Heiden.
20. 1. suyu = huyu.
21. 4. kasikilia = kafikilia.

Kauluhu taala:

Thumma dana fatadala, fakāna kāba kausēni au adna faauha ila abdihi maauha ma kazzaba ilfuadu ma ara. Tamat.

24. Ndiye mpewa salati
na saumu na sakati
na kushufai umati
siku ya nyota na ndaa.

25. Ndiye tuma muduthiru,
shems ilanwaru,
mukhulukwa kwa nuru
isiyo kuzizimia.

26. Muhammadi mukaramu
ni said ilan'āmu;
Rabbi salli wa salimu
salla tukimsalia.

27. Salla Allahu aleika
mwana muzaliwa Maka
mwenyi moyo wa shufaka
na ruhuma ze pamoya.

28. Ndiye mungi wa saburi,
ndiye mutendewa kheiri,
ndiye mpata kuffari
na jihadi kwendea.

29. Ndiye Abalkasima
wa batuli Fatima,
wana wake wasijana
wenyi nuru kama taa.

30. Ndiye tuma mustafa
muumbwa kwa nyingi sifa
mujuvi wa maarifa
mwelefu wa kutambua.

31. Ndiye muumbiwa janna
wa huru fiha sakina
wanawake wasijana
wenyi nuru kama taa.

32. Wanawake sao tamu
wasio wasaha na damu,
miongoni mwa naimu
mtume aliwekewa.

33. Awekewa mursali
na sahaba ze na Ali
na ambaye wakukubali
na tuma kufuatia

---

25. 2. anwaru, arabischer Plural von: nūr, das Licht.
31. 2. huru fiha sakina, arabisch; huru, die Huris, fi in, ha (bezieht sich auf janna) ihm; sākina, wohnend.
32. 1. sao = hawo, diese genannten.

34. Kwa sadiki Bubakari
wa Faruki Omari
na Othmani na Ghori
wa Haidari Alia.

35. Na Abudirrahamani
na Zobeiri yuani
maa wa saidini
Amri na Talihia.

36. Na kulla palipo mema
tajaziwa jaza ngema
na wawezao ni tama
na nyumbani wenda kaa.

37. Mteuzi ndiye daiyani
wa insi na muumini.
Kulikosi ni kuthanni
na thanna inapotwaa.

38. Thanna ya vuta shutumu
na kujiingisha ithumu.
Sifa za banu Hashimu
siwezi kuwasifia.

39. Sifa za Mungu jabbari
na mtume we bashiri
mutima haukadiri
sifa zake kuzimaa.

40. Nyani, awezao nyani
sifa zake kubaini?
Mashekhi wakayakini
kuona kuwa thakia.

41. Mtu angajitahidi
kwa ukuu wa juhudi,
akali yake muradi,
hawezi harufu moya.

42. Nikomile kuzukuri
sifa za Mola jabbari.
Pasilepo pa khubiri
yaliopita auwala.

43. Moyo umezetamani
hadithi kuibaini
ya tangu kale zamani
za bani Israila.

44. Mbwene hadithi ajabu
yaandishiwe maktubu
kusoma kwa kiarabu;
maana yakinielea.

45. Niyawenepo chuoni
moyo wangu hatamani
kubadili kimangani
kwa kisawahili kuioa.

46. Auwali ya matongozi,
sikizani wasikizi,
yina la suu utenzi
ni „Wa shufaka" kuyua.

---

34. 2. wa, arabisch: und.
35. 3. saidini, des Reimes wegen statt saidina, unser Herr, d. h. Muhammad.
40. 1. nyani = nani, wer.
45. 2. hatamani = nikatamani, und ich begehrte.
46. 3. yina = jina, Name.

47. Utenzi huu, fahamu,
ni wa kisa cha Kasimu
na malaika muathamu
Jibrili na Mikaila.

48. Zamani moya hakika
washindanile malaika,
kushindania shufaka
na ruhuma kusalia.

49. Ile zamani, wayuli,
za bani Israili
kuli, nawanena kweli,
na wapendao fadhila.

50. Unenile Jiburili
maalimu wa rasuli
mbele za Mikaili
kana kujihadithia.

51. Akamwambia: mwandani,
pasaliwa dunyani
ya shufaka na huzuni
rehema kuonekea?

52. Asiridhi Mikaili
kamwambia Jiburili:
siyaoni kuwa kweli
hayo ulionambia

53. Ya shufaka na rehema;
ile zamani za nyuma
mbali sasa ni malama,
shufaka haikosa.

54. Akajibiwa makali
maalimu Jiburili.
Amwambii Mikaili:
shuka, tukenze wasia.

55. Na tushuke twende kuko
wana Adamu waliko
tukasairi mashiko;
na maana kutuelea.

56. Basi. Wakatanazile
wakashuka wo wawili
madina wakawasili
kati muyi wakaingia.

57. Wakashukia madina
kwa umbo ilinsana,
khabari wakaiona
na shauri lili moya.

58. Katelea Jiburili
ali mwele alili;
na suyu Mikaili
ali tabibu, sikia.

---

49. 3. kuli, Copula = da war.
54. 4. tukenze = tukaenze; enza = tazama, besuchen, untersuchen.
55. 3. sairi = saili, fragen.
56. 2. wo, alterthümlich für wao.
56. 4. muyi = mji, Stadt.
57. 2. ilinsana, arab.: Menschen.
57. 4. lili, alterthümliche Form der Copula: er war; vergl. ali 58. 2.

59. Jiburili kushukani
akaenda mosketini.
Na Mikaili, yuani,
utukuni akakaa.

60. Walio mosketini
waungwana wa madani
kumwona we mugeni
kwa wote wakamwendea.

61. Wakaenda kumbusuri
na kamutaka khabari:
hali, umuja, shururi
au, umuja, alia?

62. Katamuka kawajibu:
inyi ndugu Waarabu
nijile, nili ngaribu
wala nisipo bithaa.

63. Na kwetu kuwa baidi
tarikii ni shadidi;
napenda mujitahidi
munirehemu ajaa.

64. Nirehemuni, wayuzi,
moyo uate simanzi,
naye Muungu, wajuzi,
tawarehemu ajaa.

65. Kanena kisikitika,
matozi kimiminika,
mutima uli na buka,
pua kivuta mara mia.

66. Wale wana wa madani
walio mosketini
wamwambia: wapenda ni
kwetu ambacho wataa?

67. Ayatuha ilgaribu,
twaa fedha na zahabu;
na ambacho watulubu
tu wenyi kukutendea.

68. Maalimu Jiburili
akaeta yake kauli,
waambia: sitaki mali,
nataka ndwele kupoa.

69. Waungwana wa madina
wamujibu iyohina:
kwetu tabibu hakuna
ya walio Allahi taala.

70. Naye sapo awambile:
tabibu mwenu yujile
muyini walingizile
na utukuni mekaa.

---

59. 2. akenda = akaenda.
63. 4. ajaa = ajala, ihr Brüder, Männer.
64. 2. uate = uache.
66. 4. taa = taka, oder talaba, des Reimes wegen verkürzt.
68. 2. akaete = akalete, alterthüml. Perfect.
69. 2. iyohina, alterthümliches Demonstrativpronomen zur nyumba-Klasse.
70. 1. sapo = hapo; awambile, yujile, walingizile, alterthüml. Perfectformen; lingiza = ingia.

71. Jeo sizo Arabia
wakauka kumwendea,
na Jiburili pamoya
asiate kutubaa.

72. Wakaenda wote kwa hima
ili kumtumai zema
penyi tabibu wakaima
alipo wakaawia.

73. Wakimala kuwasili,
salamu wakaratile
wakampa Mikaili,
naye akawapokea.

74. Thumma kala: marahaba
bi kudumika ahiba,
wa ma alazi atlaba
min, ayuha rajua?

75. Hali kwangu mwataka ni?
mujile kwa haja gani?
Wale wambi: ni mugeni
ataka kurehemwa.

76. Wakatamuka: jawabu
twapenda umtabibu
suyu mwele ngaribu
na ujira utatwaa.

77. Mutabibu tu mgeni,
kwetu utwae thamani
na kwa Muungu mannani
utapata afdala.

78. Basi, kaamba Mikaili
kamwambia Jibrili:
uzunu min ajili
pate kukuangalia.

79. Jiburili akegema,
tabibu kamtezama.
Baadaye akasema,
watu wakimsikia.

80. Tabibu akatongoa:
maradhi saya yakua
na dawa ikitakiwa
mashaka kuonekea.

81. Wale wapenda thawabu
wakamrudi tabibu:
nena ambalo wahibu
tu wenyi kukuridhia.

82. Dawa ikiwa mujini
twanunua kwa thamani,
bali suyuno mugeni
apate yake afua.

---

74. Diese Strophe ist arabisch. Die Uebersetzung in Suaheli folgt in Str. 75.
75. 3. wambi, contrahirtes Perfect für waambile.
79. 1. akegema = akaegema.
80. 2. saya = haya.
82. 3. suyuno = huyuno, alterthüml. Pronomen.

83. Tabibu kaeta lafuzi
kiwambia wasikizi:
takani muke muzazi
mzoefu wa kuzaa.

84. Ambaye mwenyi adadi
waana sabaa maadudi
walume wenyi ahadi
wasio kuwa tawia.

85. Kisha, wakamufilia
sitta wakamwondokea,
kasalia ni mmoya
ulimwenguni kukaa.

86. Mwana huyu akiwapo
kitinda mimi nilipo,
damu ye aipakapo,
fa laala akapoa.

87. Tabibu kisha waeleza
na wale wakisikiza,
iwile kwenda kufuza
majumbani kutefua.

88. Wakaifuza madina
wakuu hatta wanona;
wasizumbue kijana
illa kwa mtu mmoya.

89. Illa kwa mutu tajiri
mungi wa mali kathiri,
mutu muume basiri
mungi wa kunyenyekea.

90. Wapetepo mulangoni
wakaamba: bismillani;
kawaamuru: pitani;
nao wote wakaingia.

91. Kupita kwao kaumu
kanena mutakaddamu:
salamu, salamu
aleika, ya rajua.

92. Yule mungi wa akili
asiajize kauli
kahimiza tashili
salamu kuipokea.

---

84. 3. walume = waume, männliche.
84. 4. tawia, vielleicht = tawila, lange = warefu, na wingi wa miaka.
86. 2. tinda = chinja, schlachten.
86. 4. fa laala, arabisch: fa und, laala vielleicht.
87. 4. tefua, des Reimes wegen für tefuta, tafuta.
88. 2. wanona = watoto, die Kinder, die Kleinen.
90. 1. pete, Perfect von pata, wie im Yao.
90. 2. bismillani, ist wie eine Art Plural von bismilla gebildet, als wenn dieses ein Imperativ wäre!

93. Kiisa ambi: karibuni,
nyumbani mustakini,
munipe yenu maani
mulionikusudia.

94. Inyi waana wa Mangani
kwangu mwisiwe nini?
tafadhali nambiani
haja mulio kuyia.

95. Wale wote ajwadi
kalima wakamrudi:
matlaba na muradi
kwako we tutakwambia.

96. Kwetu leo ni mgeni
alituyiye muyini,
naye yumo muongoni;
suyu wakuangalia.

97. Twapenda umurehemu;
moyo we usitakimu,
naye Muungu rahimu
rehema takuzidia.

98. Yule mungifu wa dini
kusikia kwe maneni
yungizile furahani
moyo we kaukundua.

99. Thumma akatakalamu
akiwambia kaumu:
mupendalo liyatimu,
hasha, si mwenyi kataa.

100. Kwanza, ndugu, sikizani
tawaambia ya sirini;
ni na zikwi sabuini
nyumbani nimowakaa.

101. Ni na zikwi akithari
fedha na dinari;
fungu la Mola jabbari
linipashilo kutoa.

102. Nalimupele natwale
zote, naye tukulile
na za tunu nimwongele
mimi kumutunukia.

---

93. 1. ambi, alterthüml. Perfect.
93. 3. maani für maana.
94. 2. mwisiwe, Perfect vor isa.
96. 2. yiye, alterthüml. Perfect von ya.
98. 1. In mungifu ist die den Sinn verstärkende Endung fu an mungi (= mwenyi?) angehängt.
98. 3. yungizile, alterthüml. Perfect von ingiza = ingia.
98. 4. kundua = kunjua, entfalten; Er schloss sein Herz nicht hartherzig zu.
100. 3. zikwi, Plural von kikwi für vikwi, eine Myriade.
101. 1. akithari, arabischer Comparativ von kethîr, mehr.
102. 1. pele, Perfect von pa; twale = twae.
102. 2. tukulile = chukulie.

103. Tamupa kimututiza
nguo zahabu na fedha
na waja wa kutumiza
abidi na jariya.

104. Wamadina wamujibu:
mali siyo matulubu;
marithawa ya ngaribu:
wapenda kutabibiwa.

105. Kwako kahitaji mali
lau tembe haridali,
illa wako we ayali
ukimpa yuwatwaa.

106. Yule mungi wa Muungu
kawauza kwa utungu:
tamutenda ni mwanangu,
nimupapo kipokea?

107. Akajibiwa: fahamu,
mwana ukimusalimu,
tamutinda ja ghanamu,
damu apanguse zia.

108. Damu ya mwana, sahibu,
aipakapo ngaribu,
kwa kauli ya tabibu
marathi ye yuwapoa.

109. Fa kala: ya kaumu,
naliridhie kalamu;
damu ya wangu ghulamu
kwenda kumtabibia.

110. Iwile kwamba ni na o
waana elfu mwambao
mukinambia: mupeo,
ningemupele jumaa.

111. Kwa wote ningampee,
ili kuwa fidia ye
bi wajihi Illahi naye
Muhammadi mursaa.

112. Mauti haya hayai
muja hayamuchukii;
umuri ye uli hayi
roho isijatimia.

---

103. 1. tutiza, von tuta, wegtragen, jetzt nur noch in der Frauensprache gebräuchlich.
103. 4. abidi und jariya, arabisch: Knechte und Mägde.
104. 2. siyo = hiyo.
105. 1. kahitaji, negative Form.
105. 3. ayali, Familienangehöriger, Bruder, Sohn.
107. 3. ja, wie; ghanamu, arab.: Ziege.
109. 1. Fa kala, arabisch: und er sagte.
109. 2. kalamu (mit kaf), Stimme, Wort.
109. 3. ghulamu, arab.: Jüngling.
111. 3. bi wajihi, arabisch: beim Angesichte.
111. 4. mursaa = mursala, arab.: der Gesandte.

113. Hayui Izraili
kutwaa roho wayule
illa kwa Mola jalali
kamuamuru katwaa.

114. Ikomapo ahadi ye
muja wa Mola peke ye
hapana shaka roho ye
kutangukana na zia.

115. Na katika kuruani
ulinenee Mannani,
musomao fasirini,
sayo takayowaambia.

Kauluhu taala:

Iza jaa ajalahum la yastakharuna issaa wala yastakadimuna.

116. Hayo kuwaonya, basi.
Shani la Mola mukwasi
mbele yangu mi nafusi,
nilifuete fadhia.

117. Kwangu nisize yakini,
hapana shaka hapana;
Kamwuzeni na nina
mwenyi kiti cha kuzaa.

118. Fa kama fa kharajati
ila ummi subiyati,
mutu mke mwenyi siti,
suyu mamaye sabia.

119. Wakaingia tahakiki,
maneno wakataliki:
essalamu aleiki
ya amati Allahi taala.

120. Yule mbeja huramu
akawarudi ssalamu.
Thumma akatakalamu:
takarabuni rajua.

121. Nisaa fa kalati:
ya mashekhi takarabati,
ilaikum ulhajati
wasalitani ilaya?

---

115. 4. sayo = hayo.
116. 3. mi = mimi.
116. 4. fuete, Perfect von fuata, wie im Yao.
117. 3. nina, seine Mutter (alterthüml.), vergl. das Hererowort ina.
117. 4. kiti cha kuzaa, euphemistisch.
118. 1. 2. arabisch.
118. 3. siti, Schönheit.
119. 3. 4. arabisch.
121. Diese Strophe ist arabisch.

122. Wale wote asahabu
kalamu wakamujibu:
twapenda suyu ngaribu
umurehemu ajaa.

123. Murehemu mutumaini
adheafu masikini,
upate kwenda peponi,
jibu zote utatwaa.

124. Muungu naye takupa,
rehema ye takulipa;
matlaba yetu sapa
ni sayo, tumekwambia.

125. Mtu mke mulimwengu
kauza: iwile tangu
muyile taka ni kwangu,
ambalo lawajibia?

126. Hali ataka dinari
au fedha mashuhuri?
ambalo ali khitari,
mwenyewe kunambia.

127. As'habu wamurudi:
matilaba na muradi:
wataka wako waladi,
aliye kukusalia.

128. Kawauza: nambiani
mwanangu tamutendani?
Wakamwambia: yakini
tamutinda kama huwa.

129. Yuridi yuzibahahu
wa yakhuzu damahu
wa yamusakhu jasadahu
ili kutaka afua.

130. Tamutinda aikinge
damu chomboni atenge
mwilini aisinge,
fa laala akapoa.

131. Nisaa fa kalati,
kavuta yake sauti;
na waliopo ummati
wote wakamsikia:

132. Laula kwamba endi
alifati auladi
bi haki Allahi wadudi
hawa ngawie fidia.

133. Kwa wote ningamupee
hatta wasinisalie
bi wajihi Allahi naye
Muhammadi murusaa.

---

122. 3. suyu = huyu.
124. 3. 4. sapa = hapa; sayo = hayo.
129. 1. 2. 3. arabisch.
130. 4. fa laala, arabisch.
131. 1. arabisch.
132. 1. endi, arabisch: bei mir.
132. 2. auladi, pl. von weled, arabisch: Kinder.
132. 3. bi haki, arabisch.
133. 3. bi wajihi, arabisch: beim Angesicht.

134. Niliridhie, yuani,
mwanangu kamutindeni
mumutabibu mugeni,
fa laala akapoa.

135. Bali zidini kutaka;
ahadi yake hakika
mupate kuyua thika
kupenda na kukataa.

136. Endani hima, endani,
mwanangu kamwuzeni
kama hayo ya mugeni;
kaitwa akayaitikia.

137. Ilana ilinsani
la yarudu furukani,
roho kuawazi nyani
mauti kumukolea.

138. Hako kiumbe asahu
apendaye kusahihu
kufarikana na roho
alihayi akiua.

139. Illa peke mwenyi kuwa
apendalo lote lawa;
kufisha na kufufua
ikali yake afua.

140. Kiumbe buni Adamu
ajali ikiisha timu
hayui kutakalamu,
hawezi kufisha zia.

141. Kulla kilicho hiyati
kitapatwa ni mauti;
thumma baada mammati
mufufuzi tafufua.

142. Twahakiki na maani
yalio musahafuni;
ilmu tafusirini
mkieleza ajaa.

Kauluhu taala:

Kullu nafsi zaikatu lmauti wa nabuluwakum bi shari wa lkheir fitna wa ileina turijeūna.

143. Wale watakao pepo
maneno wasikiipo
walivyokuza: alipo
kijana? Wakamwendea.

144. Fa salamu aleihi
bi mantiki rajihi.
Yule sabihi malihi
essalamu kiwapokea.

---

137. 1. 2. arabisch.
143. 2. wasikiipo = wasikilepo, alterthümliches Perfect.
144. 1. 2. arabisch.

145. Nambiani mutakayo,
kwangu ya wa isiyeo,
sikhofuni, mpendayo
msicheni kuniambia.

146. Tafadhali nambiani,
ndugu, mwisiwe nini?
Wale wambi: ni mgeni
wataka kurehemewa.

147. Murehemu Mwarabu
mgeni suyu ngaribu,
utapata na thawabu
siku ya nyota na ndaa.

148. Asikiyibu kijana;
wote kawauza tena:
ngaribu yake maana,
sitasa kufahamia.

149. Ndugu, nifahamishani
atamanicho mugeni?
kiwa nacho, simuhini
tamupa na kumwongea.

150. Wakanena Waarabu
kwa pole na taratibu;
marithawa ya ngaribu:
taka roho yo kutwaa.

151. Damu yako we hakika
mwilini kiipaka,
maradhi yamutoka
kashukiwa ni afua.

152. Kwa amuri ya Mannani
Mola asiyo kifani
murehemu masikini,
nawe utarehemwa.

153. Asikiyibu ghulamu
waadhi yao kaumu.
Iwile kwamba: naamu
nikubalii makaa.

154. Mugeni suyu naye
kwamba nawa fidia ye,
nafsi nalikirie
na kuzidi kupendea.

---

145. 2. isiyeo, Relativsatz mit alterthüml. Perfect.
145. 4. msicheni, fürchtet euch nicht, von cha, fürchten.
146. 2. mwisiwe, vergl. zu 94. 2.
146. 3. wambe, Perfectum.
147. 2. suyu = huyu.
148. 1. asikiyibu = asijibu; diese Form scheint jetzt nicht mehr vorzukommen.
151. 1. yakowe = yako wewe.
151. 4. shukiwa, vom Himmel her begnadigt werden.
153. 4. kubalii, Perfect, makaa = makala, arabisch: Worte.

155. Nitikie moyo wangu,
nitegemee Muungu;
mupendalo, ndugu zangu,
nimezepita auwaa.

156. Hayano si ya mugeni
wala si yangu yakini,
ni hatti yake Mannani
alionikutubia.

157. Alipendalo Karimu
hapana shaka kutimu,
kiumbe mwana Adamu
angatoa kuridhia.

158. Ambalo alikutubu
Rabbi Muungu wahhabu
haliyati kumusibu,
kiumbe angakataa.

159. Ndiye kudura aziza
kwa kulla yambo aweza;
sipati kuiangaza,
shidda na dhambi katwaa.

160. Hapatasaa hiyati
isiyozuku mauti
illa kamuumba nti
katupa nasi kukaa.

161. Sote waja dunyani
tutaingia mautini.
Kama vile kuruani
alikokutubainia:

Kauluhu taala:

Kulla man aleiha fani wa yabka waiihu rabbūka iljalāli wa ilkerāmi.

162. Hayanifaa khubiri
nia yangu na dhamiri:
nitegemea Ghaffari
mwenyi kunighufiria.

163. Tendani mulipendalo,
kwangu mulitamanilo
nami niridhii kwalo
na kuzidi kupendea.

---

155. 1. itikie, Perfect.
155. 4. Vielleicht ist statt nimezepita ni mezependa zu lesen; meze, alterthümlich statt me. Vergl. zu 167. 4.
160. 1. Was ist hapatasaa für eine Form?
163. 3. kwalo, lo, alterthümliches Pronomen; vergl. die Pronomina im Herero.

164. Niliridhie, yuani,
na damu yangu kingani
na ngaribu mupakeni
atakase yake nia.

165. Basi, sapo wakondoka
jamii wakatoka,
mwana na ishe hakika
mbele wakakadimia.

166. Wakenda wakawasili
mbele za Mikaili,
na malaika Jiburili
wafuetene pamoya.

167. Maa kisha Waarabu
wamwambiapo tabibu:
saya yako matulabu
tumezile kupatia.

168. Suyu ndiye auladi,
mwana wa ajwadi,
kwake hana taradudi
yote tumewausia.

169. Tabibu akaamba: aye
mwana, mwiteni babaye
aye, amtinde yeye;
ndipo yatakapo kuwa.

170. Naye babaye kijana
amutinde dalihini,
na ngaribu masikini
damu amupake zia.

171. Wawangwana ansari
kalamu wakazukuri:
tabibu, mutu hiyari
tenda ambalo lafaa.

172. Maa wamuzungukii
tajiri wakamwambii:
kutinda kushurutii
kwako we mwenyi kuzaa.

173. Tabibu yushurutahu,
ente tazabahahu,
in kana yuridhahu
rehemaka Allahu taa.

---

164. 4. statt nia ist wohl zia, Glieder, zu lesen.
165. 3. ishe, sein Vater, vergl. ihe im Herero.
166. 4. fuetene, Perfect von fuata, wie im Yao.
167. 1. maa = marra.
167. 3. saya = haya.
167. 4. mezile = malizile, alterthümliches Perfect von mala, aus dem die jetzige Tempussilbe me entstanden ist.
168. 1. suyu = huyu; auladi ist eigentlich Plural vom arabischen weled, Sohn.
170. 2. dalihini, scheint ein Pronomen der li-Klasse zu sein.
172. 1. zungukii, Perfect.
Strophe 173 ist arabisch.
173. 4. taa, des Reimes wegen für taala.

174. Akondoka tajiri
ali kutumai kheiri,
mato mayi yakijiri
yakipita na lihia.

175. Papo penyi mukutano
akamwandika mukono,
moyo usikwamba neno
la kufuruni kuingia.

176. Moyo uli kuhimidi
na kushukuru Wadudi;
dhomiriye na fuadi
kuno akinyenyekea.

177. Fa kala lahu sabiyi
akaamba: ewe abiyi
niwia radhi radhiyi
na mi radhi nakuwia.

178. Nipa radhi bwanangu
nanyi kaumu wenzangu,
nenda mbele za Muungu
fa radhi imekutia.

179. Pakakathiri bukayi
kwa maneno ya sabiyi;
matozi yakinga mayi
yakipita na lihiya.

180. Ili kulia yakina
na moyo wa kisonona;
ndivyo zikaumatana
kwa matozi kumuyaa.

181. Yali kulia hakika
matozi kumiminika,
na jamaa kazalika
wote mema wakangua.

---

174. 2. ali kutumai, Aoristform? vergl. 176. 1. uli kuhimidi.
174. 4. lihia, des Versmaasses wegen für lia.
175. 2. in akamwandika bemerke man das Pronomen mu statt u.
175. 3. usikwamba sollte nach jetziger Sprechweise e am Ende haben, doch hat im Yao der negative Conjunctiv immer a am Ende.
176. 4. kuno, altes Demonstrativpronomen.
177. 1. arabisch.
177. 2. abiyi, arabisch: mein Vater.
178. 4. fa, arabisch: und.
179. 4. lihia = lia, vergl. 174.
180. 1. ili, es war; das Pronomen i als ganz neutrales gebraucht, obwohl das Subject kulia ist. Dieser Gebrauch kommt auch noch heute bisweilen vor.
181. 1. yali, es war, alte Copula.

182. Wakalia watu sao
wakaoza nguo zao
kwa yale matozi yao
yaliokuwapitia.

183. Muhadithi aneuee:
tajiri ulizie
hatta mawili matoye
siweze kuyafua.

184. Alizile tajiri
wa damui ikijiri
kama mayi ya bahari
ya nguo zayo kuingia.

185. Ili kupita matozi
katika yake maozi
yakinga mayi mayazi
mwandika maizi mamvua.

186. Kuona kwe huyu mwana
kilio kuliwa sana
atamushile kwa nina
bwana wake akamwambia.

187. Wanenile kiyawiza
bwana wake kimweleza:
sicho kilio nyamaza,
sitamani kuliliwa.

188. Sikia yangu makali,
abui, hati habuli,
unifunge tu rijili
na mikonoi pamoya.

189. Nifunge tu zia zangu
muu na mikono yangu
nakhofia na matungu
nisiye kutaataa.

---

182. 1. sawo = hawo.
182. 4. Man beachte die alte Form des Relativsatzes.
183. 1. anenee, Perfect für anenele.
183. 2. ulizie, Perfect.
183. 4. fua soll des Reimes wegen für fumbua stehen.
184. 2. wa, arabisch: und.
186. 3. tamushile, Perfect von tamuka, nach Art des Yao, nina, vergl. 117.
187. 1. Was heisst kiyawiza? Man will das Wort auch kinyamweza lesen, und dann soll es hier soviel als: barbarische, fremde, unverständliche Sprache bedeuten.
187. 3. sicho = hicho.
188. 2. abui, arabisch: mein Vater.
188. 4. in mikonoi ist das arabische Pronominalsuffix i, meine, an das Suaheliwort angehängt.
189. 2. muu = miguu, Füsse.
189. 4. Was ist nisiyekutaataa für eine Form?

190. Nakhofia na mutambo
roho yangu itwawapo,
ndipo hawambia sapo,
nifungani sana zia.

191. Munifunge iyohini
muu na mikono nane.
Moyo uli na khuzuni
zidi kama auwala.

192. Huzuni ikakalipa,
mato mboni zikakipa,
pasiwe na mambe sapa
na ambao watongowawa.

193. Kiisa babaye, yuani,
akakamata sakini
kamutinda weledani;
yakakoma yakamaa.

194. Akamtinda mwana we
kwa kisu na mkono we
kwa kutumai Moli we
na thawabu kupambia.

195. Wakauka malaika
muda yuu wakafika;
watu wasiyazunguka
wala wasipotambua.

196. Mwele hatta tabibu
wasioneke karibu;
ndimi zao Waarabu
wa kathabiti makaa.

197. Wakaeta mato mwanga
as'habu wakiinga,
wasimwone muganga
wala mwenyi kugengwa.

198. Wakahimidi Mannani
na mutume we amini
wakaamba: hili ni shani,
shani lake mwenyi kuwa.

199. Maa wakaeta shauri,
wale watu mazukuri;
wamwambii tajiri:
himidi Allahi taala.

---

190. 3. sapo = hapo.
191. 1. iyohini, alterthümliches Pronomen.
191. 2. Vielleicht ist statt nane: inne zu lesen. Die Eingeborenen erklären, dass auch noch Augen und Ohren zu den Händen und Füssen hinzuzurechnen seien, um die Zahl acht voll zu machen.
192. 3. 4. Diese beiden Zeilen sind nicht ganz klar; vielleicht ist der Text verderbt.
195. 3. wasiyazunguka, statt dieser conjunctivischen Form wird jetzt nur die indicative hawajazunguka gebraucht; vergl. 234. 2, 236. 4.
196. 4. makaa = makala, Worte.
199. 1. maa = marra.
199. 3. wamwambii, Perfect.

200. Tajiri katanababi
akaamba: inna lillahi;
maa: wa inna ilaihi
rajeuna, akakua.

201. Baadaye iyohina
wakamutukua mwana
wakaeta na ye kwa nina
upindoni mwa pazia.

202. Na waosha wakawasili
wakamwosha filhali;
na wanginewe rijali
kaburi wakifukua.

203. Pali na waungwana
wenyi bafuta kushona;
pasiwe mtu kunena
kwa musiba kukalia.

204. Ziumbe muyi muzima
yali yowe na zahama
kwa kilio cha ghulama
alicho akililiwa.

205. Kilio kikashitadi
kuliliwa auladi,
pasiwe mutu kufidi
kwa huzuni ye kukua.

206. Wakalia insana
wakuu hatta wanona;
pasiwe kusikizana
mmwe kaamba: nyamaa.

207. Ili kutesa matozi
kwa mato yao maozi
kama mvua mitelezi
wingu la samawia.

208. Mama ye yake mauzi
abadi ili matozi,
yakishuka mitelezi
yakipita mifumbia.

209. Turudi nyuma kutunga
mambo yalio kuzinga;
pakiwa mtu mujinga
apate kufahamia.

---

200. 2. 3. inna lillahi wa inna aleihi rajeuna, arabische Formel, gebraucht, wenn man von einem Todesfall hört.
200. 4. in akakua steckt wohl das arabische kala, sprechen.
202. 2. filhali, arabisch: sogleich.
204. 1. ziumbe = viumbe.
204. 2. zahama, arabisch: Gedränge, Getümmel.
205. 4. kukua, des Reimes wegen für kukuu, gross.
206. 4. mmwe, einer, vergl. Herero umwe; akaamba, scheint negativer Conjunctiv zu sein, die Form ist wie im Yao gebildet.
208. 2. abadi, arabisch: anfangen.
209. 2. in dem Relativsatz yaliokuzinga ist das Infinitivpräfix noch erhalten. Man kann daraus ungefähr sehen, wie die jetzige Relativform entstanden ist, vergl. 212. 4.

210. Tutunge ya malaikani,
waliokwenda mbinguni;
khabari tu zibayini
wakiisha kusikilia.

211. Wakiisha fika pambee
Jiburili unenee
akimurudi nduguye
kuno kimukariria.

212. Kamuuza filhali:
ewe ndugu Mikaili,
iiweneye suali
tuliyokushindania?

213. Uiwene shufakati
na ruhuma ya umati?
Fa kala malaikati:
niiwene, Jiburiya.

214. Niliiwene ruhuma
na shufaka na rehema;
hatta siku ya kiyama
takweta kushuhudia.

215. Kiisa ambi Mikaili
amwambii Jiburili:
Muombe Mola jallali
ukiomba na tumaa.

216. Muombe Mola wahabu
ahuike Mwarabu;
dua yo mustajabu
enda Allahu taala.

217. Muombe Mola wadudi,
afufuke auladi,
wasitarehe fuadi
wenyi kupenda fadhia.

218. Tenda hima Jiburili
kumulingana Jalali,
asa ikawa kabuli
dua yako ikapaa.

219. Na wende we maarufu
mbele za Mola sufufu
muombe Mola latifu;
uombalo lakuwia.

---

210. 1. malaikani, arabische Dualform.
210. 4. kusikilia = kufikilia.
211. 1. pambee = pambele.
211. 2. anenee, Perfect = anenele.
211. 4. kuno, alterthümliches Demonstrativum.
212. 3. iiwene, Perfect von ona, das angehängte ye ist wohl die Fragepartikel: wie?
212. 4. vergl. 209.
215. 1. ambi, Perfect.
216. 4. enda, arabisch: bei.
217. 4. fadhia = fadhila.
218. 3. asa, arabisch: vielleicht.
218. 4. paa = panda.

220. Baada sayo makali
wakashuką o wawili,
madina wakawasili
kama vivile auwaa.

221. Wakashukia madina
wali tariki nyingina,
sura zisikufanana
kama walizoshukia.

222. Kwingia kwao muyini
wale waja wa Mannani
wakaenda mosketini,
kule kuliko na taanzia.

223. Kupita wakakeleti
kavuta yake sauti;
wakutene o umati
salamu kawenekea.

224. Salamu kawakariri,
maa kiwapa khabari:
ngaribu musafiri
saasa tuanza kungia.

225. Thumma akatakalama
Jiburili akasema;
ni nani mwenyi taama,
na taama ni ziliwa.

226. Nani anipao kuti,
kala, hanusuru hiyati,
haepukana na mauti
na ukalifu wa ndaa?

227. Nyani mungi wa ruhuma
atendeao Karimu?
Nyani apenda uzima?
kesho kwenda kumufaa.

228. Ambao kula hashiba
na mayi, walau haba,
wepukana na ukuba
ni pepo kuenda kuzua.

229. Nami leo iyatimu
siku tatu mazumumu,
sijui kula taamu
na taamu ni ziliwa.

230. Mualimu Jiburili
akiisa yake kauli,
iwile kuima rijali
nyumbani akamukoa.

231. Fa kala: akalingana
babaye yule kijana
kamwambia musijana
yule mamaye sabia:

---

220. 2. wakashukao, wohl aus wakashuka wao zusammengezogen
221. 2. des Reimes wegen nyingina statt nyingine.
221. 3. Man beachte die alte Form zisikufanana.
223. 3. wakutene, Perf. von kutana, wie im Yao.
223. 4. kawenekea = kawaenekea.
225. 4. ziliwa = viliwa, was gegessen wird.
226. 1. kuti, Speise, in Lamu, aber nicht in Sansibar gebräuchlich
227. 1. nyani = nani.
228. 1. ambao = anipao.
228. 3. wepukana = waepukan.
231. 1. fa kala, arabisch: und er sprach.

232. Ewe mtu mke wangu
nakwambia, shika langu
mupe fadhili Muungu
mupayi asiyepewa.

233. Ondoka wende nyumbani,
ziliwa uzizaini,
uwaletee wageni
sawa wa maziwa kunwya.

234. Katwae hima haraka
kabula tusiyazika;
uje nazo na kwandika,
tutumai afdhaa.

235. Yule mamaye ayali
kaenda kwa tashili;
muda punde filhali
akaya nazo ziliwa.

236. Akaondoka jeo sizo
ziliwa akaya nazo
papo akawandikia zo
pasiyapita muhaa.

237. Kupewa kwe takirimu
Jiburili mualimu
ili kuuza, fahamu,
ngaribu kumamkua:

238. Ewe babaye gholamu,
tule mi na we taamu
isitawi takirimu
izide tu kutangaa.

239. Yule mungi wa akili
kamwambia Jiburili:
Kēfa ana akuli
wa kod mata buniya?

240. Nalifiliwa ni mwana
hatta siyazika ina,
waniradhi waungwana,
na mi radhi nawawia.

241. Ziawaye kula kuti
wa ibnu kod mati,
hatta haenda tiyati,
kuzika hatuyamaa.

242. Jiburili akakuli
akamweleza tajiri:
zidi moyo kusubiri
na saburi ndiyo taa.

243. Mwema, ata na huzuni
na khofu toa moyoni;
mwana alikwitwa nani
jina la mwana niambia.

---

234. 2. tusiyazika, vergl. 195. 3.
234. 4. afdhaa = afdala, bessere.
236. 1. sizo = hizo.
236. 4. pasiyapita, vergl. 195. 3.
238. 2. mi na we, ich und du.
239. 3. 4. arabisch.
241. 2. arabisch.

244. Tajiri katakalamu:
jina le ni Kasimu.
Jiburili kafahamu
ismu ikamwelea.

245. Katamuka Jiburili
akamwomba Jallali,
ulimi wakaratile,
dua Rabbi kapokea:

246. Ya kadhi ilhajati
ya mujibu daawati
ya muhiyi ilamwati,
wa ahayaa sabia!

247. Ya muhuyii ilithama
basiri mutakalama
ahayaa Kasima
mithli kama auwaa.

248. Na kulio illatifu
kudura yo maarufu
upapo in Nuni na Kafu
utakalo lakuwia.

249. Na katika kuruani
mwisoni mwa Ya Sini.
kudura yako Mannani
alikokutubia:

Kauluhu taala:

Innama amuruhu iza irada sheian an yakūl lahu: kunu, fa yakūn. Fa subhāna allazi biyadihi walkuwatu kulla sheian wa aleihi turjaūnu.

250. Maa atakalamu
Jiburili mualimu:
kumu, ente Kasimu
niyakwita nialia.

251. Kumu, ima, tulingane,
uwe kitako, tufane,
watu wote wakuone
uli hayi ukiua.

252. Ima, Kasimu, ima,
tule mi na we taama
kwa fadhili za Karimu
muumbe akiumbua.

253. Akaima kulingana
akahuika kijana
kwa izini ya Mannana
wa bi haki mursaa.

---

244. 2. le, für das jetzt gebräuchliche lake.
246. arabisch.
247. arabisch.
248. 3. in Nuni na Kafu, die Suren 68 Nun und 50 Kaf.
249. 2. Ya Sin, die 36. Sure.
250. 3. arabisch.
251. 1. kumu, stehe auf, arabisch.

254. Kiisa kwima, pulikani,
akawaegema wageni
kajilisi kurusini
pamoya na kutulia.

255. Akakeleti ghulama
na malaika muathama;
babaye katabasama
furaha kamwingia.

256. Baathi ilulamai
walihukumu sabiyi
kabla ilahayai
waliokufa sabia.

257. Hakuzumbuka Kasima
nduuye sita wasiima.
Ndio asaha kalima,
wote wakasahihia.

258. Waliokufa auwali
kwa wote wakawasili
naye Kasima, wayule,
nyuma akawandamia.

259. Wakimaa kukutana
sabaa zao zijana,
iwile kuuka tena
Mikaili na Jiburiya.

260. Wakauka wakenenda
juu la bingu wakaenda,
na kuti iliotendwa
ikalishwa fukaria.

261. Kiisa kaamba Jiburili
kamwambia Mikaili:
Kefa dunia hali?
i hali gani dunia?

262. Shufaka uionee
pamoya na rehemaye?
Mikaili akaamba: ae
mato yamejionea.

263. Pa na zema, Jiburili,
ya kumkhofu Jallali,
niswani na rijali
hawakuasi Jalia.

264. Bali akheri zamani
watakuya insani
wasio shufaka moyoni
aduwi za Mola taala.

265. Mualimu Jiburili
kaamba: naam, ni kweli,
asahi il akwali
yako, yatatekelea.

---

256. 1. arabisch.
259. 2. zijana = vijana.
260. 1. uka = ruka.
261. 2. arabisch.
262. 1. uionee, Perfect.
265. 3. arabisch.

266. Mwana na ishe na nina
nyoyo haitapendana;
kiisa itakuwa zina
na haya kupunguliwa.

267. Zina itawapendeza,
nikaha itatukiza;
lenyi tama ua mayaza
wazidi kupendelea.

268. Sala za Mola jallali
ipewizo mirusala
moyo haitakubali,
sijidi kupumukia.

269. Ai zambi na malama
itakayo kuya nyuma.
Ai akheri iluma
ai watu majuhaa.

270. Nasi tukiyafikiri
kwa mato tukibusuri,
ya Jiburili, khabari
yote imetekelea.

271. Kuliko zamani zetu
ndiswi wawao watu
hatukubali Moletu
hatufikiri rasua.

272. Tushushiwe amwali
kutuma kwa kuizili;
tusahawiwe Jalali
na mauti kutuyia.

273. Ibilisi ishsheitani
aduwi wake Mannani
wamutozile mwa ndani
kuzidi kuikumbia.

274. Allahumu mwawazi
tuokoe, ndiwe mwokozi
utufunge kwa majazi
yako tumai shufaa.

275. Tufufue na salati
na saumu na zakati;
sote jamii umati,
tuoneke na shufaa.

276. Watufufue tu na dini,
nyoyo ziwe na imani
tusifiwe kuruani
na ilimu kutambua.

---

266. 1. ishe, sein Vater; ina = nina, seine Mutter, vergl. im Herero.
268. 2. ipewi, Perf. von pa.
269. 4. majuhaa, statt majuhala.
272. 1. tushushiwe, Perfect. Passivi, ebenso 272. 3. tuhauwi
274. 1. Allahumu, arabisch: wörtl. ihr Gott, ist hier angewan indem auf die Bedeutung des Pronominalsuffixes, das d Suaheli doch nicht ganz verständlich ist, weiter ni geachtet wird.

277. Tufufue na shahada
na kulla penyi ibada
kwa abadi mukhaladi
waja wa Mola auwaa.

278. Tufufue na bashiri,
kipendo chake Jabbari,
tusiate kuzukuri
na shahada kuitwaa.

279. Iwe tama kaburini
na haja ya siratini,
tuwe nyuma ya amini
kulla ambapo aingia.

280. Haya namba mi Latifu
naye mwenyi kusanifu
na wasome kwa lutufu
tuwasikize makaa.

281. Aingiapo mukarimu
fi janna innaimu
tujaaliwe kaumu
sote kueta kwingia.

282. Tujaalie Ghaffari
na mauti ya nazari;
zambi ziwe maghafuri
tusionane na baa.

283. Ambalo walikataza
tuyepue nalo Mweza,
tusionane na giza
kwa akhera na dunya.

284. Ambao ni muselimu
Rabbi Mola murehemu,
mupunguze na jahimu,
apate mema makaa.

285. Tama, basi, akwamu,
hadithi kuihitimu.
Sasa nanyi waalimu
somani mukisahia.

286. Ningatunga sitambui,
maana sifafanui
kwa sheitani aduwi
mwenyi kutushawishia.

287. Si nyuvi wa lufati,
si mwelefu wa bayiti,
si mkondofu wa khatti,
kwa hamu kwa mashangaa.

288. Si na raha ya dunia,
si na laza ya zinua,
akili haikutua
kwa shidda kunikolea.

289. Si mjuvi wa ilmu
zuo sikutaalamu
na sayo kuwahikimu;
nawaambia hiwambiwa.

---

277. 4. auwaa = auwala.
280. 1. namba mi = na nipa mi.
281. 2. janna innaimu, arabisch: der Garten der Annehmlichkeiten.
285. 1. akwamu, arabischer Plural von kaumu, Leute.
287. 2. bayiti, arabisch: wörtl. Haus, dann Strophe.
289. 2. zuo = vyuo, Bücher.
289. 3. sao = hawo.

290. Hali yangu ni ghulama
tangu zamani za nyuma
msiambe nikuisema
hasha sikuogopea.

291. Na mukitaka yakini
nasabu kutabayani:
Aluwi buni Hasani
shajara li hadithia.

292. Hasani buni Aluwi
Fatuma rasulii
tangu jaddi mufadhiyi
aliye kumuyukua.

293. Kuliko zamani hizi
hazimukhofu azizi,
kazi yao ni uzinzi
jamii kupendelea.

294. Amuri ya Muhammadi
ambaye ni maadudi
hawawezi kuihidi
jamii aliopotea.

295. Rabbi tuokoe tuokoke
sote waume na wake,
twambe, tunene, tuitike
tuwe watu afdhaa.

---

292. a. Statt Fatuma steht im Manuscript Fataha, was mir aber keinen Sinn zu geben scheint.

Utenzi wa mi'iraji.

(Das Gedicht von der Himmelfahrt Muhammeds.)

Bism illah irrahman irrahim!

1. Nianze kunuthumu kwa isimu yake Karima
Mola muathamu mtukufu mwenyi rehema.
Hazina ukomo sifa zake mwenyi ithama.
Sala na salamu na bawazi zenyi tuma.

2. Tuma na sahaba waondoke watusalie
tunali miradi miongoni mwao tuingie.
Siku ya kiyama wasimame watuombee
tupate wokovu siku nzito ya jehannama.

3. Basi, nikomile, sikithiri muno dibaji,
kwani ni na mambo nayapenda kuyadiriji.
Ni hadithi ngema ya usiku wa mi'iraji
yake mwenyi jaha, mupandisha yuu la sama.

4. Alipowadia Mola wetu kuthihirisha
jaha ya nabia Jibrili ilimushusha.
Tuma alilele, kamwendea kamwamsha:
ondoka silale, Mola wako akwita hima.

---

1. 4. zenyi tuma, welche sich auf den Propheten beziehen.
2. 2. li, bezieht sich auf miradi, Wille, statt lo.
3. 1. nikomile, Perfect von koma.
3. 4. Object zu mupandisha ist wohl Boraki, vergl. Strophe 5.
4. 3. alilele, Perfect von lala.

5. Alipoamka mwombezi akapasua
kifua na nyongo zote ghashi akazitoa.
Akiisha kushona kana kwamba hakupasua.
Aoni Boraki mbele yake amesimama.

6. Jibrili kaamba: Mola wako akusalimu
tumiwe kukwita kwenda nawe kwake Karimu.
Upande Boraki wewe hima utakaddamu!
Boraki katupa Jiburilu katakallamu:

7. Simo, kigeuke kipendo che Mola karimu!
Kaamba: mkono we ushishie muwi sanamu.
Ndipo hakataa kunishika yake jisimu
Jibrilu kaamba: mtukue kipendo chema.

8. Kaamba: marihaba, kutukua ndio adabu
nami nayajua, yanielea yenyi sawabu.
Bali ni na yambo nami kwake nalitulubu
dhamana ya pepo kuniweka mahala pema.

9. Boraki kwona mambo yake yote kutimu
kumdhamaniye mwombezi wake Karimu.
Akanika kitwa kwa furaha na tabasamu;
tuma kamupanda akaomba Mola karimu.

10. Kwenda kwe rasuli akafika pake medina
Jiburilu kaamba: shuka hapa mwombe rabbana.
Sali taraka'i raka'āti mbili za suna
kisa umwetee Mola wako mateo mema.

---

5. 4. aoni, Perfect von ona.
6. 2. tumiwe, Perfect von tumwa.
7. 2. ushishie = ushishile, Perfect von shika.
7. 4. Im Manuscript steht kema.
9. 2. dhamaniye, Perfect von dhamana.
9. 3. akanika = akainika.
10. 4. umwetee = umletee.

11. Kisa wakenenda wakafika Turi Sinina,
Jiburilu kaamba: sali hapa tuma amina.
Ndipo pa munaja wake Musa buni Amrana
palikuwa shani ya maneno yake Karima.

12. Kisa wakenenda wakafika Betilahamu
alipozaliwa tuma Isa buni Mariamu.
Jiburili kaamba: Sali hapa utakadamu
muombe rabbuka sapa ndipo mahala pema.

13. Kiisha wakenenda wakaona jinni shadidi
na kinga cha moto kumulika tuma sayidi.
Jibrilu kaamba: soma dawa, omba Wadudi;
tuma akasoma, ifriti likazizima.

A'úzu biwajih Illah ilkarīm wa bikalimāt Illah ittammati allati la yujawizuhunna barru wala fājirun min sharri ma yanzilu min essamāa wa ma ya'ruja fiha wa min sharri ma dharaa filardh wa min sharri ma yakhruju minha wa min fitan illēli wa nnahāri wa min tārik illēli wa nnahār illa tarikan yatruku bikheiri. Ya rahmāni.

14. Kiisha wakenenda, mambo mangi wakayaona,
wakaona watu, wakiyaa punde huvuna.
Jibrilu kaamba: watu sao mujahidina;
wendao jihadi wajaziwe majaza mema.

15. Kiisha wakenenda wakanuka 'arufu jema,
Jibrilu kaamba: ni 'arufu ya mke mwema.
Kimutana nywele mke asi asiohuruma
binti Fireuni kafiri mbi asiosilimu.

---

11. s. munaja, arabisch: Platz vertraulicher Besprechung.
14. s. sao = hawo.

16. Siku ye kitani kikanguka akalingana
binti kanena walaini baba kwa nina:
hali u na Mola mwenginewe wamubaini.
Kaamba Mola wangu ni muumba nti na samaa.

17. Khabari zikaenda Fir'uni akasikia
akawakusanya mke mwema na wana we pia
katika mafuta moto ndani masufuria.
Ndio 'arufu ye inukayo ya watu wema.

18. Kiisha wakaona watu wawi wakisukuma
wakipondaponda vitwa vyao nyundo za chuma.
Jibrilu kaamba: ni wazito wa sala kima
kawana wakati, sala zao kaziwe tama.

19. Kiisha wakaona watu wa mbele na nyuma,
wa na vitambaa za firaka wala za kuma.
Jibrilu kaamba: watu sao si watu wema
kawatoi zaka, mali yao ya jehennamu.

20. Kiisha wakaona watu wawi wakila nyama
biti, wakiiata nyama bivu ilio ngema.
Jibrilu kaamba: ni wazinzi walipokoma
wake na waume wazingao usiokoma.

21. Kiisha wakenenda wakaona mti ndiani
kupasua nguo apitaye hana amani.
Jibrilu kaamba: ni wakazi wa vingojoni
watendao ndia, jaza yao ni jehannamu.

---

17. 2. Im Manuscript steht waze oder wane, ich glaube richtig wazee gelesen zu haben.
18. 3. kima = kuima?
18. 4. kawana = hawana. Kaziwe, neg. Form.
19. 2. Statt wala za kuma ist vielleicht wa lazwa koma zu lesen, aber ich kann mir beides nicht recht erklären.
20. 2. biti = bichi, roh.
21. 3. vingojoni, soll so viel wie fitina, Verleumdung, sein?

22. Kiisha wakenenda wakaona mto, wamu
muna watu ndani wangilie wakila sumu.
Jibrilu kaamba: watu sao wala haramu;
ndio jaza yao wajaziwe kesho kiama.

23. Kiisha wakenenda wakaona mutu zalili
hutaka jitweka haiwezi tweka thakili,
kuzidia tena kuongeza haihimili;
Jibrilu kaamba: ni amana katika zima.

24. Kiisha wakenenda wakaona watu shakiya;
wakikata ndimi kwa makasi zikirejea.
Ndio hali yao wakatapo ndimi komea.
Jibrilu kaamba: ni waongo washo kalima.

25. Kiisha wakenenda wakaona watu shururi;
wapapura nyuso kwa makucha yao sughuri.
Jibrilu kaamba: ni wambao watu jairi
siku ya kiyama nyuso zao kazina nyama.

26. Kiisha wakaona tundu ndogo kama kunazi,
akatoka ngombe kuregea tena kawezi;
Jibrilu kaamba: anenaye asimaizi
kunena maneno akayuta yanda kwima.

---

22. 2. wangilie = waingilile, Perfect.
23. 4. zima, Jude oder Christ, der unter den Moslemin lebt.
24. 2. rejea, eig. zurückkehren d. h. zum geöffneten Zustande.
24. 4. washo = wasio?
25. 3. Im Text steht khiyari, was keinen Sinn giebt.
25. 4. kazina = hazina.
26. 1. kunazi steht deutlich im Manuscript, aber vielleicht ist es ein Schreibfehler.
26. 2. kawezi = hawezi.
26. 3. maizi, unterscheiden, trennen, verstehen.
26. 4. kwima = ku-i-mala?? oder = kwema?

27. Kiisha wakenenda wakaona wangwa tawili
na masauti ngema na harufu isho methili
Jibrilu kaamba: sikiliza tuma rasuli
sauti ya pepo yalingana Mola karima.

28. Rabbi nawataka watu wangu nawatamani
ni neema nyingi nawangoja wayao lini.
Mola kamwambia: ni wako we kulla mumini
wake na waume uwadai nyingi neema.

29. Kiisha wakenenda wakaona wangwa wa hari,
kasikia sauti mbaya mno kama himari,
na harufu mbaya, kaihimili mwenyi saburi.
Jibrilu kaamba: ni sauti ya jehannamu.

30. Yalingana rabbi na uzika kwa nyingi hari:
Nataka shururi watu wangu, watu wa nari.
Mola kamwambia: ni wako we kulla jabbari
wake na waume waasiyo Mola karimu.

31. Kiisha wakenenda wakaona nguzo ya nuri
imetukuliwa malaika wake bashiri.
Jibrilu kaamba: wamuriwe kuikariri,
nguzo ya imani kuiweka nti ya samaa.

32. Kiisha wakenenda kasikia mutu kinadi;
tuma kanyamaza asitake yake miradi.
Jibrilu kaamba: usubie ndiye yahudi
lau witeshile wangawile watoto kama.

33. Tena kasikia mlingane jiha shemali
tuma kanyamaa asitake yake makali.
Jibrilu kaamba: ni nasari moja dhalali
ataka asiza umati yo tariki ngema.

---

27. 4. lingana, eig. gleichkommen, dann: sich an jemand wende
29. 3. kahimili = hahimili.
31. 3. waamuriwe, Perfect.
33. 2. Im Manuscript steht statt asitake: asitike.

34. Kiisha wakenenda wakaona muke muzuri
yuvee libasi na kholia za tafakhuri.
Jibrilu kaamba: ni dunya yenyi ghururi
kuonyesha wema thahirini, ndani ni tama.

35. Kiisha wakenenda wakaona mutu shaibu,
akimulingana mwombezi asimujibu.
Jibrilu kaamba: ni adwi yako habibu
ndiye Ibulisi maleuni ndiye rajima.

36. Kiisha wakenenda wakaona mitume pia;
wakimuwatia salamu ngema tamia.
Kiisha wakafika nyumba kuu, wakaingia
baiti mukaddasi, nyumba kuu yenyi athima.

37. Walipowasili moskiti wenyi baraka
wawene nuru jiha mbili zikimetuka,
moja mihirabu Daudi ya mushabaka,
ya pili ni nuru kaburi ya Mariama.

38. Wakaingia ndani wakasali rakaatani,
wawene mitume ikutene mosketini.
Jibrilu thamma akainuka akaazini
akakimu sala, wasijue nani imama.

39. Jibrilu kaamba: tangulia, ndiwe imamu;
mitume i nyuma yako, mbele utakadamu;
saada ni yako na heshima na taathimu,
ndiwe muteule mwombezi wa wote wema.

40. Wakiisha kusali kulla mtu kazukuru
sifa zake Mola na neema akishukuru,
wakajifakhari kwa zipewa zake ghafuru
sifa zake tuma zizidie zao mituma.

---

34. 2. yuvee Perfect von vaa.
38. 2. ikutene, Perfect von kutana.

41. Akashika nyota muungamo, zikaja ziombo
na zi na maji na asali na tamu tembo
kakhitari ziwa mwombezi, kasibu ombo
ombo wa imani taufiki yake karima.

42. Kiisha ikashuka mi'iraji yake peponi
ipambiwe fedha na dhahabu na marijani;
akapanda tuma na amini hatta mbinguni
wakabisha lango wakaitika watu wa sama.,

43. Wakaamba: ni nani mwenyi nuru, zenyi sama?
Jibrilu kaamba: muombezi wawi na wema.
Wakaufungua kwa haraka na himahima
wakamulakia kwa heshima na taathima.

44. Tuma kamwona babu yetu, tuma Adamu
roho za zurriya kaonyesha kazifahamu;
iwapo saidi roho ngumu, katabasamu
kulia iwapo roho mbovu ya jehannama.

45. Akaanza salamu muungamo; akaratile
kaamba: marihaba mwana mwema tuma rasuli
saada ni yako mwenyi jaha, ndiwe auwali
ndiwe mwenyi mbele na mitume yote i nyuma.

46. Kiisa wakaingia wakafika wingu wa pili;
kubisha vivile na kwitika kama auwali;
Amwene Isa na Yahya wote wawili
sura zao moya mufano we wana wa mama.

47. Kaamba: salamu; wakainuka kumondokea
kwa kumuathimu na heshima na kumutia.
Walipoagana wakaingia wakafikia
uwingu wa tatu wakabisha kwa taathima.

---

41. 2. na zi = nazo.
41. 3. 4. Möglicher Weise ist hier der Text verderbt.
42. 2. ipambiwi, Perfect.
44. 3. roho ngumu, im Gegensatz zum folgenden roho mbovu, eine gute Seele.

48. Wakaitikiwa: marahaba mwenyi athama.
Uwene sadiki Yusufu na sura ngema;
akaanza salamu muungamo, ndio heshima.
akakaribisha akaweka mahala pema.

49. Kiisha wakafika wingu wa ne kwa taisiri,
Jibrilu kaamba: funguani babu bashiri.
kaamba: marihaba pita naye, pasiusiri,
saada ni yake muombezi kiumbe chema.

50. Alipowasili kalakiwa na Idirisi,
ni yake makamu wingu wa ne pake julusi.
Kaamba: marahaba ukunduke utanafasi,
saadi ni yako mwenyi jaha isiyokoma.

51. Kiisha wakaingia wakafika wingu wa tano;
wakaingia ndani wakaona nabii Harunu;
kawakaribisha kwa heshima tukufu muno,
wakaomba Mungu kuagana kwa dua ngema.

52. Kiisha wakaingia mwombezi na Jibrili
wa sita uwingu wakafika wote wawili.
Wakabisha lango kwa heshima na tabujili,
wakafunguliwa wakaona Musa kalima.

53. Wawene jeshi yake Musa imekingama
akambiwa tuma: inua kitwa ukitazama.
Kaona na jeshi, hatambui ilipokoma.
Kambiwa: jeshi uonayo ni yako tuma.

---

48. 2. uwene, Perfect von ona.
49. 3. usiri, Schwierigkeit finden.
49. 4. Im Manuscript steht kema, vergl. 7. 4.
50. 1. kunduka = kunyuka, sich entfalten, sich von der Anstrengung erholen.
53. 1. wawene, Perfect von ona.

54. Kamwona Musa umbo lake ili la nyama,
yu na nyele nyingi zisimeme za tomatoma,
katoa salamu mwombezi kutakadama.
Musa akajibu: marihaba, bi akhi mwema.

55. Ndiwe ndugu mwema mwombezi wa watu jama
na wako umati afudhali yote uma;
wendapo kwa Mola wakipewa yake karama
nasi tukumbuke ngatujali wako khuddama.

56. Kiisha wakangia wakafika wingu wa saba.
Jibrilu kaamba: nimekuya naye habibu,
fungua mulango akapita tuma ye rabbi.
Wakaufungua akapita tuma karima.

57. Akaona mtu mwenyi jaha kuu jalili,
kauliza tuma: mtu gani? Kaamba: Khalili.
Mwandani we Mola ndiye jaddi yako asili
kamupa salamu yake jaddi Iburahima.

58. Kamukaribisha kamwambia: jaha ni yako,
ai mwombezi, wakhubiri umati wako
wapande mipando ya peponi waweke peko
na mipando ya usubhana hatta ilathima.

Subhana Allahi wa lhamdu lillah, wala ilahi illa allahu, wallahu akbaru. Wala haulan wala kuwatan illa billah ilali ilathimu.

59. Na hapo alipo pana watu weupe mno
kama karatasi na wengine matangamano
wangii matoni wakiunga wawa mfano.
Tuma akanena: watu gani wenyi heshima?

---

54. 2. zisimeme, Perfect von simama.
54. 4. bi, d. h. mit den Worten.
59. 3. Statt matoni ist vielleicht motoni zu lesen.

60. Jibrilu kaamba: watu sao ja karatasi
ndio watu wema, kawatendi mambo jasisi,
na sao wengine tengee na wasiwasi
watendao mawi, wakutubu wakawa wema.

61. Kiisha wakangia wakaona hapo walipo
beiti maamuri iwashiwe tini mwa pepo,
wakaingia ndani wakasali wawene sapo
zikwi sabuini za malāka, vyumbe vyema.

62. Na adadi siyo kulla siku kuingia ndani
wengine wengine kwa zamani zote na hini;
wazuru baiti maamuri, ni yao shani,
kulla azuruye atokapo kurudi nyuma.

63. Na mwazini wao Jibrilu ndiye amini
na imamu wao Mikala mwenyi wazini,
siku yao juma kusalisha rakaatani;
wakiisha kusali kumwomba Mola karima.

64. Dua ya amini wazinio kuwaombea
na Mikala mwa imamu kushufa'iya,
na wote jamaa maamuma kuwawania,
dua makubuli zipaazo yuu la sama.

65. Kiisha wakaingia kursiye wakaendea,
daraja ya nane mi'iraji ya nuru pia
penyi sidirati muntaha wa mambo pia;
wawene ajabu nyingi muno isiokoma.

---

60. 1. sao = hawo.
60. 2. kawatendi ist negat. Perfect.
60. 3. tengee, Perf. von tenga, anfangen; dies Wort scheint jetzt im Suaheli nicht mehr gebräuchlich.
62. 1. siyo = hiyo.
62. 4. zuru, die Pilgerfahrt nach einem heiligen Orte machen.
64. 3. Die Gemeinde, die hinter dem Imam steht, wörtlich die, denen vorgebetet wird.

66. Wawene tini mwe mito mine yote yajiri,
mai na maziwa na asali, wa ne khamuri,
na kunazi zake tamu muno kama sukari,
jani lake moya lafinika wote umama.

67. Hakuna mweza kusifu kattu hakuna,
illa Mola wetu mwenyi ezi kuu rabbana,
apendalo kuwa ni amuri: kun! fa yakūna!
Akaugeuza, wasiweze kuutezama.

68. Kiisha kauona mto wake tuma bashiri
athiya ya Mola na ina le ni Kauthari,
wakaufuasa kuwandama yake athari
wakafika nyumba ngema yenyi neema.

69. Wakaona mambo ya vyumbe wasioona
wala kusikia kwa khabari wenyi kunena,
wala muyawaza kwa moyo kattu hakuna;
wawene langoni yandishiwe hadithi ngema.

70. Sadaka ni moja kwa ashara ndio jaza ye,
na kumi na nane yuwambiwa akiridhiye
mutaka karadha kutakayo kwa dharura ye.
Mwomba sadaka kuombayo ali na nema.

71. Akaona pepo, mufano we hakuiona
ipambiwe fedha na dhahabu kwa marijani
na zambarujudi na yakuti yenyi launa
na nau'u nyingi za hariri ngema naima.

72. Kiisha wakatoka kaonyesha moto mukali
kaona vituko vya adhabu hakuhimili,
kwa kosa fahamu ikazulu yake akili,
Jibrili thamma kamudhumu akafahamu.

---

66. 3. kunazi sind die Früchte des sidirati, des Lotosbaumes.
67. 1. Im Manuscript steht mwoza; kattu, völlig, durchaus.
67. 3. kun! fa yakūn ist arabisch.

73. Daraja ya kenda akaingia tuma Bashiri,
Jibrilu kwenda hakuweza kutaakhari.
Akaamba: siwezi kwenda mbele hatta shibiri,
sapa ndipo pangu, mwombezi katakaddamu.

74. Pakaja kiwingo cha rehema yake Jalili,
kikamufunika mwombezi tuma rasuli.
Tuma kamambia: haja gani yako khalili
ambayo wataka niusia kwake Karimu.

75. Jibrilu kaamba: haja yangu niitakayo,
siku ya sirata niwe kinga ya umati yo
ninyoshe mabau yawe kinga yazawa nyayo,
wasiopatie moto harri ya jehannamu.

76. Kiisha akaingia rafirabi ikenda naye
kapita hijabu zote pia kamwoa naye
Moli wa taala, basi, kefa hayo matayo,
walabasi aina pa kimiya wala makama.

77. Mola yumwene kwa mato ye yote mawili,
akaanza salamu tahiyatu yake Jalili.
Mola kamujibu: na salamu yako rasuli,
ndiwe muteule wakuwekwa mahala pema.

78. Alipomwona Mola wake ka na methili,
asiweze neno kutamuka yake kauli;
akenda sijidi. Kamwambia Mola jalili:
omba utakalo utapewa yote timama.

79. Akaamba: Moli wa, muja wako Iburahimu
ni wako mwendani, nami ni na yangu sehemu.
Mola kamwambia: ni watuma wangu fahamu
ni kipendo changu afudhali ya wote tuma.

---

76. 3. Moli wa = Moli wangu, mein Herr; vergl. 79. 1.
78. 1. ka na = ha na.
79. 2. Statt nina vielleicht sina??

80. Kaamba: tumupele Daudi yake zaburi,
na Suleimani kumulika jini na tiri;
nawe ni auwali ya mitume, ndiwe akheri
nizukuriwapo na isimu yako i nyuma.

81. Nakambia Isa akipoza kulla kilema
na kuwafufua wafieo yake kalima;
nawe nikupele kufungua na mangi kamma
ni yako kanizi ya arishi isiyokoma.

82. Na waumati wako afudhali kuliko pia,
siku ya kiyama utakuya kushuhudia;
pindi ukanapo makufari wote na pia
hawakutabia mambo yao walio tuma.

83. Ai mwombezi wa auwali hatta akheri,
mwombea umati siku nzito ya mahashari;
siku ya sirati kutandika yuu la nari,
ndiwe muombezi siku hiyo wawi na wema.

84. Sayo upeweyo, haku mtu aliyepewa;
uhimidi kwayo ushukuru zangu zipawa;
nikufaridhie khamsini sala tukuwa,
wewe na umati kulla siku sali timama.

85. Hijabu ya nuru ikaondoka; akarejea
alipo amini Jibrilu akafikia.
Wakashuka wote wakaona Musa nabiya,
akamkhubiri khabari ye hatta kukoma.

---

80. 1. pele, Perfect von pa.
81. 2. wafieo = wafileo; file, Perfect von kufa.
81. 3. Ist nicht ganz klar.
84. 1. sayo = hayo; upewe, Perfect. Pass. von pa.
84. 2. zipawa = vipewa.

86. Musa kamwambia: umati o kawahimili,
sala khamsini kulla siku zawathakili;
regea kwa Mola, umwombe yake fadhili,
akupunguzie, ni dhaifu wako kaumu.

87. Tuma karegea na munaja wake Karimu,
akawaombea takhafifu wake kaumu.
Akapunguziwa sali tano kazifahamu.
Kafika kwa Musa, kamwambia: regea tuma:

88. Omba takhafifu kwa Moli o, Mola latifu.
Ikawa kwenenda na kurudi kuikalifu,
hatta akapungua sali tano za takhafifu.
Mola kamwambia: uridhii yangu hukoma.

89. Kaone asili ye sala tano katamukeni;
wambao thawabu sala kumi twaa yakini;
ndio hesabu ye sala tano kwa khamusini;
kalitabadali neno lake Mola karima.

90. Mwenyi kunuwia kuitenda amali ngema
hupewa hasana kwa fadhili zake Karima;
pindi atendapo yuwalipwa malipo mema;
hasanati moya malipo ye kumi timama.

91. Mwenyi kunuwia kuitenda amali mbaya
asipoitenda kaandikiwa kwa yake nia;
na mwenyi kutenda kaandikiwa moya kwa moya
kwa fadhili zake Mola wetu mwenyi rehema.

92. Kiisha wakashuka wakafika wingu wa tini;
wakaona vumbi na sauti na moshi ndani.
Tuma kamuliza Jibrilu: ni watu gani?
Kaamba: Sheitani wazuiwa kuona sama.

---

86. 1. kawa für hawa.
88. 4. uridhii, mit arabischem Suffix i, mein.
90. 1. nuwia, in Gedanken sprechen.

93. Kiisha wakashuka na usiku wakawasili
baiti mukaddasi nyumba ngema tangu asili.
Wawene Boraki yu papale pake auwali,
tuma kamupanda kwa isimu yake Karima.

94. Katika kwenenda wakaona wangi ngamia,
watokao Shamu Makoreishi kawapitia.
Waonapo nyama Boraki wakakimbia;
moja kavundika lake ondo, siweze kwima.

95. Wakenenda tena wakaona wangi ba'iri;
moja kapotea, wakenenda kumudabiri.
Katoa salamu mwombezi tuma bashiri.
Wakaamba: sauti ya salamu ni yako tuma.

96. Kiisha wakenenda wakafika Maka na giza
kusijacha sana akakaa tuma kawaza.
Ali na khofu Makoreishi yao mayaza
na kukazibisha kwa khabari yake ya sama.

97. Katika kuwaza na kumaka tuma rasuli
yumwene asi maleuni Abujahali
akamudasisi kwa thihaka kuyua hali:
Ai Muhammadi nakuona uso kunama.

98. U na yambo gani kuu mno la kughayiri?
Ukatabaddali wako uso usinawiri;
kunambia nami, nikayua yako khabari;
siyo hali yako tuyuayo Abalkasima.

99. Akaamba: naamu, takuambia yangu khabari;
usiku wa leo nalikwenda mbali safari,
hafika mbinguni nikaona Mola jabbari,
akanipa mambo ya kutunza wangu mutima.

---

94. 4. siweze für asiweze.
96. 2. kusijacha, negative Form!
97. 2. yumwene, Perfect von ona.

100. Akazikusanya maleuni zote kabili
kuisikiliza khabari ye tuma rasuli.
Alipoweleza khabari ye yote kamali
pakawa kiteko na dhihaka na kumuzoma:

101. Ai Muhammadi, ni uwongo yake khabari,
usiku umoya wafikia mbali safari!
Mbingu ukaziisha ukaona Mola jabbari
uzidie shani, uwongo, hashaye tuma.

102. Khabari za mbingu na arishi katuziisi;
kwani hatukwenda hatupati kuzikaisi;
utwambie sifa za bait ilmukaddasi,
kwani tumekwenenda, twaziyua zote alama.

103. Moyo wake tuma ukaingia nyingi shughuli,
mambo ya usiku asiweze kuyafasili.
Mola kaamuru Jibrilu kuinakili
yote kuiweka mbele zake kuitezama.

104. Akawasifia sifa zake kizikariri
kapima kwa nyayo na dhiraa hatta shibiri.
Na Abubakari naye kaamba: ai bashiri
ndizo sifa zake, usibie zote alama.

105. Wote Makoreishi wakanena: ai amini,
ndizo sifa zake umeziye kuzibaini;
tu na watu wetu safarini, bani fulani,
watakuya lini, utwambie tukifahama.

---

101. 1. Man beachte, dass in umoya das Präfix sich noch genau nach usiku richtet.

105. 2. umeziye, Perfect von maliza.

106. Kaamba: watu wenu kawa mbali, watatokea
ijuma ya tano ndio siku yao ya kuya.
Yalipowandea siyo siku wakangojea
wasione kuya hatta punde jua kunama.

107. Tuma Muhammadi akaomba Mola wadudi
jua kuwakifu kutimia yake miadi.
Wakawatokea watu wao wote idadi.
Nayo ilile po ikatimu yake kalima.

108. Wakaamba: ni kweli sifa ndizo mezifasili;
na i ni sahiri kama hayo kwake kalili,
kwani yuapenda dini yetu kuibatili,
katumufuate tukaata wetu sanama.

109. Naye mwombezi tangu siku ya kwenda sama,
kunako arufu ya miski na tibu ngema,
apitapo ndia arufu ye siyakukoma;
wapitao ndia hutambua kupita tuma.

110. Basi, tuikomile mi'iraji kuinuthumu
kwa hamudi yake Maulana, Mola karimu.
Sala na salamu na bawazi na taathimu
zimwendeye tuma na ali ze na wote jama.

111. Rabbi turehemu kwa rehema yako azizi,
warehemu wote wasomao na wasikizi.
Sote turehemu kwa baraka za mwombezi
siku ya kiyama watuokoe na jehannama.

112. Na mwenyi kutunga mja wako muhuyi daiyani,
atumai jaza kwa khidima yake amini
kwa miongoni mwake tuma kesho peponi;
mwenyi kukhudumu watu wema hupata mema.

---

106. 1. kawa, negativ.
106. 3. siyo = hiyo.
107. 4. Dieser Vers scheint nicht ganz richtig überliefert.
108. 2. sahiri = uchawi.
109. 3. Man beachte die Form siyakukoma.

113. Hatta ye kalubu kufuata wenyi kahafu
kuingia peponi kwa lutufu yako latifu.
Ja kaifa, miye tatumai kwako wokovu
kwa baraka zake mwombezi wawi na wema.

Tama hadithi mi'iraji irrasul bihamd Illahi ilmalki iljalīl
wa salla Allahu ala sahab ilwajihi iljamīl
saidna Muhammed ilhādi ila sawe essebīl
wa **ala** āhlhu wa sahabihi wa
min tabaa hadāhum
ila yom ilbaath
wanushūr.

Amen

Amen

Amen.

Utenzi wa kutawafu kwe Muhammadi.

(Lied vom Sterben Muhammeds.)

Bism illahi irrahmani irrahimi.

1. Nianze jina la Illahi
auwali: bismillahi
raziku, ndiye fattahi
subhana wa taala.

2. Na sifa za Muhammadi
siwezi pisa juhudi;
ni idadi kwa idadi
sifa zake ziwaelea.

3. Sasa taka wakhubiri:
niwene hadithi nzuri
Muhammadi mukhtari
kutawáfu kwe nabia

4. Naliiona chuoni
hadithi hiyo yakini,
alizukuru Hasani
kabila Basariya.

5. Naye aliipokea
kwa maulana Aliya
karama Allahu radhiya;
nami tawahadithia.

6. Tawapa na mwanzo wake:
Muhammadi ali peke
yeye na watoto wake
yumwene Jibriya.

7. Yu na mwenziwe mwengine
wajile wafuetene.
Yule tuma amwene,
shaka moyo akatia.

8. Jibrili kakalimu:
salamu ndako salamu.
Yule tuma muungamu
salamu kaipokea.

---

2. 2. pisa = pisha.
3. 2. wene, Perfect von ona; vergl. 6. 4.
7. 2. jile, Perfect von ja = ya; fuetene, Perfect von fuatana.

9. Kiisa pokea rasuli
kamuuza Jibrili:
huyu mwenzio wa pili
i nani? nami nambia.

10. Siku zote kuja kwako
huja wewe peke yako;
leo una mwenzi wako;
nambie, pate mujua.

11. Akanena Jibrili
akamwambia rasuli:
huyu ni Izraili
yujile kukwamkua.

12. Ndiye malaka mauti,
ndiye mtwaa umati,
kulla kilicho hayati
ndiye mwenyi kukitwaa.

13. Ndiye mvunda majumba,
ndiye mweka wa tumba,
na mwana ndani ya mimba
ndiye mweza mtwaa.

14. Akanena yule tuma:
Jibrili mualimu,
yujile kunitazama
au yujile nitwaa?

15. Jibrili akajibu:
ewe mtume habibu,
nimetumwa ni wahhaba
kuja kwako kasidia.

16. Yujile kwako kasidi,
ewe tuma Muhammadi,
alilo nalo hana budi
illa nawe kukwambia

17. Mtume wetu rasuli
kamuuza Jibrili:
yu na ni Izraili
kwangu aliye nijia?

18. Jibrili atongoi:
Rabbi akutaka wewe
apenda onana nawe;
tena amenipa aya:

**Wa mā jaalnā libasharin min kablika lkhuldaa;
fa in mitta fa humu lkhālidūna?**

19. Kwisa kwe soma rasuli
akajua kwa dalili,
kwamba hino ni ajali
leo imefikilia.

20. Baada hayo kujua
yule mtume rasua
kilio akashangua,
akakithiri kulia.

21. Akalia Muhammadi,
kilio kikashitadi.
kwa huzuni ya fuadi.
Jibrili kamwambia:

22. Ewe mtume wa Muungu
waliliani, nduu yangu?
Kulia ko ni matungu
naona yakiningia.

---

18. 1. atongoi, Perfect von tongoa.

23. Kilio cha mukhtari
ni kilio akhiyari
au pepo au nari
au Fatuma zuria?

24. Mtume akamjibu:
ya Jibrili habibu,
sililii masahibu
yalionifikilia.

25. Simlilii Fatuma
wala baba wala mama,
wala siku ya kiyama,
wala pepo na dunya.

26. Simlilii Omari
wala Abubakari
wala Ali Haidari
hao siwakulilia.

27. Simlilii Hasani
wala ndugu ye Huseini
Abasi na Othmani
Khadija na zaujia.

28. Nililialo, nduu yangu,
ni huu umati wangu;
watamwassi Muungu
nifarikipo dunya.

29. Niondokapo dunyani,
wataibadili dini;
hawaassi wa Mannani,
watazidi kupotea.

30. Akasema Muhammadi:
hapa mwenyi kuwarudi,
kuffari na mayahudi
na baki watapotea.

31. Akiisha sema rasuli,
akapaa Jibrili
nakurudi tashili
na aya kamletea:

Kauluhu taala:
Innak la tahdi man aḥbabta walākin Allahu yahdi man yashaau wa huwa a'lam bilmuhtadīna.

32. Siwe ghafuru azizi;
kuwaongoa huwezi;
illa ndiwe mwombezi
kesho utawaombea.

33. Kesho siku ya kahati
utawatenga umati
ukiwapisha sirati
wema wema kitaowa.

---

29. 3. Man beachte hier die Form hawaassi, sie ist hier positiv und scheint ein Plural von huassi zu sein.

34. Kusema kwe Jibrili
pale mbele ya rasuli
wamwene Mikaili
papo akiwashukia.

35. Akaja na malaika
wengi waliokushuka;
idadi ye mukitaka
hesabu ye tawambia.

36. Ni elfu wa sabaini.
Salamu wakabaini,
akapokea Amini
salamu ya malakaa.

37. Akanena Mikaili:
salamu ndako rasuli,
akusallimu Jalali;
tena amenipa aya:

Kauluhu taala:

Innak mayyitun wa innahum mayyitūna, thumma innakum yauma ikiyamahi 'inda rabbikum takhtaṣimūna.

38. Illa ndiwe muokozi
kesho siku ya telezi
kwa yakini muombezi
ajali kufikilia.

39. Akayakini mauti,
umefikia wakati.
Pale alipo keleti
akaondoka muda saa.

40. Akaenda kwake amini
kwa mwana 'Isha nyumbani.
Akamuuza amini
Kilio hichi chạ nini?
Mume akamuambia.

41. Akanena Muhammadi:
nenda mwitika wadudi,
ameniita, sina budi
illa kwenda mwitikia.

42. Leo ndio kuagana,
mimi hamtaniona;
hatu wenyi kukutana
illa siku ya nazaa.

43. Leo ni siku ya kwisha
mimi nawe mwana 'Isha;
huoni mtu kubisha
nyumbani mwako kwingia.

44. Ndio mwisho wa kusema,
ndio mwisho wa kalima,
hatta siku ya kiyama,
ndipo tushuhudia.

45. Asikiapo mke we
maneno ya mume we
akalia kwa mayowe.
na akili ikizua.

---

35. 2. Man beachte die alterthümliche Form waliokushuka.
36. 4. malakaa, des Reimes wegen.
37. 2. ndako = li yako.
40. In dieser Strophe ist eine Zeile zuviel.

46. Kaamba: ewe mume wangu
kufariki ulimwengu
waniata na matungu.
Akakithiri kulia.

47. Akalia kwa kelele
sauti ikaenda kule.
Wenzi we wamusikile
jamii wakamendea.

48. Mikono ili vitwani,
ni vilio vya ndiani
hatta wakenda nyumbani
kwa mwana 'Isha kuingia.

49. Wakilia kwa matozi
wachamba: ewe mwombezi
watuata na simanzi,
siku zote tutalia.

50. Ewe tuma ndiwe baba,
watuata na musiba,
ndiwe muweka akiba
ya akhera na dunya.

51. Kilio cha nisyani
kikenea majumbani.
Ali ali nyumbani,
kilio kakisikia.

52. Kusikia kwe Alii
akatoka kwa fazai
akanena: kwa nabii
ku na kilio kaliwa.

53. Akatoka kwa kilio
kwa kelele na zomeo
akaja kimbiombio,
hatta nyumbani kaingia.

54. Kuwingia kwake nyumbani
akamuuza Amini:
nakuona na huzuni
na sura kubadilia.

55. Akajibu mukhtari:
ewe Ali Haidari,
leo nikisha umuri,
ajali amefikia.

56. Na leo tuagane,
umati hatuonani
na Hasani na Huseini
na sahaba wote pia.

57. Na hayo nikwambiayo
ndio mwisho nnenayo,
akatongoa; kilio
Ali akazidia.

---

48. 1. ili, man beachte die alte Copula li.

48. 4. kufia = kufika; aber hier ist das Wort fa noch in der alten Bedeutung: erreichen, bei etwas endigen, gebraucht.

49. In wakilia und wachamba ist die Form mit ki als erzählende gebraucht, wie in manchen Sprachen des Innern.

49. 2. wachamba = wakiamba.

51. 1. insani, arabisch: Menschen.

51. 3. ali, mit der alten Copula li.

53. 4. kafia, vergl. 48.

56. 1. Im Manuscript steht, wohl als Schreibfehler, statt tuagane: tunganene.

56. 2. hatuonani, man beachte das Praesens an Stelle des Futurum.

58. Kilia akijirusha
kinuka na kujiangusha,
akalia mwana 'Isha
na wenzi we wakalia.

59. Ali katanabahi
akaamba: inna lIllahi!
na kuhimidi Ilahi
rabbi asiye mithaa.

60. Kilio kilipovuma
akasikia Fatuma
akenda kwa muungama
kenda mbio akilia.

61. Akalia kwa matozi
achamba: ewe mwombezi
wanipa yu pi mlizi
awezaye kunilia.

62. Siku zote i na wewe
na leo mimi si nawe.
Fatuma na mume we
wakakithiri kulia.

63. Fatuma akaradidi:
ewe tuma Muhammadi
wanawatia waladi
mimi siwezi kulia.

64. Yule tuma wa wahabu
kalima hapati jibu,
kwa ajali kumsibu
mato hawezi funua.

65. Yamwingia sakarati
yamemuzinga mauti,
la kujibu halipati
kwa dhiki ya mautia..

66. Akaamba mwana Fatuma
ewe baba, ewe tuma,
wa lau kunitazama
huwezi kuniangalia?

67. Vua mato mtume,
mara moja utezame,
ulilo nalo useme
sote tupate sikia.

68. Yule mtume rasua
mato akayafunua,
kwa shida kayakundua,
Fatuma kamlekea.

69. Kamutwaa muombezi
kwa mahaba na mapenzi,
akamfuta matozi
kwa mkono we rasua.

---

59. 2. inna lillahi, arabisch.
59. 4. mithaa = mithala.
61. 2. achamba = akiamba.
61. 3. Die Wörter yu pi sind mir unverständlich.
68. 3. kundua = kunjua.
69. 1. taa = tazama?

70. Mauti aliyo nayo
yasimpate pa moyo;
akumbukapo kilio
mwana we alicholia.

71. Akamwambia maneno:
mwanangu silie mno;
haya mambo ni mfano
na ajili kutimia.

72. Silie ukakithiri
ukingia kukufari;
mauti ni makadari
kulla mtu takinia.

73. Jamii bin Adamu
siku yake ikikoma
hataweza kusimama
illa kuiandamia.

74. Silie ewe mwanangu,
kufa kolewa ni Muungu;
kulla kote walimwengu
ni faradhi kulekewa.

75. Na muomba Subhana
kesho siku ya nadana,
ndio kwanza kuonana
kesho ya nazaa.

76. Takuona siku hiyo
katika we na mama yo
pamoja na mume o
na maulana Aliya.

77. Fatuma akalingana
akamuuza amina:
ni wapi pakukutana?
sema nipate nelea.

78. Akamjibu rasuli:
tutaonana mahali
pema panapo jivuli
na umati wote pia.

79. Umati wote ulio
jamii takuwa nao.
Mavuli huu mumeo
ndiye mwenyi kuzuia.

80. Takuwa babu amina
na umati kukutana
hiwapa maji wakinwya.
Fatuma akamwambia:

81. Nisipokuona hapo
ni wapi nikuonapo?
Mtume kajibu papo,
mwanawe akamwambia.

82. Hapo usiponipata
tutaonana sirata
na umati na umata
wote pia ukaingia.

83. Takuwa na Jibrili
pamoja na Mikaili
tukipita tashili
na umati wote pia.

---

70. 2. Hier ist pa fast wie eine Präposition gebraucht.
72. 4. takinia, vom arabischen kān, sein??

84. Na mimi tuma rasuli
siku hiyo tatongoa:
ya Rabbi peke, nivua
na umati wote pia.

85. Na ndia hiyo ni refu
miaka tiltalafu,
illa mapana dhaifu
kana unywele umoya.

86. Alifu ni ya kuingia
alifu ni ya kuendea
alifu nda kushukia;
sifa zake takwambia.

87. Nabii na mursali
watazukuru Jalali:
tupeleke tashili
ina dhiki hino ndia.

88. Wasema: Rabbi mkwasi
tupeleke kwa upesi,
ya rabbi nafsi nafsi
roho zao waombewa.

89. Illa nami ntasema:
rabbi tuvushe salama
na umati hali jema
tusione na uzia.

90. Rabbi peke subhana
kalima niye kanena:
ai malaka mwaona
Muhammadi mursaa.

91. Mitume yote nabii
na jamii mawalii
sadiki na shuhadai:
roho zao waombewa.

92. Wao pia roho zao
kuokoka peke yao
Muhammadi anenao;
kwa yote mamusikia.

93. Haombei nafusi ye
ya kuokoka peke ye,
aombea umati we
jamii awaombea.

94. Akasema: Rahmani,
malaka shuhudiyani,
dhambi zao ghufurani
umati wake nabia.

95. Alikuwa dunyani
umati wake amini,
akasema kwa lesani
ali katika dunia.

96. Akasema kwa sahihi:
la ilah illa Allahi,
Muhammadi rasul Illahi.
Dhambi nimemondolea.

97. Fatuma akalingana:
hapo nisipokuona?
Muhammadi akanena:
ewe, mwanangu, sikia.

---

87. 4. hino, alterthümliches Pronomen.

98. Usiponiona hapo
meza nene takuwapo
hiwatenga wenyi pepo
walio katika taa.

99. Hiwaombea mitamu
hiwanywesha islamu
pema na wote huramu
wake na waume pia.

100. Mitume yote nabii
salihi na mawalii
ndimi wa kuwapa maji
insha Allah taala.

101. Akaamba yule Fatuma:
takuona muungama
siku hiyo, yule mama
ni wapi endapo kaa?

102. Akamjibu Amini:
atakwenda kiwandani
kiwanda hicho peponi
ki na arufu ajaa.

103. Hapo katika raudha
pana arufu ya fedha
kwa killa ngema bidha
ndipo endapo kukaa.

104. Mtanga we ni ambari
miski wa kaafuri.
Fatuma kashukuri
na kumuhimidi taa.

105. Akiisa sema rasuli,
akatokea Bilali
akanadia kusali.
Mtume akasikia.

106. Yule Bilali kanadi:
Salati ya Muhammadi.
Yule tuma karadidi
Bilali kamamkua.

107. Akatamka rasuli:
sikia sana Bilali,
leo siwezi kusali,
na mangine nasikia.

108. Nimetoshewe miwili
na roho i na shughuli;
Abubakari na sali
aweza kunikefia.

109. Na sali Abubakari,
wafuate muhajari
pamoja na ansari
na sahaba wote pia.

---

98. 2. hiwatenga = nikiwatenga, vergl. in der folgenden Strophe hiwaombea und hiwanywesha.
Strophe 99 ist nicht ganz klar.
102. 4. in dem ajaa am Ende steckt wohe ajaba, des Reimes wegen verändert.
104. 4. taa = taala.
108. 1. toshewe ist Perfect. Pass.

110. Mimi siwezi kwenda
mimbarini kuipanda
kwa mwili kunipinda
na roho i na fazaa.

111. Imefikia ajali.
Kunena hao rasuli
kusikia kwe Bilali
kilio awile lia.

112. Akalia kwa kilele
achamba: enyi wenzile
kheiri msinizali
kheiri nami kujifia.

113. Maisha ya kashuhudi
mauti ya Muhammadi,
yali msiba shadidi,
madina uliungia.

114. Kafika mosketini
kasimama mlangoni
akasema kwa lesani,
sahaba wakasikia.

115. Akaamba: enyi muhajiri
nitumiwe ni Bashiri;
na sali Abubakari,
yeye hatapata kuya.

116. Nanyi nyote muungamo
jamii awasallimu.
Abubakari na kimu
sala yuwamtoshea.

117. Hawezi kuja amini,
amenena: kasalini;
moyo umo shughulini
kwa mauti kumwingia.

118. Roho haina kituo
kwa mambo ayaonayo,
zia zote ziliyo
hawezi kujiondolea.

119. Awaambia asahabu,
duu ze na akirabu,
Wamaka na Washiribu,
mliopo nyote pia.

120. Bilali awaambiapo,
sahaba wasikiapo,
kwa jamii waliopo
wawile wote kulia.

121. Kilio cha ansari
pamoya na muhajiri
hatta watoto saghiri
madani wawile lia.

---

111. 4. awile lia, Perfect mit kuwa gebildet.
112. 2. Die Form wenzile kann ich nicht recht erklären.
113. 4. uliungia = ulioingia.
115. 2. nitumiwe, Perfect.
116. 3. kimu, arabisch: aufstehen.
119. 2. duu = dugu.
120. 4. wawile kulia, Perfect mit kuwa, vergl. 121. 4. wawile l

122. Kilio kikienda kule
muyi wote makelele.
Bilali aondoshile
akaikimu sala.

123. Akaima Abubakari
kasogelea mimbari
makamo ya mukhtari
alipokurubia.

124. Alipokwisha simama
makamo ya muungama
akaingiwa na huruma
kilio awile lia.

125. Kalia Abubakari
pamoja na muhajiri.
Kasikia mukhtari,
kilio akasikia.

126. Akasikia amini
akauza: ku na nini?
ku nani mosketini?
ku na yowe la kulia.

127. Akamwita shekhi Ali
na nduu yake Fadhili,
wakaenda wote wawili
mtume wakawambia.

128. Mtume awambizile:
simameni mnitwale,
mwende nami polepole
hatta kuliko jamaa.

129. Mikono yake miwili
moya kampa Ali;
na wa pili ni Fadhili
ndiye aliyepokea.

130. Kawaweka mafuzini
mikono yake amini;
kipata mosketini
safu zimetengelea.

131. Saidi Abubakari
kumwona kwe Bashiri,
sala akataakhiri,
nyuma nyuma karejea.

132. Yule tuma akasema:
wasalishe wewe jama
mimi siwezi simama
nitasali kwa kukaa.

133. Abubakari khalili
akete, asikubali
kutakadamu kusali
akaona ni mo haya.

134. Kuoneka mukhtari
masahaba hawakiri,
akasogea mimbari
akasalisha jamaa.

135. Akiisha sali bashiri
wakakutana muhajiri
na jamii ansari,
tuma akawawusia.

122. s. ondoshile, Perfect von ondoka, wie im Yao gebildet.
133. s. akete, Perfect von kataa.

136. Nawausia: wenzangu,
sikizani haya yangu:
kufa ni kadha ya Mungu,
hapana takayesaa.

137. Basi, mtume kasema:
nawausia yatima
watoto wasio mama
baba zao wafiliwa.

138. Akaamba tena amini:
nawausia jirani,
Allah Allah watunzeni
hatta wasipo wafaa.

139. Nawausia: na sala
msiate Allah Allah,
msifanye mghafala
wakati wakifikia.

140. Nawausia: ramadhani
msiate ifungeni,
ghururi ya duniani
isije kuwakhadaa.

141. Nawausia: na zaka
na heja kwenda Maka.
Kulla wakati kufika
msiate nawaambia.

142. Nawausia sahaba:
na kuoga majanaba,
mtendapo ni ukuba
mwilini mwautia.

143. Nawausia: fitina
na mwenzi o ukumnena,
faraghani kumsema
hayo hayakwelekea.

144. Kulla lisilopendeza
hamuhitaji kweleza,
moja nimezile saza,
nami napenda waambia.

145. Akasema tuma: wangu
nawauza, dugu zangu
nilimkosa matungu
naseme himsikia.

146. Mtu niliyemuasi
leo n'atoe kisasi
asije kuninukusi
kesho mbele za Jalia.

147. Tuma kasema akiisha
wote wakasema: hasha.
Yuondoshile Ukasha
sahaba wake nabia.

148. Akasema Muarabu
akamwambia habibu:
mimi walinidhurubu
yAllahi siku moya.

149. Sikuyajua sababu
walio kunidhurubu, [dhabu
haenda kwangu na gha-
kwa fimbo walionitia.

144. 2. hamuhitaji scheint ein negativer Conjunctiv zu sein.
145. 1. Man beachte die Form himsikia = nikimsikia.
146. 4. Jalia = Jalila.

150. Akamwambia amini:
Ukasha sema yakini
siko hiyo siku gani,
sema yapate nielea.

151. Yule Ukasha kasema:
siku hiyo yalingama,
wewe walipanda nyama
wali juu ya ngamia.

152. Akanena muungamo:
kama hayo sifahamu,
illa maneno timamu
hayo waliyonambia.

153. Akamwambia habibu:
twaa kisasi; sahibu;
kuliko mi siajabu
hayo kukufanzia.

154. Abubakari siddiki
akamwambia: rafiki,
maneno yako ni hakki,
mimi tuma nafidia.

155. Kisasi kitwae kwangu,
tafidia tuma wangu,
usimkose matungu
kwa vile alivyokaa.

156. Ukasha asikubali;
sharti yeye rasuli
alinipiza mwili,
huwaje kwako kutwaa?

157. Omari akamjibu:
ewe Ukasha sahibu
nije mi, unidhurubu,
kisasi upate twaa.

158. Ukasha asiyakiri
maneno yake Omari;
sharti yeye mukhtari.
Kaamba: yangu mwasikia.

159. Akatamuka rasuli
kamwambia shekhi Ali:
mtume huyu Bilali
ende nyumbani ajaa.

160. Akamwambie Fatuma:
fimbo yake muungama
aitaka iende hima.
Bilali kaandamia.

161. Akipata mlangoni
kabisha kaamba: hodini
waliomo nyumbani.
Fatuma kamwitikia.

162. Kamuuza: we u nani
uliopo mlangoni?
karibu uingie ndani!
Naye Bilali kangia.

163. Yule Bilali kakuli
akamwambia batuli:
mtumiwe ni rasuli,
fimbo aihitajia.

---

151. 4. wali, du warest.
152. 2. ist sifahamu hier positiv oder negativ?
153. 3. mi für mimi.

164. Akatamuka batuli
akamwambia Bilali:
ku na nini kwa rasuli
kuja itaka 'asaa?

165. Fimbo yake Muhammadi
hutwaa siku ya 'Idi
au siku ya jihadi
mwenyewe akachukua.

166. Fatuma akamuuza:
huwaje kuiyagiza?
Bilali akamweleza
kisa chote kamwambia.

167. Bilali kiisha mwambia,
Fatimata zahria
papo awile kulia
na maneno katongoa.

168. Wali papo asahabu
nduu ze na akirabu
hatta ye bin Talibu
huwaye akaridhia?

169. Na fimbo yake rasuli
kamusallimu Bilali,
naye wakenda wawili
hatta wakasikilia.

170. Akipata mlangoni
ile fimbo ya amini
ikenda mihirabuni
batuli kampokea.

171. Akenda nayo kanadi,
kalima akaradidi:
ana binti Muhammadi
nimekuja wangalia.

172. Ndimi binti ye amini
ndimi mama ye Hasani,
nambiani, nambiani
mambo yaliotokea.

173. Asinijua nijue,
asikuwapo nambiwe;
leo ni siku, ni leo
mwenyi kilio hulia.

174. Nalipokea khabari
moyo wangu hakasiri,
ya kuwa tuma bashiri
kisasi atatolewa.

175. Fatuma akasema kiisha,
kampokea Ukasha
ile fimbo kamshisha.
Na maneno kamwambia:

176. Kisasi chake nabii
nitwaa mi binti ye;
si adabu kwake yeye
kisasi kumtolea.

177. Ukasha asikubali
akamwambia batuli:
sharti yeye rasuli
mkitaka ya sharaa.

---

169. 4. sikilia = fikilia.
171. 3. ana, arabisch: ich.

178. Hapo akaamba habibu:
twaa kisasi sahibu
upenda po, ni dhurubu.
Ukasha akamwambia:

179. Takutoaje kisasi?
uli ndani ya kamisi,
ivue yako kamisi,
nipate kukurubia.

180. Kumwona kwe rasuli
kuuata wazi mwili.
Yuwile kukabili
kitofu kusujudia.

181. Ukasha katakalamu
kamwambia mungamo:
siku moja ulisema
na miye hakusikia.

182. Ashikaye kitofu changu
amepata radhi yangu
hatta mbele za Muungu
atapata mashafaa.

183. Ndipo hafanya gharadhi
kwa ule wako waathi;
nami niwilia radhi.
Hayo nalio kuambia.

184. Akatamuka rasuli:
nalionena ni kweli,
mwenyi kushika mwili
hana adhabu asia.

185. Akalingana amini:
mlio mosketini,
mtu endaye peponi
alama ye tawambia.

186. Ni kama huyu Ukasha,
hana tena mushawasha;
zambi zake ameziosha,
zote zimeondolewa.

187. Kiisha hayo Muhammadi
mosketini kanadi:
nenda zangu, sitarudi
muda umetekelea.

188. Akamwita shekhi Ali
na duu yake Fadhili,
mikono wake miwili
mabegani kawatia.

189. Na huyule mwana 'Isha
ali katika firasha
baadaye akandosha
kampakata nabia.

190. Tuma mato kayafumba,
pasi kauli ya kuamba;
waliopo wenyi nyumba
jamii wakasangaa.

191. Kumwoneka rasuli
kufumba mato mawili
wakayakini ajali
leo imefikilia.

179. 2. uli, du bist.
180. 3. yuwile, Perfect von kuwa.
188. 1. eta = leta.
189. 1. huyule, alterthümliches Pronomen.
189. 3. akandosha = akaondoka?

192. Wakalizana nyumbani
na Hasani na Huseini
walio mosketini
wakajawa lifazaa.

193. Wakalizana muhajiri
pamoya na ansari;
papale pa mukhtari
wawene mtu mmoya.

194. Wamwene Muarabu
amekima fi lbabu
akasema kiarabu:
nataka rukhsa kuingia.

195. Taka rukhsa niingile
mtume nimemkuli.
Fatuma amrudile:
ewe mwarabu sikia.

196. Tuma yu na sakarati,
yamemzinga mauti,
hawezi hatta kuketi,
huwaje kumwangalia?

197. Kanyamaza Mwarabu
asipate ya kujibu;
papo kaleta jawabu:
taka rukhsa kuingia.

198. Fatume akaradidi:
Mwarabu ni kurudi,
humpati Muhammadi;
hayo naliokuambia.

199. Kasema mara ya tatu:
taka rukhsa wakwetu,
namtaka tuma wetu,
kwa ni kunizuilia?

200. Sisi hatukukatazi
kutezama muombezi,
illa taona hawezi.
Ndipo hayo hakuambia.

201. Mara ya ne akanadi:
ya ahali liibadi,
namtaka Muhammadi;
kwa ni kunizuilia?

202. Fatima kaeta kauli:
Ya Mwarabu, rasuli
tamwona na shughuli
kwa mauti kumfia.

203. Kusikia kwe rasuli
maneno yake batuli
akatamuka khalili:
ewe Fatuma nijia.

204. Akanena yule tuma
akamuuza Fatuma:
huyu ambaye mwasema
jina lake lakwelela?

205. Akatamuka Fatuma:
simujui lake jina.
Muhammadi akanena:
ewe mwanangu sikia;

192. 4. lifazaa = ilfazaa. vgl. 201. 2. liibadi = ilabidi, arabisch.
193. 4. mmoya = mmoja.
195. 2. was ist nimemkuli für eine Form?
202. 1. eta = leta.
202. 4. kumfia = kumfikia.

206. Huyu siye Mwarabu,
huyu ni tuma ya rabbu;
ndiye mutwaa kulubu
roho za viumbe pia.

207. Ndiye hadimu lazzati,
ndiye malaka mauti,
ndiye mvunda buyuti
na miji ikipotea.

208. Ndiye mtungua baba
na angawa na mahaba;
ndiye mweka msiba;
roho zote yuwatwaa.

209. Yule tuma amwambii:
mlango mfungulie
naye mauti aingie.
Fatuma akafungua.

210. Mlango wake rasua
Fatume akafungua.
Akapita mwenyi kuua
hatta ndani akaingia.

211. Akaamba na salamu,
kapokea muungamo.
Kiisha akatakalamu
mtume akamwambia.

212. Mtume akafatahi
akamuuza: sahihi,
ujile ni twaa rohi
au kuja niangalia?

213. Kanena Izraili:
Amenambia Jalali,
kamshauri rasuli
apendapo roho twaa.

214. Akataapo sitwae,
roho yake muatie,
rudi nyuma ukakae;
ndiyo aliyonambia.

215. Sasa khitiyari kwako,
nangoja majibu yako;
unenapo rudi kuko
sasa hivi tarejea.

216. Mtume akatamuka:
Izraili pulika,
nina haja naitaka
nawe ni kunifanyia.

217. Yule nduli kabaini:
haja kwangu wataka ni?
Akamjibu Amini:
enenda muda wa saa.

---

207. 1. Dieses Wort hadimu (mit h), der Zerstörer, ist nicht zu verwechseln mit khadimu, der Knecht, welches nur missbräuchlich hadimu gesprochen wird.
209. 1. amwambii, Perfect.
212. 3. rohi des Reimes wegen.
217. 1. nduli, der Todesengel.

218. Namngoja Jibrili
kwenda akatanazili,
nna maneno mawili
nataka mbainia.

219. Yule nduli papale
kaondoka polepole,
akaenda nde, akele
akaketi kungojea.

220. Akashuka Jibrili
akaonana na nduli
kwanza akamsaili:
ya akhi Ziraili ya,

221. Umekwisha kuitoa
roho ya tuma nabia?
Ziraili katongoa:
roho sitasa itoa.

222. Yunambizile rasuli,
nisaburi saa mbili,
nimungoja Jiburili,
ndipo nami hatulia.

223. Kaonanene kabisa
nami naja hivi sasa;
usije sema hatasa
mimi naja kumtwaa.

224. Akenenda Jiburili
kwa Muhammadi rasuli:
Salla Allahu wa salli.
Salamu kampokea.

225. Kaitikia muungamu:
wa alaika salamu,
Jibrili mualimu,
karibu, upate kaa.

226. Akaja na malaika
wangi walio kushuka;
idadi ye mwaitaka
elifu walitimia.

227. Akaja na ridhwani,
ni bawabu wa peponi,
na malaka lake tena
hao waliotelea..

228. Na pepo yote kupewa
na manukato kutiwa
yamngojea rasuli
akienda apate ingia

229. Yule mtume rasuli
kamuuza Jibrili:
uwene Izraili,
hapo nde amekaa.

230. Jibrili akanena:
ni kweli nimemwona,
wa amma tuma Amini
sikhofu akikujia.

231. Kaamba rabbi subhana:
amefanya mambo mema
hatta siku ya kiyama
mambo aliokuwekea.

---

219. 1. papale, altes Pronomen.
219. 3. akele, Perfect von kala = kaa.
223. 1. diese Zeile kann ich mir nicht völlig erklären.
228. 1. statt pewa vielleicht kupepewa.
231. 4. alo für alio.

232. Kwanza milango mbinguni
i wazi na ya peponi;
hatta mahuru laini
wamejipamba jamia.

233. Pepo imetengeleza
mapambo na kuvukiza.
Alipokwisha mweleza
sura zikampotea.

234. Sura akabadilika
kwa mauti kumshika,
mishipa ikajituka
na roho i na fazaa.

235. Na mwili kayayuka,
marra huona mashaka,
hawezi tena kuinuka
kwa shida ya mautia.

236. Mishipa ya mukhtari
yote ikatoka hari
kwa misiki na ambari
ndio iliyoawia.

237. Na Hasani na Huseini
wali wakele kitwani,
mwana 'Isha kuumeni
upande aliokaa.

238. Fatuma izzaharati
kushotoni kukeleti,
na jamii zaujati
ikawa kumzingia.

239. Ikawa kumzunguka
na kilio na hataka
hamu na kusikitika;
mtume kawasikia.

240. Mtume kuona sayo
waliliavyo kilio
na maneno wanenayo
huruma ikamwingia.

241. Huruma zake rasuli
mambo akayafunua
akiwa kumamkua:
mwana 'Isha nisikia.

242. Sasa ndipo kuwaagana
na mauti nayaona,
hatta nguvu sina tena
siwezi kujizungua.

243. Na kushoto kitezama
akamwona Fatuma
kamwambia: ewe mama,
kwa kherini nyote pia.

---

235. 4. mautia, des Reimes wegen für mauti.
237. 2. wakele, Perfect von kala = kaa; davor ist dann noch das Hülfsverbum li gebraucht.
239. 2. hataka, arabisch: das Zerreissen des Schleiers.
240. 1. sayo = hayo.
243. 4. von kwa kheri ist, als wenn es ein Imperativ wäre, ein Plural kwa kherini gebildet.

244. Na Hasani na Huseini
si mo tena duniani
kwa kherini, kwa kherini,
muda uli kunyamaa.

245. Sasa tuma mukhtari
mimi nijile taiyari,
nawe unipe amri
roho nipate itwaa.

246. Yule tuma yumwambie:
roho yangu jitwalie,
hayo yako niridhie,
bali ni na yambo moya.

247. Taka roho uitwale
uitwale polepole
matungu yasiende kule
roho utakapo twaa.

248. Izraili kajibu:
nitatwaa taratibu
sitatwaa kwa adhabu.
Basi, roho akatwaa.

249. Kasikia Muhammadi,
kutawafiku saiyidi.
Wakasikia munadi
mbinguni wakinadia:

250. Enyi mulio duniani,
tezamani, tezamani
kipendo cha Rahmani
hali yake aliokaa.

251. Tezamani mauti ye
yaliompata yeye;
hatta zambi yusafiwe,
hana zambi hatta moya.

252. Tunzani yaliompata
na mauti na matata
na dhiki zaliomkuta
siku ya roho kutwaa.

253. Tunzani mkifikiri
msitwawe ni ghururi
madhambi mkakethiri,
kumbukani mautia.

254. Yakumbukeni mauti;
ufikiapo wakati
mbele yake ya kahati
ajali ikitimia.

255. Hizi tili za mwili
kulla ndwele mbalimbali
pana ndwele ya ajali
i pale ikikujia.

Zwischen 244 und 245 fehlt wohl eine Strophe: Gabriel oder Izrail spricht.
246. 2. ji in jitwalie ist alterthümliches Pronomen für das jetzt gebräuchliche i.
251. 3. safiwe, Perfect passivi.
256. 1. was heisst nabiyaka eigentlich?

256. Mtunzeni nabiyaka
ndwele alipomshika
na roho ilipotoka
hali yake aliokuwa.

257. Kaifa bin adamu
aliye kula haramu
kulla saa kula tamu
huwaye akifikia.

258. Basi, komile, tamati
kuwakhubiri umati
maombezi ya mauti
yote nimewaandikia.

259. Pasilepo yatunzeni
mauti yake Amini.
Nasi tumo duniani
na siku zitawadia.

260. Kulla mtu siku hiyo
sikiza niwambiayo,
msidharau kwa hiyo
mtakwenda jionea.

261. Huko akhera kuzuri,
illa ndia ni khatari
na ndia ye kaburi
ni ndia ya kupotea.

262. Pana na hiyo sirati
ni ndia nayo hupita
kwa shida na kwa matata
na ukalifu wa ndia.

263. Hatta akhera kufika,
olewapo ni rabbuka,
mtu haoni mashaka
hupita muda wa saa.

264. Illa uwapo na shida
utapita kwa matata
na adhabu ya baida
isio kurehemiwa.

Tamat ilkitāb biaun Illah ilmalik ilwahhāb. Allahum aghfir ilkātibihi wa lwalidihi wa lmuslemina. Amina ya rabb ilalamina.

258. s. so steht im Manuscript, aber die Worte geben so, wie sie sind, keinen Sinn; ich möchte lieber mwombezi lesen, aber auch dann macht die Wortstellung der Uebersetzung Schwierigkeit.

Hekaya na visa.

(Märchen und Geschichten.)

Hekaya ya nabii Musa na kipofu.

(Moses und der Blinde.)

Alitoka nabii Musa siku moja katika siku kuenda sema na Mola wake. Hatta alipofika jiani akakuta ziwa kubwa sana akaona watoto wengi wanakwoga katika lile ziwa. Na mmoja kipofu katika wale watoto, haoni, macho yake yamepofuka. Na wenziwe wanamwuzi sana wanamsukuma wanampiga wanamtekea wanamfanza killa namna.

Nabii Musa akasimama kutazama yale mambo ya wale watoto, akasimama muda mkubwa sana kutazama zile khabari za wale watoto na mambo yanaompata yule kipofu. Nabii Musa akamwonea huruma sana yule kipofu akamwombea dua kwa Mngu apate macho yake yule kijana.

Mwezimngu akajaalia yule kijana macho yake kama kwanza. Alipoona nabii Musa yule kijana kapata macho yake akashukuru Mola wake akasema: alhamdu lillah rabb ilalamina, atapumzika huyu kijana sasa. Akawaacha wale watoto vilevile wanakoga katika lile ziwa akashika njia nabii Musa akenda zake akafika alikotaka akafanyiza shughuli yake. Akesha akarudi hatta alipofika pale ziwani akaona wale watoto wanakoga vilevile.

Na yule aliyokuwa kipofu yumo anakoga. Akasimama nabii Musa kutazama wale watoto akamwona yule kipofu anafanyiza fiili mbaya sana, alipopata yale macho yake. Akaona nabii Musa yule kipofu anawazili wenzi we sana. Nabii Musa akastaajabu sana kwa ile khabari ya yule kipofu anaofanyiza. Nabii Musa akarudi alikotoka hatta pale anapokwenda kusema na Mola wake. Akasimama akaomba dua akasujudu Mola wake.

Akamjibu: Ya Musa, nini unataka? Musa akajibu: Mola wangu, bwana wangu, nimeona ajabu kubwa sana, sijapata kuona. Mola wake akamjibu, umeona nini, ya Musa? Akasema: nimeona kijana anakoga na wenziwe, naye kipofu, wenziwe wakamwuzi sana nikamonea huzuni sana kwa yale mambo yanaompata, nikaomba dua kwako ili apate macho yake yule kijana awe kama kwanza, apumzike uzia wa wenzi we; ukamjaalia macho yake kama kwanza na kuzidi kuliko kwanza; nikashukuru sana kupata macho yake yule kijana akawa kama wenziwe; nilipoona vile nikaona vyema nikashika tariki nikenda zangu; hatta sasa narudi namwona yule kijana kipofu anafanyiza mambo mabaya sana, anaumiza wenziwe anawazili wenziwe sana kwa sababu ana macho yake; nikastaajabu sana kwa yale mambo anaofanyiza yule kijana, hatta nikarudi kwako kuuliza khabari hii; ndilo neno niliojia.

Akamjibu Mola wake: Ya Musa, mimi umenifanya, sijui mambo? Akajibu nabii Musa: kwa nini, Mola wangu, bwana wangu? Akamwambia: Mimi yule hatta nikamtia apofue, najua kwamba fiili zake baya sana, hatta nikamtia upofu. Akajua nabii Musa kwamba vipofu si watu wakuandamana nao, si watu wema- Akarudi nabii Musa akenda zake hatta alipofika pale ziwani akawakuta wale watoto wanakoga vilevile. Na yule khabithi alamali karudia upofu wake kama kwanza na kuzidi.

Nabii Musa alipoona vile akajua kwa kuwa yule si mtu mwema. Nabii Musa ashika njia akenda zake.

Hiyo ndiyo khabari ya: kipofu si watu wema.

Asili ya vitu vya themani vinavyotoka katika ardhi.

(Woher stammen die Schätze in der Erde.)

Vitu vilivyo katika ardhi: Almās, yakuti, fyeruzi, dhahabu, fetha, chuma, risasi, shaba, sandarusi na vitu vingine baathi ya vitu.

Aidha khabari ya vitu vilioko katika uso wa ardhi, vitu vya maádani methili ya hivyo tulivyonena.

Fahamu kwamba kanena mtu mfanya hadithi kwamba vitu hivyo vyote mali ya Karuni*).

Katika zamani za kwanza katika siku ya nabii Musa aleihi salām alikuwa mtu jina lake Karuni. Mtu huyu alikuwa na mali sana. Amenena mfanya hadithi kwamba funguo zake hamula ya ngamia 14 yaani mizigo ya ngamia kumi na mine. Aidha ilipoba'thiwa nabii Musa kuwa mtume, aidha Karuni hana mali. Yeye mtu mmoja maskini sana.

Aidha amenena mtu mfanya hadithi, kwamba Karuni ilikuwa kabila yake katika bani Israel, naye alikuwa ami yake nabii Musa aleihi salām. Naye alikuwa mtu alimu sana katika bani Israel, alikuwa mtu mwenyi akili sana, alikuwa mtu mcha Mngu sana. Alikuwa mtu mmoja anajua sana kusoma taurati, hapana katika bani Israil ajuaye kusoma taurati kushinda Karuni.

Aidha na nabii Musa alikuwa Mngu kamjaalia ilmu alkimia alikuwa anajua sana yeye na Haruni nduguye. Alipoona Karuni kwamba nabii Musa anajua ilmu alkimia akataka naye ajue. Akaenda kwa nabii Musa aleihi salām akanena kwamba: nifundishe ilmu hii. Nabii Musa alipomwona Karuni mtu mcha Mngu sana akanena katika moyo wake kwamba huyu hataki dunya walakin anataka kujua ilmu. Maana anamwona mtu moja mtaowa sana anaogopa Mngu sana akamfundisha ilmu alkimia. Alipojifunza Karuni ilmu alkimia hatta akajua akamchukua Iblisi maleūni akamharibia ibada yake kidogo kidogo.

Tokea Karuni akiabudu siku mbili, siku moja anaasi Mngu. Hatta akawa siku mbili anaasi Mngu siku moja, siku moja anaabudu. Hatta ikawa siku tatu anaasi Mngu na siku moja anaabudu Mngu. Ikawa siku sita anaasi Mngu, siku moja anaabudu Mngu. Hatta ikawa kabisa haabudu.

Ikawa kazi yake ilmu alkimia, hatta akafanya mali athimu yaani mali mengi sana. Akafanya batara katika kichwa chake

*) Eigentlich müsste dieser Name immer Kar'uni geschrieben und gelesen werden.

asimjue Mngu aliyemwumba wala asijue nabii Musa aliyemfundisha. Kazi ileile ikawa yeye mtu mkubwa sana katika bani Israili yaani yeye mtu tajiri sana katika zamani yake. Hiyo ndiyo khabari ya Karuni.

Ama khabari ya nabii Musa aleihi salām. Alipomwona Karuni kafanya kiburi katika moyo wake kwa sababu ya mali, akajuta kumfunza ilmu alkimia, maana kafanya kiburi kwa Mngu. Aidha hatta siku moja katika siku Mngu mtukufu akamuamurisha mtume wake Musa aleihi salām kwamba killa mtu mwenyi mali lazim atoe zakaa reale elfu kuwa moja na ngombe elfu kuwa moja na buzi elfu kuwa moja na ngamia elfu kuwa moja na kwa killa baathi ya vitu elfu kuwa kimoja na kwa killa mtu mwenyi mali atoe zakaa.

Aliposikia nabii Musa maneno ya Mola wake akanena: nimesikia. Mtume wa Mngu Musa aleihi salām akamwita Karuni kumkhubiri khabari kama hiyo. Maana yeye mkubwa wa matajiri katika mji. Akamwambia khabari yote. Aliposikia Karuni maneno ya nabii Musa aleihi salām akanena: nimesikia, walakin ntakwenda kwambia wenzangu khabari kama hiyo na khalafu ntaleta jawabu. Nabii Musa akanena: insha Allahu.

Karuni akatoka akaenda kwake akahesabu katika reale elfu moja akatenga akaona fedha methili ya mlima, chungu nzima. Akanena katika moyo wake: fedha hii yote nimpe Musa kwa sababu gani? Akaona uchungu sana katika moyo wake. Aidha Karuni alikuwa na khazina elfu na kīla hunena asharat alāfu na kīla hunena ashirina elf, na kwa killa khazina funguo eshirina elf. WAllahu a'lam.

Aidha alipoona Karuni fedha nyingi ametoka akawaita matajiri wenzi we akawaambia: mnazo khabari za Musa? Matajiri wakanena: la, hatuna khabari. Karuni akawaambia kwamba Musa anataka kunyanganya mali zenu. Matajiri wakanena: kwa nini? Karuni akanena: mimi sijui sababu, ameniita jana; nimekwenda kwake; amenambia kwamba kwa killa reale elfu lazim utoe zakaa reale moja na kwa killa kitu baadhi ya vitu; nami nilipotazama nikaona hapana sababu yakutoa fedha burre; basi nini mashauri yenu? Matajiri wakanena; sisi hatuna

shauri, yote unayo wewe, maana wewe mkubwa wetu na shauri jema unajua wewe kushinda sisi.

Karuni akanena: vyema; akafanya akili zake akaona mashauri mazuri. Akanena: Musa kanena kwamba hokumu ya Mngu mwezi hukatwa mkono na mlevi hupigwa fimbo themanini na zāni hupigwa fimbo mia akiwa hana mke, n'akiwa a na mke hurujumiwa, basi. Sasa lazim tutafute mwanamke tumpe fedha akiri nafsi yake kwamba Musa kazini naye; akiisha kunena mwanamke kwamba Musa kazini naye, hatuna buddi illa tumpige hatta afe, tutastarehe na mali zetu.

Matajiri wakanena: shauri jema sana, wakamtafuta mwanamke wakapata wakapeleka hatta kwa Karuni. Alipofika mwanamke kwa Karuni, Karuni akamwambia: unataka kukaa katika iddunya kwa raha au kwa taabu. Mwanamke akanena: nataka kukaa kwa raha. Karuni akamwambia: nataka unene neno moja, ntakupa elfu dinari. Mwanamke akanena: ntanena maneno kumi si moja. Karuni aliposikia majibu mazuri, akanena: nataka unene mbele ya Musa kwamba kazini nawe; utaweza kunena? Mwanamke akanena: naweza kunena zayidi ya hayo. Karuni akanena: vema; akampa dinari mia.

Marra Karuni akawaita matajiri wote wenzi we. Marra akamwita nabii Musa aleihi salām, akaja, akamwambia: ya Musa nimekwita unene maneno yako unaotaka kwetu, maana hawa matajiri hawakusikia maneno yako. Nabii Musa akanena kwamba: nimetumwa na Mngu kukuambia: mtoe kwa killa reale 1000 kuwa moja na kwa killa kitu katika baadhi ya vitu 1000 kuwa kimoja; na mwezi akatwe mkono na mtu mlevi apigwe fimbo themanini na mtu zani apigwe fimbo mia. Hajaisha nabii Musa kunena maneno yale illa Karuni alisimama vema akanena: ikawa wewe umezini kazalika upigwe fimbo mia? Nabii Musa akanena: naam. Karuni akanena: wewe umezini na mwanamke. Musa akanena: mimi? Karuni akanena: naam. Nabii Musa akanena: yu wapi mwanamke? Karuni akanena: kwamba mwanamke akanena kwamba sahihi, umezini naye; nini jazaa yako? Nabii Musa akanena: ikiwa

mwanamke akinena kwamba Musa kazini nami, maneno yake sahihi, nifanyeni kama mtavyotaka.

Karuni akanena: mwiteni mwanamke. Akaitwa. Mwanamke alipomwona nabii Musa akamwambia mwanamke: tafadhal ntakuuliza neno. Mwanamke akanena: niulize. Nabii Musa akanena: unaona mbingu sabaa zimekaa bila miguu; nani kafanya mambo haya? Mwanamke akanena: Mngu. Nabii Musa aleihi salām akanena: nataka unene kweli kama unavyojua kwamba mbingu imekaa bila nguzo na ardhi kazalika; basi, nena kweli, mimi nimezini nawe? Mwanamke aliposikia maneno ya nabii Musa, akafanya khofu katika moyo wake kunena uwongo kumfanya mtume wa Mngu, kanena: la, ya nabii Allahu, walakin Karuni kanipa fedha maksudi nifanye uwongo; walakin mimi siwezi kunena neno lisiokuwako.

Aidha aliposikia nabii Musa maneno ya mwanamke akatambua kwamba Karuni amefanya hila maksudi amfanye fedhehi mbele za watu. Marra nabii Musa aliangua kilio akalia sana akamsujudia Mola wake akanena: ya Mola wangu wa thamma bwana wangu, wewe unaumba mimi umeniumba, angalia khabari ya Karuni ambao aliyonitenda, anataka kunitilia aibu mbele za bani Israili, naomba kwako ya Allahi unilipie kwa Karuni. Mngu akamjibu mtume wake Musa akamwambia: Ya Musa killa jambo unalolitaka amurishe ardhi, itakutendea.

Nabii Musa aliposikia maneno yale kwa Mngu akashukuru. Marra akapiga ukelele kwa sauti kubwa sana akanena: killa mtu aliye karibu ya Karuni ambaye anayemfuata Karuni na akae karibu yake, na killa mtu ambaye aliye karibu na mimi na ajitenge; maana Mola wangu kaniamurisha kwa Karuni kama alivyoniamurisha kwa Firauni. Watu waliokaa karibu na Karuni wakaondoka wote. Akabaki mtu moja. Maana sahibu yake sana Karuni naye alikuwa mtu tajiri sana akaona haya kumwacha Karuni peke yake.

Marra nabii Musa alipoona watu wote wameondoka kwa Karuni, walakin wamebaki watu wawili, yeye na sahibu yake, akajua kwamba ndio khasimu zake. Marra nabii Musa akaamrisha ardhi kwamba: watwae ardhi. Ikiwatwaa hatta magoti.

Nabii Musa akanena: ardhi watwae. Ardhi ikawatwaa hatta kiuno. Akinena: ardhi watwae. Ardhi ikawatwaa hatta kitofu. Nabii Musa akanena: ya ardhi watwae. Ardhi ikiwatwaa hatta kifuo. Na Karuni na sahibu yake wanapiga kelele, wanaomba kwa nabii Musa. Hakubali maneno yao akanena kwamba: ardhi watwae. Ardhi ikawatwaa hatta mabega. Akanena: ardhi watwae. Ardhi ikawatwaa hatta shingo. Akanena: ardhi watwae. Ardhi ikawatwaa hatta kichwa. Akanena: ardhi watwae. Ardhi ikawatwaa kabisa kabisa. Alipoona vile nabii Musa akaenda zake. Hiyo ndiyo khabari ya mtume wa Mngu Musa aleihi salām.

Aidha khabari za watu kwamba jamaa zake Karuni. Walipoona kwamba nabii Musa kamgharikisha Karuni wakanena: Musa asingetenda kitendo hiki illa anataka mali ya Karuni. Maana watu wakanena hivyo kwa sababu yeye ami yake Karuni na Karuni hana murithi illa Musa, ndio wakanena hivyo. Aliposikia nabii Musa maneno yao kwamba jamaa zake Karuni wanena hivi na hivi, nabii Musa akaomba dua kwa Mngu kwamba mali ya Karuni yagharike kama mwenyewe. Mngu akamwitikia dua yake. Na mali yake Karuni yakaghariki methili ya mwenyewe. Hiyo ndio khabari ya nabii Musa na Karuni. WAllahu a'lam.

Aidha khabari za watu wambao kwamba wafanya uhadithi hunena kwamba almasi yakuti na marjani na zumradi na sandarusi fetha dhahabu chuma shaba na vitu vingine baathi ya vitu vinavyotoka katika ardhi yaani killa maadau ya ardhi, watu hunena kwamba mali ya Karuni. Maana sasa yanatoka. WAllahu a'lam.

Kisa cha Alibegi Kashkashi.

(Geschichte des Alibeg Kaschkachi.)

Alikuwa mtu moja katika mji wa Musri jina lake Alibegi Kashkashi. Naye alikuwa a na wazimu kidogo hutoka akaenda tembea katika mji wa Musri, basi. Mle katika njia watoto

humfuata nyuma yake wakamdhihaki humpigia makelele: Alibegi Kashkashi! Alibegi Kashkashi! vivyo hivyo, hatta anakofika na kirudi vilevile, watoto wa Musri wamfuata killa siku.

Hatta siku moja katika siku Alibegi kaudhika sana kwa sababu watoto kumfuata wakapigia kelele akainama akaokota jiwe kubwa katika mkono wake akalitupa lile jiwe katika kunde la wale watoto. Likampata mtoto moja katika kichwa likampasua mahali pakubwa. Mtoto akalia sana.. Akaja baba yake akamwona mwanawe kaumia sana.

Akamwuliza: nani kakupiga? Mtoto akanena: Alibegi Kashkashi kanipiga hivi. Aliposikia baba yake maneno ya mwana we akawadhika sana kwa khabari ya Alibegi akamshika Alibegi akamchukua hatta katika hokumu kwa kadhi akamwambia kadhi: huyu Alibegi kampiga mwanangu jiwe la kichwa kamumiza mahali pakubwa basi, na mimi nimemleta katika hokumu utayokwisha wewe basi.

Kadhi akamwuliza Alibegi: nini sababu kumpiga mtoto burre? Alibegi akamjibu akamwambia kadhi: yaani ya kadhi, salla ala nabii. Kadhi akanena: Allahum salla wa salam aleihi. Akamwambia marra ya pili: ya kadhi, salla ala nabii. Kadhi akanena: Salla Allahu aleihi wa salam. Akamwambia marra ya tatu: ya kadhi, salla ala nabii. Kadhi akanena: elfu sallatu aleihi. Akamwambia marra ya ne: Ya kadhi, salla ala nabii. Kadhi akaudhika kwa makelele ya Alibegi, na Alibegi akamwambia: salla ala nabii. Hatta kadhi akachukiwa sana akanena kadhi: nimechoka makelele.

Alibegi akajibu akanena: Ya kadhi, umechukiwa kumsallia mtume, kefu mimi killa siku nikienda njiani hunipigia makelele killa siku siudhike, wewe marra moja umeuthika, kefu mimi killa siku.

Kadhi akajua kama Alibegi hana hatiya akamwambia: nenda zako Alibegi, ahsanta. Na yule akamuguza mwanawe.

Hio ndio khabari ya Alibegi Kashkashi.

Hekaya za Abunawasi.

(Geschichten von Abunawas.)

I.

Alikuwa Abunawas anapendwa sana na Harūn errashīd. Alikuwa Harūn errashīd hawezi kukaa muda wa kutwa asimwone Abunawas. Hatta siku moja alikuwa Abunawasi anataka kununuà punda naye hana fedha. Akatoka akaenda hatta nyumbani kwa Harūn errashīd. Na wakati ule si wakati wa kwenda watu kwa Harūn errashid.

Akaenda hatta mlangoni akawakuta mabawabu akataka ithini ya kupanda juu. Mabawabu wakamjibu wakamwambia: hapana rukhusa ya kwenda juu. Na bawabu wanajua kwamba Abunawasi leo muhtaji. Akatoka mkubwa wa mabawabu akanena: ntakupa rukhsa upande, walakini utachopata tutagawana sawasawa mimi nawe.

Abunawasi akanena: vema nimekubali, wakaandikiana shahada kwamba: atachopata wagawane sawasawa. Khatti ya bawabu akatwaa Abunawasi na khatti ya Abunawas akatwaa bawabu akamwambia: panda. Akapanda Abunawasi kwa Harūn errashid.

Alipofika juu asipige salamu wala asiamkie akakaa kitako kimya. Harūn errashid asipendezwe na khabari ile ya kunyamaza Abunawas akamwuliza: ya Bunawas, u na nini? Akajibu akanena: nataka unipige fimbo mia. Harūn errashid hawezi kumpiga anampenda sana akamwambia: huachi maneno haya? Bunawasi akanena: lazima unipige.

Haruni akatwaa fimbo akampiga lakini kidogokidogo walimpiga hatta zikatimia fimbo khamsini. Alipokwisha alitwaa khatti ya bawabu akanena: yuko mwenzangu, tumeagana: nitachopata huko kwako tugawane nussu kwa nussu; na sasa nimepata fimbo khamsini basi, yeye lazima aje atwae fimbo khamsini. Akamwonesha barua Haruni. Akaamurisha Haruni, ende akaletwe mkubwa wa mabawabu. Akaletwa akamwambia: mpigeni fimbo khamsini. Akapigwa akamwambia: hii adabu, usifanye

siku ya pili. Bawabu akawa zalili sana akajuta kuagana na Abunawas. Akashuka akaenda zake.

II.

Khalafu Abunawas akafanya ujanja wake akapata dinari mia akashuka akaenda zake hatta sokoni akazabuni punda akanunua akampanda. Akienda naye hatta nyumbani kwake hakushuka illa juu ya kitanda chake chumbani.

Hatta siku moja akaja mtu kuazima punda akanena: niyazime punda. Bunawasi akajibu akanena: punda hayuko. Marra punda akalia. Yule mtu akanena: si huyo punda analia, na wewe unanena hayuko. Bunawasi akajibu akamwambia: umekuja kuyazima punda ama umekuja azima mlio. Kama umekuja kuazima mlio na mimi nitalia. Akalia Abunawas: hō, hō, hō. Akamwambia: na pande. Akaenda zake.

III.

Hatta siku moja akawa punda wake a na kiu sana. Na kitu cha kumtilia maji hana. Akaenda kwa jirani wake akanena: niazime sufuria nimtilie punda wangu maji. Akampa sufuria, akaenda zake. Akakaa nayo siku tatu. Siku ya ne akatia ndani ya sufuria kisufuria kidogo akapeleka akanena: Hii sufuria yenu. Wakatwaa sufuria wakaona ndani yake kisufuria kidogo. Wakanena: hiki kisufuria si chetu.

Bunawasi akawajibu akanena: mimi si mwizi, siwezi kula mali ya watu, sufuria yenu imezaa pangu na huyu mtoto wake. Wenyi sufuria wakafurahi sana wakanena: nyumba ya Abunawasi i na baraka sana. Akaenda zake Abunawas.

Hatta siku ya tatu akaenda kuyazima marra ya pili wakampa asirudishe Abunawas, mwezi mzima akakaa nao. Wenyi sufuria wakaenda wakataka sufuria yao. Abunawasi akawajibu: sufuria imekufa. Wakanena: shaba haifi. Bunawasi akawajibu: haikuzaa? Wakanena: imezaa. Bunawasi akanena: killa kitu kinachozaa khatima yake kufa. Wakashindwa kumdai wakauliza watu maalimu wakanena: Killa kitu kinachozaa hufa. Sufuria ikapotea, akakaa nayo Abunawas. Wa salamu.

IV.

Alikuwa Bunawas katika mji Baghdadi anachukiwa sana, hatta siku moja katika siku wakamtilia fitina kwa sultani akataka kuuawa lakini kwa hila; akaambiwa: jenga nyumba ya juu kwa juu, kama hukuweza kuyenga utachinjwa na sultani. Bunawas akasema: Samaan wa tāan (nimesikia nimekubali). Akapewa muda wa kujenga nyumba siku tatu. Akasema: insha Allah. Akienda nje ya mji akafanya kartasi zake na uwanga na miti na kamba ndefu akafanya portangi (tiara) kubwa sana. Akafunga na kengele nyingi sana akangoja baridi akarusha na kamba akaifunga katika mti. Likaruka portangi katika hawa hatta katikati ya mji.

Watu mjini wote wanaona portangi, na kengele zinalia, na wasituka sana na khabari ile. Maana hawajapata kuona kitu namna ile. Alipoona Abunawasi shughuli yake imetengenea akaenda mbio hatta nyumba ya sultani akafika mlangoni akataka ithini yakuonana na sultani akapewa rukhsa akapanda hatta juu akamwona sultani akamwambia: nimekwisha jenga nyumba, fungua dirisha, utazame.

Akafunga dirisha sultani akamwonesha akamwambia: unaona ile? Akamwambia: naona. Akamwambia: ndio nyumba niliyoijenga. Akamwambia: unasikia vitu vinalia; akamwambia: nasikia. Akamwambia: mafundi wakafanya sakafu, na hizo zinazolia nyundo na mismari, wallakini zimepungua mbao kidogo, tafathali sultani, toa watu wapeleke mbao. Sultani akastaajabu sana maneno yale, akanena: watapita wapi watu wapeleke mbao. Akanena Bunuwasi: iko njia niliopita mimi kwenda jenga.

Akatoa mbao sultani akawapa watu akawambia: pelekee mbao. Wakafuatana nao Bunawas hatta alikofunga kamba, akawaambia njia hii. Watu wakanena: hatuwezi kupita juu ya kamba. Akamwambia: sharti mtapita. Wakanena: hatuwezi kupita. Wakarudi kwa sultani wakanena: hatuwezi kupita juu ya kamba.

Sultani akanena: Hakuna mtu awezaye kupita juu ya kamba kwenda juu. Bunuwasi akamwambia: unajua haya;

kwamba mtu hawezi kwenda katika elhawa. Akamwambia: najua. Akamwambia: kwa nini ukanambia: nijenge nyumba katika elhawa? Sultani asiweze kumjibu akanyamaa kimya. Akatoka Bunawas akaenda zake akakata kamba, likaruka portangi likapotea. Ndio asili yake portangi, kazi ya Bunawas. Wa salaam.

V.

Alikuwako mzee mmoja na mwanawe naye yu maskini sana yeye na mwanawe. Akaondoka tajiri mmoja akamwambia yule kijana: nenda kaingie katika ziwa la barafu ukae hatta assubuhi, ukikaa hatta assubuhi ntakupa dinari asharat alāf. Yule kijana akaenda akaingia magharibi hatta assubuhi. Na mama yake alikuwa akimurika kwa moto kucha.

Assubuhi akienda kwa yule tajiri akamwambia: nipe fedha yangu. Akamwambia: sikupi. Akamwuliza: kwa nini hunipi fedha yangu; na mimi nimekaa katika bardi kucha. Akamjibu: mama yako amekufanzia moto kucha. Akamwambia: la, moto akinimurika basi. Akamwambia: la, uwongo. Akaenda akamshitaki kwa Bunawas. Akasema: vyema, maneno yako nimesikia, walakin utanipa kiasi gani utakapopata mali yako. Akamwambia: ntakupa elfu mbili. Akamwambia: la, nipe tatu. Akamwambia: ntakupa. Akamwambia: enenda kumshitaki kwa sultani kwanza. Akaenda kumshitaki kwa sultani. Sultani akanena: tajiri huyu kweli maneno yake na weye hu na haki. Akaondoka akaenda zake yule kijana hatta kwa Abunawas akamwambia: nimeshitaki kwa sultani sikupata haki. Akamwambia: kesho jioni utapata haki yako kwa fadhili ya Muungu.

Bunawasi akanunua mbuzi na mchele na samli akanunua na vizari na vitu vyote vya karamu. Akachinja mbuzi akachuna akatia nyama ndani ya sufuria na mchele akatia katika sufuria akakoka moto mbali na vyakula akaweka mbali. Akawaalika sultani na mawaziri na matajiri wote wa mjini wakaenda wakakaa wakabarizi tokea ussubuhi hatta jioni wasipate hatta kahawa. Watu wakakasirika wakaenda wakachungulia mekoni. Wakaona nyama iko mbali na moto uko mbali na watu wanatia moto sana.

Sultani akamwambia: Weye Bunawasi umefanya wazimu sasa. Akamwambia: kwa nini maulana? Akamwambia: tokea assubuhi tumekaa hapa hatta sasa hatuioni ile karamu uliotuitia. Akamwambia: Watu wanapika walakin nyama haijawiwa. Sultani akaenda akatezama. Akaenda akaona sufuria ya nyama iko mbali na moto uko mbali. Akamwambia: nyama hii haiwiwi hatta kuwa miaka kumi. Akamwambia: itawiwa. Akamwambia: haitawiwa na mimi nitakwenda zangu na watu ntawaambia waondoke.

Akamwambia: usikasirike, sababu yule kijana aliolala usiku kucha katika barafu, nawe umesema kana amepata moto katika barafu naye mama yake kwa uchungu wa mwana akimwurika kumtazama. Naye amekuja kushitaki kwako hukusadiki, basi, tafadhal mpe haki yake maskini ya Mngu. Maana hakupata moto na kana amepata moto na nyama ingalipata moto. Sultani akasema: kweli, akaenda akamwambia tajiri: lazim yule kijana umpe haki yake. Basi. Abunawas akiwaamrisha watu kupika vyakula wakala wakaregea katika mji. Akaitwa yule kijana akapewa fetha yake asharat alāf dinari.

VI.

Alikaa Bunawas alikuwa na mkewe akamwambia; leo muhtaji sana basi, uipe mashauri. Akamwambia: sina shauri mume wangu illa weye utafanza. Akamwambia: mimi takwenda kwa sultani nitamwambia: mke wangu amekufa, na wewe uenende kwa mke ndani utasema: mume wangu amekufa, ukipata fetha na mimi nikipata tutakuja kutumia. Wakaondoka wakaenda. Bunawas akaenda barazani akasema: mke wangu amekufa. Na mke we akasema kwa bibi ndani: Abunawas amekufa. Bunawas akapata saanda na fetha na vitu vyote, na mkewe akapata ndani vilevile. Wakaenda wakagawana.

Sultani alipoingia ndani akamwambia mkewe: Mke wa Bunawas amekufa. Na mke akamwambia: Bunawas amekufa. Kulla mtu akacheka. Sultani akapeleka watu wakaenda wakaona mke wa Bunawas anamtia maji mumewe amevaa saanda. Akasema: mume wangu amekufa, na watu wakamsayidia

kufanza saanda. Walipotaka humtia katika jeneza akasema: Jukhuri ulhai min elmait wa jukhuru ilmait min elmait. Watu wakamtoa wakampeleka kwa mfalme. Sultani akamwuliza: umeniambia uwongo kwa kuwa mke o amekufa. Akamwambia: nimekwambia kweli, ussubuhi nalikufa mimi akaja mke wangu kwa mke o Zubeide akasema: mume wangu amekufa; nikafufuka mimi akafa yeye, nikaja kwako nikakwambia: mke wangu amekufa. Na leo Muungu anaondoa kilicho hayi ndani ya maiti anaondosha maiti katika hayi. Watu wakacheka.

VII.

Alikuwako mtu moja mzee akamwambia Bunawas: tucheze bao. Akamwambia: sitaki. Akamwambia: lazim tucheze. Akamwambia: sichezi mburre. Akamwambia: nini unataka? Akamwambia: nataka tucheze kwa mashindano. Yule mzee akamwambia: kama mashindano yapi? Akamjibu: ukinishinda ntakupa dinari tano, ni kikushinda nitakutia maji matakoni. Akamwambia: haya. Wakacheza. Mzee akashindwa. Bunawasi akasema: ondoe nguo zako nikutie maji. Akamwambia: mimi mzee na ndevu nyeupe unistahi. Akamwambia: kama weye ungalishinda mimi singalinisilahi ungalitaka dinari tano. Akamwambia: haya; mzee akavua nguo. Bunawas akachukua paka wake akaenda kumtia paka na maji na yule mzee. Paka akamparura yule mzee paji akatoka damu. Akaenda akashitaki kwa Harūn irrashid. Akaletewa askari akaenda kwa mfalme na paka wake pamoja ndani ya nguo. Mfalme akamwambia: weye umemparura huyu mzee. Na yeye akamwambia: huyu paka amemparura. Mfalme akamwuliza: kwa nini? Bunawas akajibu: mimi nimemtia maji, na paka ndiye aliyemparura, basi; na paka alimparura huyu; ukimtia gerezani ao ukimchinja ao ukimpa maskini kuchukua, haya.

Wa salaam.

Wanawake watu gani.

(Werth der Frauen.)

Alikuwako mtu mmoja mwanamume akaoa mke akakaa na mke we siku nyingi ampenda sana mke we, hawezi kumfariki hatta saa moja kwa hali anavyompenda.

Hatta siku moja katika siku ikafika ajili yake mwanamke akafa. Akamzika mke we akafanya matanga makubwa sana akawa na msiba, hali wala hanywi, kazi yake kulia, haogi wala hafui nguo akawa nyele zake anakalia.

Hatta siku moja katika siku akapita nabii Musa aleihi salām kwa sura ya mtu mzee akamwona yule mtu aliyefiwa na mke we akamwuliza: kēf halak?*) Yule akajibu: taiyib.*) Nabii Musa akamwuliza: u na nini wewe bini Adamu; nakuona katika dhiki sana: Akamwambia: nilikuwa na mke wangu, nampenda sana na sasa amekufa, basi; mimi si na tabassam kabisa, nafanza msiba hatta ajali yangu ifike, nife, basi.

Nabii Musa akamwambia: ewe bini Adamu, tafuta mke mgine uoe uondoshe msiba ukae na furaha ushukuru Muungu. Yule mtu akajibu akanena: siwezi kwa hali navyompenda mke wangu, nitakaa na msiba hatta nife. Nabii Musa akamwambia: ma samehin almaraa illa mararit ilkulūbu.*) Maana yake: wasingekwitwa maraa wanawake illa wa na nyongo katika rohoni mwao.

Yule mtu akajibu akasema: walau maana yake iyapokuwa, walakin nampenda. Nabii Musa akamwambia: ma samehin ilharīm illa harram Allahu kulūbuhum.*) Maana yake: wasingekwitwa harīm waanawake illa Mwenyiezimgu kawaharimisha mioyo yao. Yule mtu akajibu: walau maana yake iyapokuwa mimi nampenda.

Akamwambia nabii Musa: ma samehin niswān illa nisiyāni il fadhil. Maana yake: wasingekwitwa niswān illa husahau fadhili sana. Yule mwaname akajibu: walau, nampenda.

Nabii Musa akamwambia: Umuri wako miaka thelathini uliobakia hatta utapokufa; akhiari, ondosha msiba, maana utazili sana. Akamwambia: walau. Akamwambia: utaweza kutoa nussu ya umri wako umpe mkeo a fufuke, na siku ya kufa mfe pamoja? Maana umri wako miaka thelathini, khamustashara mupe wako mke o, khamustashara uwe wako wewe.

Akajibu mwaname: semaa wa taa, ninapenda sana namna hiyo. Basi. Wakaenda hatta kaburini. Akamwambia nabii

*) arabisch.

Musa: sema: nimekupa umri wangu nussu, ya fulani binti fulani. Nabii Musa kapiga fimbo katika kaburi akafufuka mwanamke, akamwambia mwaname: chukua mke wo. Nabii Musa akaenda zake.

Na yule akaondoka akafuatana na mke we akaenda zake. Akafurahi sana siku ile, wanakwenda njiani yule na mke we hatta walipofika kati ya njia akaona mti mkubwa u na kivili kizuri sana. Akamwambia mke we: natupumzike hapa kidogo; wakikaa kitako chini ya mti. Yule akapata usingizi mwaname kwa furaha nyingi ya kumpata mke we akalala kidogo.

Yu mo katika usingizi, yeye akalala na mke we kakaa kitako. Marra si marra akapita mtu moja khayali, mwaname mzuri sana, akamwona yule mwanamke; na yule mwanamke mzuri sana. Yule khayali akamwambia: unafanya nini hapa chini ya mti? Mwanamke akajibu: napumzika. Akamwambia: huyu aliolala nani? Mwanamke akamjibu: simjui mtwana huyu. Akamwambia: unakwenda wapi sasa? Akamwambia: sijui nnakokwenda. Akamwambia: unataka nikuchukue twende kwetu? Mwanamke akamjibu akamwambia: naam, nataka. Akamwambia: njoo tupande farasi twende zetu. Akaondoka mwanamke akataka kupanda farasi.

Marra mume we akazindukana akaamka akanena: Unapeleka wapi mke wangu? Yule khayali akamjibu akamwambia: umpate wapi mke kama huyu, huna adabu wewe. Yule akasema: mke wangu. Na khayali akasema: mke wangu. Wakagombana sana wakenda katika hokumu hatta kwa nabii Musa. Lakini yule mwaname hajui kwa kuwa yule ndiye nabii Musa, maana sura nyingine akajigeuza. Lakini nabii Musa anajua kwamba ndiye huyu mtu na mke we.

Wakashitakiana khayali na yule mwaname. Yule mwaname akasema: mke wangu huyu. Na khayali akasema: la, si mke we; huyu mke wangu mimi. Nabii Musa akasema: kweli anajua mwanamke, tutamwuliza mwanamke. Nabii Musa akamwuliza mwanamke: Ya ghulama, nani mume o katika wawili hawa? Mwanamke akajibu akamwambia: mtwana huyu

ana wazimu; atapata wapi mwanamke kama mimi; mimi, mume wangu huyu khayali; lakini huyu a na wazimu.

Nabii Musa akamwambia: wasikia maneno wa mwanamke? Akamwambia: mimi nasikia. Akamwambia: sikukwambia mimi kama: ma samehin nisaa lla nisyān ilfadhili. Maana yake: sikukwambia mimi kama wasingekwitwa niswani illa husahau fadhili sana. Akamwambia: naam, ya nabii Musa.

Nabii Musa akasema akamwambia mwanamke: Mboni huyu anahudai kwa kuwa wewe mkewe? Mwanamke akamjibu: majnuni huyu. Akamwambia: kitu kimoja hokumu yangu, nitahokumu. Mwanamke akamwambia: hokumu. Akamwambia: kama wewe ni mkewe kweli, huyu hana buddi illa kutoa mahari, hatta kakupata, basi; waweza kumrudishia mwenyewe?

Mwanamke kamjibu: hakunipa kitu huyu mimi, nimrudishie nini? Nabii Musa akamwambia: sema: kwa kulla kitu alichonipa nimerudishia mwenyewe kama kanipa kitu. Mwanamke akanena: kama kanipa kitu nimemrudishia mwenyewe. Akaanguka akafa mwanamke.

Nabii Musa akamwambia khayali: chukua mke wo. Khayali akamjibu: kabisa simjui kahaba huyu. Akapanda farasi wake akampiga akakimbia zake. Nabii Musa akamwambia mwaname: sikukwambia mimi kama waanawake si kitu. Akajua yule mwaname kwa kuwa waanawake si watu wema.

Akamzika yule mwanamke akajitengeneza yule mwaname akafanya uzuri sana akaoa wake wane baada ya yule mmoja akakaa raha mustarehe.

Hii ndio khabari ya waanawake si watu wema.

Kisa cha sungura na cheche.

(Die Geschichte vom Fuchs und vom Ichneumon.)

Aliondoka cheche akamwambia sungura: mimi si na mke wala si na mama wala si na mtoto, na wewe kamān, hu na mke hu na mtoto, afadhali tu kae pahali pamoja mimi na we, tutachopata tule; na siku tusiopata, tushukuru Mngu.

Sungura akasema: vema taiyib, mashauri yako mema; wakakaa mahali pamoja. Na kazi yao wakatega ndege wakila. Hatta siku moja wakaenda maguguni kutega ndege wakagundua pahali mayayi ya kanga. Sungura akamwambia: tutege kanga. Cheche akasema: vema. Sungura akaenda akafanya mtego akatega akanasa kanga akamchukua hatta nyumbani kwao.

Sungura akamwambia cheche: kanga huyu mchome na mayayi yachome, mimi nimechoka ntalala kidogo. Cheche akasema: vema; akachoma. Sunguru akalala. Alipoiva kanga cheche akasikia arufu nzuri mno ya kanga akamla wote na mayayi akala. Akatwaa yayi moja ganda lake akalitengeneza vizuri akaliweka akalificha mahali sana. Akatwaa manyoya yaliobakia na miguu ya kanga akatia motoni naye akalala.

Yakanuka manyoya katika moto yanaungua. Sungura akazindukana kwa arufu akamwamsha cheche akamwuliza: kanga ilikuwa pi? Cheche akasema: nimemwacha hapa katika moto usingizi ukanishika nikalala, basi, kaungua kanga. Sungura akasema: basi.

Lakini sungura anajua kama cheche kamla kanga walakin kasingizia moto. Sungura akasema: twende kwetu, twende kutafuta chakula. Cheche akasema: vema, na mimi nitakwenda kwetu sasa hivi. Sungura akaondoka akaenda zake akajificha mahali. Cheche akashiba sana akalala. Sungura akatafuta majani ya ngomba akaenda polepole hatta karibu ya cheche. Akamfunika majani akamfunga vema akampiga sana, cheche akalalamika sana. Khalafu sungura akaenda zake.

Cheche akalia khalafu akanyamaza, na mtu aliompiga hajui. Akaja sungura akamsukuma cheche kwa miguu yake akasema: nini hichi? Akamsukuma. Cheche akamwambia: mimi hapa rafiki yako. Akamwuliza: u na nini? Akamwambia: akaja mtu akanifunga akanipiga sana. Sungura akanena: unamjua mtu huyu? Cheche akamsema: simjui. Sungura akasikitika sana akamfungua akamwona akataabika mno. Wakakaa kitako.

Hatta siku moja katika siku pakatokea kiumbizi kwao cheche. Cheche akamwambia sungura: Nakualika kwetu, kuna kiumbizi leo. Sungura akasema: vema, walakini nitakwenda

kwetu kwanza, alasiri ntakuja. Cheche akasema; vema, basi. Sungura akaenda zake.

Cheche akaoga akavaa nguo zake akatwaa yayi la kanga akavaa kichwani akatwaa nyoya la kanga akachomeka juu la yayi akaenda zake kwao akacheza kiumbizi hatta alasiri. Akaenda sungura katika kiumbizi. Alipomwona cheche sungura akamkaribisha akakaa kitako sungura.

Marra cheche akatwaa zomari akapiga:

Kanga pia singizia moto, ti! ti! ti!

Maana yake: kanga nimemla wote. Sungura akasikia maneno yale katika zomari akaruka akashika ngoma kubwa akapiga:

Nikamtwaa nikamfungafunga na majani ya mgomba nikampiga, pu! pu! pu!

Cheche akasikia maneno ya ngoma akakasirika mno akashika fimbo wakapigana sana, hatta mashikio ya cheche akatwaa sungura na mashikio ya sungura akatwaa cheche.

Ndio maana ya sungura na mashikio marefu. Kwanza yalikuwa cheche na mashikio marefu, sungura alikuwa na mafupi.

Mwisho.

Maneno matatu.

(Drei Worte.)

Aliondokea kijana moja na wazee wake akakaa; siku kaza wa kaza zikapita hatta mwaka moja katika miaka baba yake akafa na mama yake akafa, akarithi mali kwa baba yake na mama yake. Na ajtamal ya mali hayo elfu tatu aliorithi.

Akakaa katika dunya yule kijana aliyeusiwa na baba yake mambo matatu. Akaambiwa: mwanangu mambo matatu haya tafathali yakamate, ya mwana, usiyasahau, Allah, Allah; yatakuja kukufaa mwanangu. Khalafu hayatendapo mali yako yakiisha. Yule kijana akasema: naam, kweli baba.

Hatta khatima yule kijana akafilisika akahama katika mji wao akasafiri akaenda kunako mji mungine akafikia katika

nyumba ya tajiri akakaa siku mbili. Hatta siku ya tatu akamwambia sheikhi tajiri: mimi nimekuja kwako, tafadhali, nataka unipatie kiwanja, nataka kujenga nyumba nifanye duka.

Na yule tajiri akamwambia: Insh Allah, utapata walakin unataka kuuza nini katika duka lako, na weye hukuchukua mali huko unakotoka. Akamwambia: nataka kuuza maneno matatu na thamani ya neno moja reale elfu mbili; na maneno hayo ni mausia na baba yangu, basi.

Yule tajiri akampa kiwanja akajenga duka lake hatta alipokwisha kujenga akaweka kiti mlangoni akakaa. Alhasil na kulla mtu apitaye humuliza: unauza nini hapa? Naye hujibu: nauza maneno ya wasia. Watu humwuliza thamani ya neno moja kiasi gani. Yeye husema: neno moja elfu mbili reale. Na kulla mtu asikiaye maneno yake humwambia: u na wazimu, huenda zake.

Hatta siku moja akaja kijana mmoja anakaa pale akamwambia: salam aleika; akamwitikia: wa aleik salamu. Akamwambia: karibu. Akamwambia: astarehe. Akakaa yule mgeni akamwuliza: akhi unauza nini hapa? Akamwambia: mimi nauza maneno hapa. Akamwambia: themani yake kiasi gani neno moja. Akamwambia: neno moja themani yake elfu mbili reale. Akamwambia: Mbona ghali ya akhi? Akamwambia: si ghali, kwa mtu atakaye na mtu ajuaye.

Akamjibu: mimi ya akhi mji huu mgeni na mimi nimerithi kwa baba yangu elfu sita, si na zaidi. Akamwambia: mimi sijui, mimi najua themani ya kilme elfu mbili; na kama unataka nunua.

Alhasil akamwambia: nataka. Akampa elfu mbili, akamwambia neno moja akamwambia: Ukiona neno usinene neno na ukinena neno litakujia neno, wasalam.

Akamwambia: nambia la pili. Akamwambia: lete elfu mbili reale nyingine nakwambia la pili. Akampa elfu mbili. Tena akamwambia la pili: ukisafiri katika bara jua likikuchwea njiani lala hatta na kama unakokwenda unakuona Allah Allah lala, wa salām.

Akamwambia: nambia la tatu. Akamwambia: lete elfu mbili reale. Akampa elfu mbili reale. Akamwambia la tatu. Akamwambia: ukienda njiani ukiona mtu akakukaribisha ya kwanza mwambie astarehe, mara ya pili kazalika, mara ya tatu, tafadhal kaa kitako, wa salām.

Yule kijana mali yake aliorithi elfu sita yote yakiisha akawa maskini akafanya kazi katika ule mji akapata mia mbili reale akanunua ngamia reale mia na reale mia akanunua bidhaa akatoka ule mji aliokuwa akaenda hatta akafika mji mgine. Akapata rafiki kwenda naye kufanya biashara. Akamwambia: unakwenda mji gani ya akhi? tufuatane. Akamwambia: mimi nakwenda kutarazaki kutafuta riziki na weye na kama unataka tafadhali tuende, walakin nunua ngamia awezaye kukuchukua bidhaa zako. Akamwambia: insha Allah taala, yule rafiki yake.

Akaingia katika mji akatafuta ngamia akapata akanunua, akatafuta na bidhaa akanunua alhasil wakalala. Siku ile wakatengeneza shughuli yao wakaisha. Hatta siku ya pili wakapanda ngamia zao wakasafiri alhasil wakaenda siku arbaa wa ishrini wasipate mji wala wasione mji alhasil. Hatta kwa siku ya thamania wa ishrini wakaona moto wakasikia na majogoo kuwika na jua limekuchwa.

Yule aliyenunua maneno akamwambia mwenziwe: ya akhi, mimi ntalala hapa maana jua limekuchwa. Mwenziwe akamwambia: la, ma yumkin, tumelala ya akhi siku kazawakaza katika mwitu na leo tumefika katika mji si afdhali kwenda mjini, na sasa tumefika. Akamwambia: la, ndilo neno lisiopatikana hilo la kuingia mjini. Yule asiyenunua maneno hajui maana ya kukatalia kwenda yule mwenziwe nini.

Alhasil akaondoka yule asiyenunua maneno akasema: mimi silali hapa; mwenziwe akamwambia: kana vile unavyotaka, walakin mimi naona afdhali ulale hapa. Yule akasema haihati mimi kulala hapa na ule mji tunaotaka tumefika. Akamwambia: nenda ya akhi. Yule akaondoka akaenda zake yeye na ngamia wake. Na yule akalala hatta asubuhi akaamka akapanda ngamia wake akaenda zake hatta akafika katikati

ya njia amwona rafiki yake amekufa na ngamia wa rafiki yake amekufa.

Akatazama sababu iliyomwua nini rafiki yangu akaona mkuruzo wa nyoka. Na nyoka huyu nundu amemtopoa katika utosi. Na ngamia katopolewa katika utosi. Wote wawili wamekufa. Akasema: Alhamdu lillah rabb ilalamina, sasa fayida ya elfu mbili nimeona bado, elfu nne sijaona bado.

Alhasil akashuka akaingia katika mji akatafuta watu wakuzika akapata akazika rafiki yake akashukuru akakaa katika ule mji. Siku nyingi zikapita. Khalafu akamwona sultani njiani akamwita akamwambia: unatoka wapi, kijana weye? na asili yako wapi weye?

Akamwambia: Mimi bwana maskini ya Muungu, kwetu mbali na hapa gharibu. Sultani akasema: njoo ukae kwangu, unitilie kahawa. Akasema: heiwallah, ya saiyidina. Akaenda akakaa kwa sultani kutia kahawa. Na yule sultani akampenda sana akamwambia: sasa usitie kahawa, kwa kana watu wanaokuja barazani. Akasema: heiwalla maulana. Akakaa siku nyingi kwa hali ileile.

Alhasil sultani akampenda sana akamwamini sana, tena akampa libasi nzuri na majambia mazuri, akamwamini hatta katika nyumba yake ndani kwa wake wa sultani akaingia. Aidha siku moja sultani akatamani kwenda kutembea kwinza nyama. Akamwambia: tuende, tufuatane wote. Akasema: heiwallah. Sultani akaenda naye hatta wakafika katika njia. Sultani amesahau saa yake ndogo akamwambia: tafadhali rudi nyumbani katika chumba changu kwa mke wangu mdogo utaona saa yangu katika shibaka, tafadhali lete sasa hivi.

Akasema: heiwallah maulana. Akaenda yule kijana hatta akafika akaingia ndani akaingia chumbani akamkuta yule mke wa sultani na waziri katika kitanda cha sultani wamelala. Yule kijana asiseme neno akatazama kazi yake aliyotumwa akafanya akaichukua ile saa akaenda zake akafunga mlango vilevile akaenda hatta akafika kwa sultani akampa saa. Yule sultani akamwambia: nini khabari ya nyumbani. Akamwambia: kheiri.

Alhasil yule waziri siku ya pili akawaambia mabawabu: nendani shamba, mkachimbe shimo kubwa sana, atakuja mtu kutazama; akija mkamateni mumtie hatta nikawa mimi. Mabawabu wakasema: heiwallah waziri, semaa wa taa ya waziri, bassi. Wakaenda wale mabawabu shamba wakachimba shimo kubwa.

Na yule waziri alipojua ya kama shimo limekwisha akamwambia yule kijana: tafadhali nataka kukutuma shamba. Yule kijana akasema: heiwallah waziri. Akamwambia: nenda. Akaenenda yule kijana. Hatta alipofika njiani akaona mtu anayemjua baba yake zamani akamwambia: ewe kijana unakwenda wapi huku? Akamwambia: nakwenda shamba. Akamwambia: tafadhali karibu. Akasema: astarehe. Karibu. Astarehe, marra ya tatu. Akakaa hatta akasahau shamba alikotumwa.

Huko nyuma waziri akasema: labuda sasa wamekwisha kumfukia yule kijana, nitakwenda kutazama sasa. Akaondoka waziri akaenda. Alipofika mabawabu wakamkamata waziri wakamtia katika shimo wakamfukia.

Na yule kijana hatta alipopata fahamu akamwambia yule mtu: mimi nimetumwa na waziri nimesahau na sasa nataka kwenda zangu. Akamwambia: haya enenda. Akaenda zake akafika shamba akawaona mabawabu akawauliza: je? mnatoka wapi huko. Wakasema tunatoka shamba kwetu, waziri amesema: chimbeni shimo shamba na atakayekuja yote mtieni hatta nikawa mimi, na sasa amekuja yeye waziri tumemtia yeye, wa salām.

Yule kijana akasema: Alhamdu lillah rabb ilalamina, shimo hilo langu mimi hapa, walakin Mola amenivua mimi.

Bassi, wakarudi mjini hatta wakenenda kwa sultani, sultani akamwuliza: mnatoka wapi? Yule kijana akasema: tunatoka shamba. Yule kijana akasema khabari ya waziri yote tokea mwanzo hatta mwisho. Na khalafu akasema khabari yake yote alionunulia maneno kwa reale elfu sita. Sultani akamwambia: maneno hayo ulionunua ni ghali. Akampa elfu ishrini na sita akamwambia wewe sasa waziri wangu mkubwa, wa salām.

Wa katabahu ilhakir Allahu taala Amur bin Nasur il-Omeiri fi arth issultan iljerman Berlin. Huu ndio ukomo wake kisa hiki na hadithi hiyo. Na mimi nimeipata kwa ndugu yangu Khalid bin Muhammed bin Surūr ilOmeiri katika Unguja na mimi nataka kuibadili kwa lugha dachi kwa bwana waugu iddaktari Bittner mwalimu kwa lugha ya kisawahili. Wa salām. Tamat bikheiri.

Kisa cha Mwarabu na Mgunya.

(Die Geschichte von einem Araber und einem Mgunyamann.)

Aliona mtepe Mwarabu unakwenda Amu. Akawaambia: ntakupeni vitu mpeleke Lamu. Wakamwambia vema. Akapakia Mwarabu magunia ya tende katika mtepe na nauli akawapa wakatweka Wagunya.

Hatta baharini wakaona mtepe u na sheheni nyingi sana hauwezi kwenda. Nakhodha akasema: Yule Mwarabu akapakia nini, ela tezameni katika makanda. Wakakata gunia moja wakaona tende wakathani ukwaju wakasema: a na wazimu Mwarabu yule katupa kwaju kupakia katika mtepe wetu hatta mtepe unataka kuzama, yatoseni makanda. Wakayatosa.

Wakasema: moja liacheni tuungie mchuzi. Wakalacha moja. Na mle ndani ya mtepe kuna mtu moja jina lake Mchendewa, hawezi a na kidonda miguuni akaona baridi sana. Aka-nena ndani ya moyo wake: hela niende nikatwae ukwaju nile. Akaenda hatta chini akatoa kisu chake akakata kanda akatwa akala kidogo akaona tamu sana. Akakaa palepale anakul watu mtepeni wakamtafuta hawamwoni.

Wakamtafuta sana. Nakhodha akasema: tafuteni san labuda katumbukia majini. Wakamtafuta hatta wakamgund chini kunako gunia la tende wakamkuta amekaa kitako an kula. La gunia upanda mzima limekwisha. Wakasema hu a na wazimu, a na nini, anakula ukwaju; hela na tuonje sisi. Wakaonja wakaona tamu.

Wakapigia makelele wakaitana wakala tende yote wak mpeleke nakhodha wao kidogo. Akala nakhodha wao aka

ambia: huu si ukwaju ni chende, rudisheni mtepe. Wakapindua matanga wakasema: andamieni, hatta wakafika walipotosa makanda.

Akasema: izamieni. Akazamia wa kwanza, akafa. Wakathani labuda amekaa kitako ndani ya maji anakula. Akasema nakhodha: mwandamieni. Akazama wa pili akafa. Wakasema: labuda wamefanza mashauri wao wanakula wote, mwandamieni. Akazama wa tatu, akizama moja moja hatta wakeesha akabaki nakhodha na serahangi, basi.

Hawa wamefanza shauri: wote wanakula tende chini ndani ya maji, mwandamie. Serahangi akajitia baharini akazama akafa. Akabaki nakhodha akasema: huyu serahangi amefanya shauri pamoja na mabaharia wanakula tende wote. Akasema: nami ntawaandamia. Akajitosa akafa.

Akabaki ndani ya mtepe yule Mchendewa peke yake naye kujitosa hawezi, a na kidonda miguuni, anaogopa maji ya chumvi. Akageuza mtepe akatweka peke yake hatta akafika Amu. Watu wakacheka sana, bassi.

Hatta leo tena Mgunya ukimwambia: si ukwaju ni chende, akasirika sana.

Mzee kipofu na bunduki yake.

(Der blinde Greis und sein Gewehr.)

Alikuwako mzee moja kipofu ndani ya baghala. Na yeye anataka kuabiri kwenda katika inchi ya Maskati akafika Basra. Akakaa pwani bandarini, nokhoza akashuka na mabaharia wake. Akabaki yule kipofu na sanduku lake na mtumwa wake mdogo. Bassi. Akaja mwizi akamwibia sanduku lake.

Mwivi akaja ndani ya maji akajitwika majani juu ya kichwa akaogelea akaja hatta akafika katika chombo. Akaliona sanduku la yule mzee kipofu akaliba, na yule kipofu hana khabari. Akalichukua hatta pwani akampigia makelele. Mwivi akasema: Ewe mzee, ewe mzee kipofu. Akasema: nami. Akamwambia: wewe ulio chomboni. Akaitikia: naam. Akamwambia:

wakija mabaharia na nokhoza usiwakamate, sanduku lako nimechukua mimi. Akamwambia: sema tena. Akamwambia: Ikiya nakhoza na mabaharia usiwakamate, sanduku lako nimelichukua mimi.

Na huku yule mzee kipofu anatia risasi katika bunduki yake akamwuliza marra ya pili: sema tena. Akamwambia: kana umesikia sikia; kana hukusikia bassi. Hakudiriki kumaliza maneno illa amempiga risasi ndani ya kinywa akamwambia mtumwa wake: nende karudisha sanduku, mwizi amekufa. Akaenda akarudisha sanduku akaona fedha kamili.

Asili ya mgomba.

(Die Entstehung der Bananen.)

Watu walikuwa wakagombana na watu hawo ni wawili bassi. Wakenda panapo shimo wakenda wakasema maneno yao katika shimo wakasema: sisi hatugombani tena, na maneno yetu tunatia shimoni tupate kuridhia. Na hatta assubui wakaona mche ndani ya shimo. Wakasema: mche huu ni mti gani? Mmoja akasema: na mimi si vilevile sijui. Ukakaa mche ule ukakua hatta ukawa mkubwa ukazaa, wakasema: ule mche umezaa sasa. Mmoja akasema: ule si mche, ule ni mti; na mti ule jina lake mgomba, ni ule ugomvi letu na matunda yake ndizi ni kule kuridhiana kwetu. Akasema: naam, sahihi. Ndipo ukawa mgomba na ndizi.

Kazi ya shamba.

(Von Feldarbeiten.)

Watu wanaokaa mashambani: msimamizi na nokoa na mukadamu. Msimamizi ndiye mwenyi kutunza vitu vyote ndio mwenyi mamlaka ya kazi zote, lakin si shamba lake wala si watumwa wake. Na nokoa ndio mwenyi mamlaka ya kazi zote na kutazama vitu vyote. Na mukadamu ndio mwenyi mamlaka ya kupiga makoongo na kupiga mrabba; nakutazama kazi na kutunza kazi zote na vinavopandwa na vitu vinavolimwa na vinavovunwa juu ya mukadamu, nakutazama watumwa, huyu

mzima au mgonjwa juu ya mukadamu. Hiyo ndio shughuli ya watu hawa. Na katika shamba na mipaka na ukomo wa mashamba na mapana ya shamba na gunda na k'oto. Mwenyi shamba lake gunda na k'oto mashamba ya watumwa wanaolima wenyewe.

Na kwa kulla shamba la mtu mwenyi mali namna yake hii. Hupanda migarafuu na minazi na michungwa na miembe na mibibo, hupandwa na mananasi katika njia na embe Burbo karibu na nyumba na embe dodo. Hupandwa shambani na mapera na mapera ya kizungu. Na shamba liliokuwa hivi themani yake inapata tokea elfēn reale hatta ashara elfu reale. Na mashamba hayo ya upande wa Donge au Mzizima au Nyanjale au Mangapwani au Dole au Kizimbani au Mkokotoni au Kinduni upande huu au Kitope. Ndio kunako mashamba yenyi themani hizi. Hupatikana shamba la tokea elfu mbili hatta elfu eshirin themani yake. Sababu ndio Unguja mwenyi nguvu ya mashamba mahala humo.

Fuoni au kwa Kidoti au kwa Wira au Miembe miwili au Mbiji au Uzini au Kwarara hapana themani mashamba walakin Viungani na Chukwani au Nyangombe an Miwaleni au Sebuleni au Felejini au Mtoni hatta Bububu hapana migarafuu lakini ghali, sababu karibu na mji. Na kulla shamba kana hali na migarofuu themani yake huwa chache, illa likiwa karibu ya mji, themani yake huwa zaidi kuliko lenyi migarofuu.

Katika khabari ya mapando ya garofuu. Kwanza watu wanaotaka kupanda migarofuu wanachukua mbegu garafuu walakin si kana garafuu, nene, nazo nyeusi nazo haziuzwi, hapana atayenunua. Huchukuliwa zikatiwa katika maji zikarowekwa khalafu hukobolewa na huchukuliwa kiini cha ndani, watu wakafanza banda, kibanda chembamba, wakaburuga ndani ya kibanda wakiisha wakapanda. Na hukaa miezi mitatu ndipo ikatoa mche na khalafu huchimbuliwa miche inapokuwa mikubwa. Watu wakaenda wakapiga mirāba katika shamba wakachimba na mashimo ndipo inapongolewa miche ikatiwa katika mabango ya migomba ikaenda ikapandwa; na kwa kulla ufapo

mgarafuu moja hupelekwa wa pili hatta ikashika yote. Hii khabari ya garofuu.

Na baada ya miaka sita mgarofuu huvunja ungo, huanza kuzaa.

Khabari ya nazi: hulimbikwa nazi juu ya minazi muda wa mwaka hatta zikakauka makumbi keesha huanguliwa zikavumbikwa ndani katika ghala muda wa miezi sita na khalafu hutazamwa nazi moja kama imefanza joya ndani kuchukuliwa zikapandwa hatta zikafanya zikatoa mche hungolewa zikienda zikapandwa mahala pake hatta zikakuwa.

Na khabari ya mwembe humwagwa kokwa zikatiwa jivu na kama hukutiwa jivu embe hubadilika ikawa namna nyingine. Na zikesha kutiwa jivu baada ya miezi minne huchepuka. Tena huota hukangoa kwa vizuri ukienda ukapanda mahali unavyotaka. Embe zote namna hii.

Kisa cha Binti Matlai Shems.

(Die Geschichte von Fräulein Matlai Schems.)

Aliondokea mtu mmoja mfalme akakaa katika mulki wake siku nyingi na yeye a na watoto sita wa mke na mtoto mmoja wa suria. Naye ndiye kitinda mimba. Bass. Akaondoka yeye na waana we wote sabaa. Akienda katika bustani wakabarizi; marra katika kikao chao walichokaa akatokea ndege mzuri sana a na bawa za zahabu a na miguu ya rangi ya lulu na si mrefu wala si mfupi si mnene wala si mwembamba. Akaja akatua karibu ya mti; akaondoka yule baba yao akawaambia waana we: tafadhalini wanangu anipendaye mimi sharti anipatie ndege yule. Wakaondoka waana we wa mke wakasema: tutakupatia baba. Akasema: vyema. Na yule mwana wa suria asiseme neno. Bass. Hatta khalafu wakaondoka wakaenda zao nyumbani. Wakafanza mashauri ya safari kulla mtoto akapewa farasi mmoja na watumwa mia. Yule kitinda mimba akamwambia baba yake: Na mimi baba ntasafiri pamoya na ndugu zangu nikatafute ndege huyu. Baba yake akamwambia: Wewe mwanangu kijana bado hutaweza kwenda katika barra. Mtoto

akajibu: hali yangu hali ya mwenzangu, nimepata ndio, sikupata bass. Baba yake akamfanzia safari naye akapewa farasi na watumwa mia na fedha, sababu ndiye mtoto anayependwa zaidi kuliko wenziwe. Bass. Wakaondoka wakaenda wote sabaa. Wakaenda mwendo wa siku tano katika barra hatta wakafika mahala karibu ya mwitu wakafanya mashauri wale ndugu zake sita ili kumwua yule ndugu yao.

Wakamwambia: tupe mali yako yote na farasi wako na watumwa wako na kama hutaki tutakuua. Akasema: Hapana haya ya kuniua, mkiniua mimi ntapoteza roho yangu mtapata mali, walakin afathali chukueni mali mniachie roho yangu. Bass. Wakamnyanganya mali yote wakamwacha yeye na nguo yake na kitabu chake, bass. Na wale watu sita walionyanganya wakasema: baba yetu a na wazimu ametwambia tukatafute nyama mwenyi bawa, tutamwona wapi nyama mwenyi bawa, na nyama mwenyi bawa anaruka yuu na sisi tunakwenda chini. Bassi baba huyu a na wazimu; afadhali sisi tufanze maskiani hapa tufanye mji, maana kulla mtu katika sisi tulio a na watumwa mia, na sisi wanatutosha kutufanya kazi hapa tulipo, na jumla ya watumwa wetu tulio nao sita mia na mia tulionyanganya yule maleuni jumla sabaa mia bassi, wanatutosha. Tufanze maskiani kabisa urefu wa umri wetu tutakaoishi katika dunya.

Akaondoka yule kiyana alipokwisha nyanganywa akenda zake msitu na nyika msitu na nyika msitu na nyika hatta akapata mwendo wa siku mbili kwa miguu akatokea mahali pana jangwa kubwa upeo wa macho yake, na katikati ya jangwa hilo pana mti mkubwa sana akienda yule kijana akakaa chini ya mti ule ili kupumzika. Marra akatupa macho akasikia katika mwitu kwa mbali kishindo akanyamaza marra akaona zimwi kubwa sana. Marra likaja pale alipo yule kijana akamwuliza yeye: mtoto wee unatoka wapi unakwenda wapi. Akamjibu akamwambia: sijui nitokako wala nendako. Akamwambia: umethulumu roho yako weye hunitoshi chakula changu hatta cha saa moja. Akamwambia: naam, sahihi. Bass. Akamwambia: utatwaa damu yako nifanye maji ya kusukutua, ni

twae na mafupa yako ni fanye mswaki wa meno yangu, ni twae na nyama yako nifungue kinywa, khalafu niingie mwituni ni tafute tembo wawili nile maana wewe hunitoshi kitu. Bass.

Yule kijana akamwambia: kama atakaokuamru Muungu nifanze, maana mimi si na amri, amri yote i na Mungu na mtume we. Maana mimi nimeondoka kwetu na ndugu zangu watu sita mimi wa sabaa na baba yetu ameona ndege akatamani kwetu ili kwenda sisi kumtafutia ndege yule aliomwona tukaondoka siye sote sabaa hatta tukafika katika mwitu karibu na hapa, wakanikamata wenzangu ili kutaka kuniua au kuninyanganya mali yangu. Bassi nikawaambia mimi: msininyanganye roho yangu afadhali twaeni haya mali mniachie roho yangu nikafie mbele. Bass wakaninyanganya yote. Nikaondoka mimi na roho yangu nikafika hapa peke yangu mimi na Mola wangu na roho yangu hatta ukaniona wewe hapa na leo vile atakavyokuamru Mungu ndivyo.

Bassi yule zimwi akamwambia: kana unataka wewe roho yako nifanyie chakula unipe nile. Yule kijana akamwambia: Mimi peke yangu si na chakula nitapata wapi chakula cha kukupa wewe katika mwitu kuu. Akamwambia: Nitakuua kana hutanipa. Akamwambia: Nipe muda wa saa mbili utapata chakula. Akamwambia: Nimekupa muda wa saa mbili. Bassi. Yule kijana akatwaa kitabu chake akasoma akaomba Muungu; marra akaona masufuria arbaini ya vyakula. Bass. Yule zimwi akasema: sasa nimefurahi kwa kupata chakula. Akaingia zimwi katika masufuria yote arbaini akayala yote, na kwa kulla sufuria uzito wake ratil miteen. Yule kijana akastaajabu sana alipomwona zimwi yule amekula masufuria arbaini. Alipokwisha kula zimwi akamwambia: sasa tuulizane hali maana nimeshiba sasa na akili yangu imetulia katika kichwa. Akamwuliza yule kijana: nipe khabari yako unayotafuta. Akamwambia: natafuta ndege mwenyi maumbo ya thahabu na lulu Akamwambia: Namjua anakokaa, walakin mbali sana. Aka mwambia: haithuru twende. Wakaondoka yeye na zimwi w kaenda mwendo wa siku tatu hatta wakafika mahali mbali i

majumba akamwonyesha akamwambia: nenda nyumba zilė unazoziona, utakwenda ona watu wengi wamelala; utaona na ndege huyo unayemtaka na wengine ndani ya tundu moja, walakin ukisikia watu wanazungumza wamelala ukisikia wamenyamaza wa macho hawakulala. Bass. Akaondoka yule kijana akaenda hatta akafika kule. Akasikia vishindo vya mazimwi akasikia na makelele ya mazimwi akaenda peke yake hatta akaona lile tundu lenyi ndege. Akaenda akataka kukamata. Bass. Wakaondoka mazimwi wakampigia makelele wakamkamata wengine wakisema: tumle, wengine wakisema: tumpeleke kwa sultani. Bass. Akaja yule mkubwa wao akasema: tusimle, tumpeleke kwa sultani. Wakampeleka kwa sultani. Sultani akamwuliza: jambo gani liliokuleta huku. Akamwambia hapana illa ndege nataka. Akamwambia: na kama unataka ndege, nenda ukanitafutie upanga wa radi, ukinileteа ntakupa ndege, licha ya moja hatta wote ntakupa.

Bass, akaondoka yule kijana akasema: inshallah. Akarudi hatta pale njiani alipo rafiki yake zimwi. Yule zimwi akamwuliza: Ye mbona hukupata ndege? Akamwambia: sikupata; nimeambiwa nikatafute upanga wa radi; nikiupata nikileta ntapata ndege, licha ya moja hatta wote.

Yule zimwi akamwambia: vyema rafiki yangu walakin nipe chakula kwanza nile tupate kufanya safari ya kwenda kutafuta upanga wa radi. Bass, akasoma yule kijana zikaja sufuria arbaini kana kwanza akala yule zimwi na yule kijana kidogo wakaondoka wakaenda mwendo wa siku mbili. Wakaona majumba akamwambia zimwi majumba yale ndio yenyi upanga wa radi. Akamwambia: enenda nyumba zile unazoziona. Akaondoka akaenda akaona kama alivyoona kunako ndege panga tatu zimetundikwa akanyoosha mkono kutaka kukamata panga. Wakaja watu wakamkamata wengine wakasema: tumle, wengine wakasema: tumpeleke kwa sultani. Bass. Akaja mkubwa wao akasema afadhali tumpeleke kwa sultani. Wakamchukua wakampeleka. Sultani akamwuliza alipofika: unatafuta nini huku? Mimi natafuta upanga wa radi. Akamwambia: kana unataka nenda ukanitafutie binti Matlai Shems; ukienda ukinileteа binti

Matlai Shemsi nitakupa panga zote tatu. Akamwambia: inshallah. Akaondoka akaenda hatta akafika pale alipo rafiki yake yule zimwi.

Akamwuliza: Je mbona hukuleta upanga wa radi? Akamwambia: nimeambiwa nenda nikamlete binti Matlai Shemsi, nikesha mleta mbinti Matlai Shemsi nitapewa panga zote tatu. Bass, wakaondoka wakafanya mashauri ya kwenda kumtafuta binti Matlai Shemsi aliko. Wakienda hatta wakafika mahali karibu ya pwani wakangoa miti mikubwa mikubwa. Wakafanza markebu nzuri sana wakaitosa katika bahari wakaingia wakasafiri wakenda hatta wakafika katika mji anaokaa binti Matlai Shems na mji ule mfalme wake baba ya binti Matlai Schems, ndio mfalme wa inchi ile. Bass, yule kijana alipokwisha fika akamwambia rafiki yake: sasa tumekwisha fika, sasa tufanzeje hatta tumpate binti Matlai Shems? Yule zimwi akamwambia: utampata, wala usifanye haraka, walakini nataka hila kubwa sana ya kufanya hatta mtu akampata. Akamwambia: hila gani? Akamwambia: jigeuze wewe mganga kwa kuwa unajua dawa na hirizi, mtu akifanza dawa hii hafi. Yule kijana akamwambia: vyema. Akamwambia: kesho shuka wende katika mji wende hatta kwa sultani kamwambie kama mimi najua dawa hii bassi; ukiitwa kufanza dawa fanza; walakin akikwambia: fanya dawa ya binti wangu, mwambie: dawa ya mtoto katika inchi haifai illa katika bahari, na akija huku binti wake tutamchukua. Bassi, yule kijana akaitikia maneno ya rafiki yake akamwambia: kesho nitakwenda nikijaaliwa. Bass. Akalala hatta assubui kulipokucha akaondoka yule kijana akienda hatta akafika kwa sultani akataka rukhsa ya kuonana na sultani akapata rukhsa akapanda hatta juu kwa sultani. Akamwambia sultani hatta alipokwisha kumwamkia akamwambia: mimi nimekuja kwako seyidina na mimi najua dawa kazawakaza, mtu akifanza hafi.

Bass, sultani akamjibu akamwambia: mimi nataka unifanyie mimi na waanangu na wake wangu na masuria zangu na jamaa zangu. Bassi, yule kijana akamjibu akamwambia: heiwalla seidina, nitafanza. Akaenda marikebuni yule kijana

akachukua dawa zake akaja nazo hatta kwa sultani akafanza dawa ya watu wote illa yule binti asimfanzie dawa akasema: dawa ya binti haifai kufanyia katika mji wala katika inchi; dawa ya binti lazim kufanyiwa katika bahari. Bass yule baba yake yule binti akasema: vema, kesho atakuja. Yule kijana akasema: inshallah, walakin asije na watu wengi sababu dawa inataka sirri. Baba yake akasema: vyema. Yule kijana akaondoka akaenda zake. Akamwambia rafiki yake zimwi akamwambia: yule binti Matlai Shemsi kesho atakuja. Na yule rafiki yake akamwambia: inshallah, na mimi ni tayari kwa safari yetu.

Bassi na huku nyuma kwa sultani akamwambia binti wake: kesho fanza safari wende markebuni kwa yule mganga wala usende na watu wengi nenda wewe na mjakazi mmoja, bass. Yule binti Matlai Shemsi akasema: heiwallah baba. Akalala hatta assubuhi akafanya safari na mjakazi wake wakenda hatta markebuni. Walipofika markebuni akaondoka yule kijana akamkaribisha yule binti Matlai Shems chumba cha chini akimwonyesha madawa ya uwongouwongo. Kumbe nyuma huku yule zimwi amekwisha fungua merikebu inakwenda. Na yule bibi hana khabari ndani hatta walipoondoka kule ndani marikebu imekwenda mwendo wa kutwa. Bibi akasema: wapi huku? Yule kijana akamwambia: huku kwetu na wewe inshallah taala usitie khofu iwayo yote, inshallah utaregea kwenu kama ulivyokuwa kwanza. Bass, na huku nyuma walikotoka baba yake alipoona ile marikebu haiko bandarini akafanya wazimu akili yake yote ikampotea kwa ginsi alivyokuwa akimpenda binti wake akaziambia marikebu zake zote ziende katika dunya yote kumtafuta binti yake. Marikebu zikaondoka zikaenda zikamtafuta hatta zikachoka zikarudi hazikumwona. Baba yake akalia akashukuru Muungu akanyamaza. Bass.

Na yule kijana aliyemchukua binti Matlai Shems akenda naye hatta akafika karibu na mahali alipoambiwa: lete upanga wa radi. Akamwita rafiki yake zimwi akamwambia: Yee rafiki yangu nipe mashauri yako, binti Matlai Shemsi tu naye na upanga tunataka tufanze shauri gani sasa hatta tupate upanga.

Yule rafiki yake akamwambia: Shauri hapana illa mwombe kijakazi chake binti Matlai Shemsi; ukipeleka useme: huyu ndiye binti Matlai Shems. Bass, akamwambia: vyema, akamwambia binti Matlai Shems: tafadhal nipe kijakazi chako nikambadili kwa upanga wa radi. Bass. Binti Matlai Shemsi akamwambia: fadhili yako kijakazi changu. licha ya kijakazi hatta mimi kijakazi kwako. Yule kijana akasema: ahsanta, ya binti Matlai Shemsi. Akampokea yule kijakazi akampamba nguo nzuri nzuri akamvika na fedha na zahabu akawa kijakazi kizuri sana. Bassi rafiki akamwambia: sasa mpeleke ukaseme: huyu binti Matlai Shems. Bass, akasema: inshallah. Akamchukua yule kijakazi akenda naye hatta akafika kwa yule sultani wa mji ule. Akaingia katika mji akenda hatta kwa sultani akamwambia: huyu binti Matlai Shemsi uliomtaka, nipe upanga. Yule sultani akafurahi sana akamwambia: chukua panga zote tatu za radi licha ya moja. Akamwambia: la, mimi sitaki illa upanga moja bassi. Akamwambia: khiari na shauri kichwani mwako, akanyanyua mkono akachukua upanga moja. Akaja nao hatta kwa rafiki yake akamwambia: huu upanga wa radi nimekuja nao. Akamwambia: haya twende zetu sasa. Wakaondoka wakaenda zao hatta wakakaribia karibu na panapo ndege. Rafiki yake akamwambia: sasa tumekwisha fika panapo ndege, tufanye shauri gani sasa hatta tupate ndege. Rafiki yake akamwambia: shauri kubwa na ndogo naijua mimi. Bassi, wakenda hatta wakakaribia wakakaa kitako katika khema yao wakatoa vyakula vyao wakala. Walipokwisha kula yule zimwi akamwambia rafiki yake: kata mti tufanye upanga. Rafiki yake akakata mti akampa yule zimwi akauchonga akaufanza kana upanga wa radi akaupaka dawa ukageuka chuma akamwambia: uchukue huu upanga wende nao hatta kunako ndege upeleke umwambie sultani, kwa kuwa upanga wa radi unaotaka huu nimekuletea; nipe huyu ndege nichukue. Bass, yule kijana akaupokea upanga akauchukua akenda nao hatta akafika kule kwa sultani mwenyi ndege. Alipofika kule akenda hatta kwa sultani akampa ule upanga akamwambia: huu ndio upanga wa radi unaoutaka. Yule sultani

akafurahi sana akamwambia: chukua ndege wote watatu licha ya mmoja. Yule kijana akasema: la, uthuru wangu mimi ndege mmoja bass. Akamwambia: vile upendavyo. Bass, yule kijana akachukua ndege moja na tundu lake. Akarudi akaja naye hatta kwa rafiki yake zimwi. Wakaondoka wakenda zao hatta karibu ya pale walipo ndugu zake, yule zimwi akamwambia: Yee rafiki yangu nikupeleke kwa baba yako au ntakwenda kwa ndugu zako hapa walipokaa. Yule kijana akasema: la, rafiki yangu, nitakwenda kwa ndugu zangu, nipate kwenda nao pamoja kwa baba.

Yule rafiki yake akamwambia: haya nenda, walakin nitakupa akiba nyoya langu ufutike ukesha wende zako na likikupata neno liwalo lote la dunya twaa nyoya langu litie katika moto, marra ukesha litia katika moto utaniona mimi niko mbele yako nimekutokea.

Bass, yule kijana akalipokea lile nyoya akaichukua akalifutika wakaagana na yule rafiki yake akenda zake. Akaondoka yule kijana yeye na binti Matlai Shemsi na yule ndege na ule upanga wakenda hatta wakafika kwa ndugu zake. Akawakuta wote sita wamefanya mashamba wanalima; akaingia yule kijana akawaamkia akawaambia khabari yote na wale ndugu zake wakamwuliza: ndugu yetu, mwanamke gani huyu, nani jina lake mwanamke huyu? Yule kijana asiseme akasema: mwanamke huyu nimemwokota njiani na jina lake silijui na huu upanga nimemkuta na huyu mwanamke na huyu ndege ndiye anayemtaka baba. Bassi na sasa twendeni kwa baba kwa shauri moja tutasema kama ndege huyu tumempata pamoja, bass. Wakalala hatta usiku wakamkamata ndugu yake wakamkaba roho hatta akazimia wakamchukua wakenda wakamtupa katika mto na yule binti Matlai Shemsi alipoona vile ikawa hali wala hanywi wala hasemi. Wakaondoka wale ndugu zake wakaenda zao wakamchukua binti Matlai Shems na upanga ule na yule ndege hatta wakafika kwa baba yao. Baba yao alipoona watoto wake akafurahi sana akapokea na yule ndege akazidi kufurahi. Akawauliza watoto wake: ndugu yenu yuko wapi kitinda mimba? Wale wakasema: hatujui, amekwenda na njia

zake. Baba yao akasema: na apotelee mbali sababu hakushika mashauri naliomtuma. Bass na mama yake yule kijana akatolewa katika nyumba akafukuzwa akapewa nyumba nje ndogo akakaa.

Na wale ndugu zake yule kijana wakaulizwa na baba yao: mwanamke huyu jina lake nani? Wakasema: hatumjui, tumemwokota njiani na upanga wake. Baba yao akauliza: kwa nini hali mwanamke huyu wala hasemi mwanamke huyu wala hanywi mwanamke huyu. Ginsi gani? Wale vijana wakasema: labda mwanamke huyu anawaza kwao, alikopotea, bassi. Yule mkubwa akasema: nitamwoa mimi mwanamke huyu. Wakafanya mashauri ya kuoa. Bass.

Na yule kijana kule mtoni alikotupwa akalala hatta assubui ukampiga upepo wa alfajiri akapata fahamu ya dunya akafufuka; akaondoka akakoleza moto akatoa unyoya wa rafiki yake akautia motoni. Marra akamwona rafiki yake mbele yake. Akamwambia: Yee rafiki yangu, u na nini? Akamwambia: kuja kwangu jana hapa kwa ndugu zangu yamenipata mambo ginsi kazawakaza; akamweleza khabari yaliompata yote. Akamwambia: haithuru, twende zetu nikupeleke hatta kwa baba yako. Akamchukua akampa nguo nzuri yule kijana akavaa akenda naye kwake akampandisha juu ya frasi akamchukua hatta akampeleka kwa baba yake barazani. Na watu wamejaa baraza tele: mawaziri na makathi na wale ndugu zake wamekaa na baba yake amekaa. Akaanguka mbele ya baba yake akasema khabari yake yote iliompata kwa ndugu zake tokea mwanzo hatta mwisho akasema na mwanamke huyu jina lake binti Matlai Shemsi akasema na khabari aliompatia mwanamke yote na khabari aliompatia ndege yote na khabari aliompatia upanga wa radi yote na khabari iliompata kwa ndugu zake yote. Na yule zimwi amekaa palepale.

Na ndugu zake wapo palepale. Akaja na binti Matlai Shems akajinadi akasema watu wote wakastaajabu kwa kusikia mwanamke yule kusema. Marra baba yake aliamrisha watu akawaambia: wachukueni watoto hawa sita mkawaue wote. Wakachukuliwa wakenda wakatiwa katika mafumba wakenda

wakatoswa katika bahari. Bass, na yule kijana akapata heshima kubwa kwa babaye na yule mama yake akapata heshima kubwa sana zayidi kuliko kwanza. Yule kijana akafanya arusi akamwoa yule binti Matlai Shemsi wakakaa wakafanya arusi siku kazawakaza. Wakasafiri wakafika hatta kwa baba yake binti Matlai Shems. Alipoona yule mzee mwana we amerudi akafurahi sana akamwambia: ahsanta, umenichukulia mwanangu khalafu umeniletea. Akamwoza marra ya pili akafanza arusi kubwa zayidi kuliko aliofanza kwanza. Wakakaa wakila wali wao na mikate hatta wakachoka. Tamat.

Nimeipokea hadithi hii mimi Amur kwa binti Hasan bin Husein.

Nini bora, mbingu au ardhi?

(Was steht höher, der Himmel oder die Erde?)

Kitu cha kwanza katika ardhi bora kushinda vitu vyote ilkaaba, maana nyumba ya Mngu; aidha ya pili meskiti maana nyumba za Mngu; aidha ya tatu makaburi ya mitume ya Mngu mtukufu. Maana makaburi yao katika tumbo la ardhi.

Aidha kama walivyonena watu maulamau, fahamu kwamba siku moja katika siku ilijidai mbingu kwamba bora kuliko ardhi, na ardhi ikajidai kwamba bora kuliko mbingu. Zikashitakiana kwa Mola wetu. Mbingu ikanena kwamba mimi bora kuliko ardhi, na ardhi ikanena kwamba mimi bora kuliko mbingu. Mola wetu akanena: kwa nini mbingu bora kuliko ardhi. Mbingu ikanena: kwa maana. Mngu akauliza: kwa maana gani? Mbingu akanena: kwamba arshi wa lkursi juu yangu na malaika wote juu yangu, mimi bora kuliko ardhi.

Mngu akaiuliza ardhi: na wewe kwani ukawa bora kuliko mbingu? Ardhi ikajibu ikanena: kwamba ilkaaba na meskiti na mitume yote katika tumbo langu. Mngu aliposikia maneno ya ardhi akaiambia: rudi mahali pako. Ardhi ikarudi. Mngu asinene kwamba bora ardhi wala mbingu. Na hivyo ndivyo tulivyosikia kwa watu maulamau. WAllahu aalam.

Sababu ya maji yakiyaa yakipua.

(Ursache von Ebbe und Fluth.)

Aidha baharini maji marra imejaa na marra imekupwa. Fahamu kwamba watu maulamau watu wajuao wamenena kwamba ardhi chini ya bahari. Aidha wamenena watu maulamau kwamba Mngu kaumba bahari na chini ya bahari hawa yaani upepo na chini ya upepo kudura ya Mngu mtukufu. Aidha mwanzo wa ardhi samaki jina lake Chewa na juu ya mgongo wa Chewa jiwe kubwa sana. Chewa katika bahari na jiwe juu ya Chewa. Na juu ya jiwe ngombe mkubwa sana. Wamenena watu maulamau kwamba ngombe huyu a na pembe sabaini elfu na miguu arbain elfu. Miguu yake juu la jiwe na juu ya pembe zake ardhi, yaani kaziwia ardhi kwa pembe zake. Na pua yake katika bahari na killa siku hupumzika marra moja, watu wamenena kwamba bahari ikijaa ngombe hupumzika yaani hushusha pumuzi; bahari ikipwa ngombe hupandisha pumzi. WAllahu aalam.

Hadithi ya mapomboo.

(Geschichte von den Delphinen.)

Aidha wamenena watu wafanya hadithi kwamba asili ya samaki anayekwitwa pomboo. Na kwanza ilikuwa hapana, aidha alipokuwa nabii Suleimana hakimu alikuwa maliki yaani mfalme kubwa, akihukumu killa kitu kilioko katika iddunya, watu majinni nyama ndege upepo. Na ufalme wake katika pete yake.

Hatta siku moja nabii Suleimana akaghafulika akaja jinni moja akaiba pete yake akaichukua hatta siku moja ikamanguka katika bahari. Ndio sababu kuwako mapomboo katika bahari. Maana alipoona Mngu kwamba pete ya nabii Suleimani imeibiwa na jinni, na jinni imemanguka katika bahari, marra akawatuma mapomboo kutafuta pete ya nabii Suleimana. Ndio mapomboo wanazama wakiinuka maana watafuta pete. WAllahu aalam.

Aidha pete imeonekana walakin wao hatta sasa wangalia wakitafuta, aidha hawakomi kutafuta hatta siku ya kiyama. Hiyo ndio khabari ya mapomboo.

Hadithi ya chewa.

(Geschichte vom Chewa-Fisch.)

Aidha khabari za samaki anayekuitwa chewa. Chewa watu hunena sultani samaki sana maana kwa sababu kaziwia ardhi. Naye a na kinywa kikubwa sana kushinda samaki wote katika bahari. Aidha wamenena watu wafanya hadithi kwamba chewa asingekuwa na kinywa kikubwa illa kwa sababu uchungu wa mke we. Wamenena watu wafanya hadithi kwamba chewa alikuwa na wazee wake na ndugu zake na ahali zake na mke we. Akasafiri chewa akenda mbali peke yake hatta siku katika siku akamjia mtu anatoka kwao wazee wake akampasha khabari ya kwamba baba yake kafa. Chewa akanena: kazi ya Mngu. Asifanye msiba wala asione uchungu katika moyo wake. Hatta siku ya pili akaja mtu mwingine mjumbe akamwambia, kwamba mama yako kafa. Chewa akanena: bassi. Hatta marra ya tatu akaletewa khabari kwamba nduguye kafa. Akanena: bassi. Hatta ahali zake wote wakafa na killa akiletewa khabari chewa hunena: bassi, hafanyi msiba wala uchungu.

Hatta siku moja katika siku akamjia mtu ambaye atokaye kwao akamwambia: u nao khabari? Chewa akanena: la, si na khabari. Mtu yule mjumbe akanena: mke o kafa. Aliposikia chewa kwamba mke we kafa akastaajabu sana akaona uchungu sana katika moyo wake akanena: a a ah, kinywa chake kikafunuka sana kwa kustaajabu. Ndio sababu ya kuwa chewa kinywa kikubwa.

Binti la ngombe mia.

(Eine Frau für hundert Rinder.)

Aliondokea mtu mmoja na mke we wakakaa siku kaza wa kaza katika nchi ya Pate nao wakazaa mtoto mwanamume

mmoja na ras mali yao walikuwa na ngombe mia; hawakuwa na zayidi hatta ya ndama katika ngombe wao walio nao.

Bassi hatta khatima yule mtoto wao akawa kijana mkubwa; hatta akapata kijana wa miaka kumi na tano, yule babaye akafa. Na muda wa miaka miwili mitatu na mamaye akafa, bassi. Akiwa yule kijana kuwarithi wazee wake wote wawili akarithi na wale ngombe mia aliyoacha akakaa akafanya matanga ya wazee wake. Hatta yalipokwisha matanga ya wazee wake akatamani kuposa mke ili aoe.

Akawaambia majirani zake, kwa kuwa mimi nataka kuoa mke maana wazee wangu wamekufa na sasa mimi niko peke yangu, bassi. Siwezi kukaa peke yangu illa kuoa mke, bassi. Wale majirani zake wakamwambia: haya, oa, maana kweli sasa uko peke yako, nasi twakuonelea afdhali wendapo ukaoa mke. Akasema: naam, bassi.

Akasema: nataka mtu a ende akanipose mke. Wale wakasema: inshallah. Bassi akaondoka yule jirani yake mmoja akenda akamutafutia mke wa kumwoza hatta akamupata akaja akamwambia: mke unayetaka nimempata walakin si katika mji huu wetu. Akamwuliza: wapi? Akamwambia: katika mji mwingine mbali sana, athani mwendo wa saa nane tokea hapa hatta huku.

Akamwuliza: binti wa nani mwana mke huyu? Akamwambia: binti Abdallah na baba yake ana mali sana, mwanamke huyu a na ngombe elfu sita naye wala hana mtoto illa huyu binti wake mmoja, bassi wa salamu.

Bassi yule kijana aliposikia vile akafanya hamu sana yakumtaka mke yule akamwambia yule jirani yake: nenda kesho upeleke maneno yangu, kwa kuwa mimi nimekubali.

Bassi akasema yule jirani yake: inshallah, kesho nikijaaliwa nitakwenda. Hatta kulipokucha assubuhi akaondoka yule mjumbe akaenda hatta akafika kwa yule mzee Abdallah akamuaridhia maneno yake yule aliokuendea yoyote. Bassi.

Hatta khatima yule mzee akajibu akasema: maneno yako nimeyasikia walakini mimi nataka kwa kulla mtu atakaye binti wangu kuoa lazim namtaka mahari yake atoe ngombe mia,

endapo na kama atatoa mahari yake ngombe mia nitamwoza, bassi. Yule kijumbe akasema: inshallah, ntakwenda kujibu. Akamwambia: haya. Bassi akaondoka akarudi akamjibu yule kijana maneno aliyopata kule yote. Na yule kijana akasema: nimesikia maneno yako, walakin anataka ngombe mia mahari yake na mimi sina kitu illa ngombe mia; nikiisha kumpa ngombe mia wote, akija kwangu mke wangu atakula nini? na mimi sina ras mali illa ngombe mia niliorithi kwa baba yangu.

Bassi hatta khatima yule jirani yake akamwambia: na kama hutaki nambie nende nikajibu ao unataka nambie nikajibu, bassi. Yule kijana akainama akawaza, hatta alipoinuka akasema: haithuru, nenda ukamwambie: nimekubali, nitatoa ngombe mia nitampa. Bassi akaondoka yule kijumbe akaenda hatta akafika kwą yule mzee akamwambia: yule kijana amekubali kutoa ngombe mia, bassi. Na yule mzee akasema: na mimi nimeridhi na kama atatwaa binti. Wakafanya maneno akatumwa mtu akaenda akamwita yule kijana. Akaja akakaribishwa akakaa hatta khatima wakafanya mashauri ya kuoa. Akaoa akatoa ngombe mia akafanya arusi. Bassi.

Hatta khatima akamuchukua mke we akaenda zake kwake, bassi. Wakakaa siku kumi moja, vile vyakiba vyake vikisha ikawa yule kijana hana kitu cha kumlisha mkewe, bassi. Akamwambia mkewe akasema: Mke wangu, mimi sina kitu sasa cha kukulisha; kwanza nalikuwa na ngombe wangu nikikama nikipata chakula nikila na leo ngombe wangu wote nimekuolea wewe wote, na sasa sina kitu, bassi; mke wangu nitakwenda kwa majirani zangu wenyi ngombe nikakamishe nipate kiwacho chote tupate kula. Bassi yule mke wake akamwambia: haya mume wangu. Bassi, akaondoka yule kijana, ikawa kazi yake, huenda akikamiza ngombe wa watu ili kupata kiwacho chote apate kula na mke we ikawa kazi yake kwa kulla siku.

Hatta siku moja akaondoka yule mwanamke akasimama mlangoni pake marra akapita kijana mzuri sana pale mlangoni. Marra yule kijana alipoona yule mwanamke amesimama pale mlangoni akamtamani ili kumtongoza azini naye akapeleka watu makwadi zake kwa yule mwanamke. Bassi.

Yule mwanamke akasema: inshallah, maneno yako uliyotumwa nimeyasikia walakini ngoja, na yangu nitakwambia khalafu, walakini si sasa. Bassi akaondoka yule kawadi akenda zake, basi. Hatta walipopata muda wa miezi mitatu akaondoka yule baba yake mke kule aliko akasema: leo nitamani kwenda kumtazama binti wangu kwa mume wake. Bassi. Akaondoka akafanya safari akenda zake hatta akafika kwa yule mkwe wake akabisha: hodi, hodi. Akaondoka yule binti wake akamwitikia: hodi, nani wewe? Akajibu yule mzee akasema: Mimi hapa fulani. Akaondoka yule binti wake akamwambia: karibu. Akaingia ndani akamwamkia binti wake akamkaribisha barazani akakaa kitako yule mzee. Akaondoka yule binti wake, akamwuliza hali yake babaye akamwambia: jema baba, bassi.

Hatta khatima akaondoka yule kijana mwanamke pale alipo naye babaye akaingia ndani akawaza akalia kwa sababu ndani ya nyumba yake hamukuwa na kitu hatta kidogo cha kumpikia babaye. Bassi, akatoka kwa mlango wapili wa uani akatupa macho yake nyuma ya ua akamwona yule kijana mwanamume anayemtongoza akamwita. Akaenda yule binti kwa yule kijana. Bassi, alipokwenda akamwambia: gissi gani wewe shekhi? Nimetuma mtu kuja kwako ili uje kwangu utajamal na mimi na wewe ukamujibu kwa kuwa utakuja na wewe hukuja, bassi, ndio khabari gani ya kuzungushana; na mimi tokea nilipokuona siku uliosimama mlangoni hatta sasa nikilala sipati usingizi, ni kulla siku kukuota wewe ndani ya usingizi wangu.

Bassi yule binti akamjibu akamwambia: Sasa inshallah sikuzungushi hatta kama unanitaka sasa hivi nitakuja kwako walakini nipatie nyama nimpikie mgeni wangu ale akisha kula nitakuja, bassi. Yule kijana akamwuliza akamwambia: mgeni gani ulio naye? Yule binti akamujibu akamwambia: baba yangu ndiye mgeni nilio naye. Akamwambia: inshallah, ningoje hapahapa sasa hivi nitakuletea nyama, bassi.

Akaondoka akaenda zake na yule binti akasimama palepale, hatta marra akaja yule kijana na paja la ngombe aka-

mwambia: hii nyama, walakin sasa usinizungushe. Akamwambia: inshallah, sikuzungushi. Bassi, hatta khatima akanyosha mkono akampa ile nyama na yule binti akaipokea akaingia nayo ndani. Na yule mweke nyama ikawa kukaa nje akizungukazunguka anangoja wahadi wake aliomwambia yule binti, bassi.

Na yule binti alipokwisha kuingia ndani akaitwaa ile nyama akaikatakata akaitia ndani ya chungu. Marra kuitia kwake mle chunguni akatokea mume we akamkuta mkwe wake yuko barazani amekaa. Alipomwona mkwe wake barazani, marra yule kijana damu ilimkauka, hakuwa na neno la kusema wala na shauri ya kufanya, bassi. Akakaribia hatta akafika pale alipokaa mkwe wake akamwamkia akamwuliza hali. Alipokwisha akaingia ndani kwa mke we akamukuta yule mke we anapika nyama akamwuliza: mke wangu unapika nini? Akamwambia: napika nyama. Akamwambia: umeipata wapi nyama hii? Akamwambia: nimeipata kwa jirani, wamenipa. Aliposikia vile mume we akanyamaza na huku akisikitika kwa sababu hana kitu. Akamwambia mke we: mke wangu tutafanya shauri gani sasa na sisi tu na mgeni hapa?

Mke wake akamjibu akamwambia: sijui la kufanya. Mume akasema: mimi nitatoka nienende kwa matajiri zangu ninakukama ngombe nikawambie, na kama mimi ni na mgeni kwangu; nataka tafadhali ninyi nipatieni kiwacho chote nikampikie mgeni wangu, bassi. Akaondoka akenda hatta akafika kwa matajiri zake akawaaridhia khabari yake yote aliyo nayo, bassi.

Wale matajiri zake wasikasiri wakampa nyama kidogo na maziwa kidogo akapokea akachukua, bassi.

Na huku nyuma yule binti akaipika ile nyama aliyopewa na yule mtongozi, hatta akisha, bassi. Marra akatokea mume wake na nyama akanyanua mikono yule binti akampokea mume wake nyama akaitua chini, bassi. Akaondoka yule mume wake akanawa mikono yake akatokea barazani marra. Na huku ndani yule mwanamke akaipakua ile nyama akaitia ndani la chanu wanacholia chakula, bassi.

Na yule anayetongoza amekaa akizungukazunguka akaona

wakati umepita alioagana naye yule mwanamke akasema ndani ya roho yake, afdhali nende nipite pale mlangoni nitazame, labuda nitamwona yule binti, bassi. Akaondoka akaenda akapita akamkuta yule mume wake yule binti amekaa na yule mkwe wake wanazumgumza, bassi. Marra alipoona vile yule fasiki akapiga salamu akaondoka yule mume wake yule binti akaitikia salamu akamukaribisha yule fasiki akaja akakaa, bassi.

Akajizumgumza na yule kijana mume wa yule binti haijui khabari ile kama yule ana maaribu yake pale ayatakayo, bassi. Ikawa kujizumgumza pale pamoja yule baba wa binti na yule mume wa binti na yule nguruwe anayetaka kufisidi nyumba ya yule kijana na jumla yao wakawa watu watatu waliokaa pale barazani, bassi.

Na huku ndani yule binti alipokwisha kuitia ile nyama ndani ya chanu akaitoa barazani. Akaondoka mume wake akaipokea, akasema yule binti: kuleni nyie wapumbafu watatu. Akaondoka yule baba yake akasema: nini upumbafu wangu mimi. Yule binti wake akamjibu akamwambia: tafadhali baba, kula kwanza, ukiisha kula nitakwambia upumbafu wako. Yule baba yake akasema: la, mimi sili illa unambie upumbafu wangu kwanza, ndipo nile. Akaondoka yule binti akamwambia: baba yangu umeuza kitu kilicho ghali kwa kitu cha rakhisi. Baba yake akamwambia: nini nilichokiuza rakhisi? Akamwambia: mimi baba, umeniuza rakhisi. Akamwambia: kwa nini? Akamwambia: baba wewe huna mtoto mwanamke wala mwanamume illa mimi binti wako mmoja, bassi; na wewe ukenda ukaniuza mimi kwa ngombe mia, na wewe baba u na ngombe elfu sita; ukaona ngombe mia afdhali kuliko mimi; ndipo nikakuambia umeuza kitu kilicho ghali kwa kitu kilicho rakhisi, bassi.

Yule baba yake akasema: kweli, binti wangu, mimi mpumbafu bassi.

Akaondoka na yule mumewe akasema: tafadhal nambie upumbafu wangu. Na yule binti akamwambia: wewe upumbafu wako zayidi. Akamwambia: kama upi? Akamwambia: wewe umerithi ngombe mia kwa wazee wako wala hukurithi

zayidi hatta ya ndama, na wewe ukawachukua wote ukaja ukaniolea mimi ngombe wako mia wote, na waanawake wako tele katika mji wenu wa mahari yao ngombe kumi, ngombe asherini, na wewe usiwaonee, ukaja ukanioa mimi kwa ngombe wako wote; na sasa huna hatta chakula cha kulisha mimi wala chakula wewe, umekuwa sasa mtumishi wa watu wanakwenda ukikamiza ngombe wa watu ukipata chakula; ungalikuwa na ngombe wako nussu ungaliolee mke na nussu ungalikula, bassi; huu ndio upumbafu wako wewe mume wangu.

Na yule hasharati akamwuliza: na mimi upumbafu wangu nini? nambie! Akaondoka yule binti akamwambia: wewe upumbafu wako mkubwa zayidi kuliko wenzio. Akamwambia: kama upi? Akamjibu akasema: kitu kilichonunuliwa kwa ngombe mia unakitaka ukipate wewe kwa paja la ngombe, bassi; wewe si mpumbafu?

Likaondoka likakimbiambia, wa salaam.

Hatta khatima akakaa yule baba yake siku mbili; hatta siku ya tatu akaondoka akaaga akaenda zake kwake. Alipofika kwake akafunga ngombe mia aliyotoa kwa mkwe wake akawarudisha akamujia na wengine miateen, bassi. Ikawa kukaa raha yule binti na mume wake siku kazawakaza. Wa salaam.

Na hadithi hii nimeipokea kwa Omar bin Himidi bin Muhammed Ruwehi katika Nyanjale wakati wa saa ya tatu ya usiku barazani pake. Tamat. Na kulla atakayesikia atatamani kusikiliza. Na jina lake hadithi hii: Binti la ngombe mia.

Mutanebbi.

(Geschichten von Mutanebbi.)

I.

Alikuwa na chongo. Siku moja aliondoka ili kwenda kuposa mtu mke alipofika njiani akiona kijana mzuri mwaname akamwambia: wewe kijana unakwenda wapi? Akamjibu akamwambia: ninakwenda kumposa binti Zubeida. Akamwambia: oh, natoka kwake sasa nimemkuta anambusu mwaname. Yule

kijana akaghairi akarudi. Akenda yeye akamposa. Akakubaliwa akamwoa.

Bassi yule kijana akapata khabari kana binti Zubeida amemwoa yule mzee Mutanebbi akaenda yule kijana hatta kwa Mutanebbi akamwambia: umenambia yule mwanamke hafai kuolewa umemkuta na mwanamume unambusu na leo mbona umemwoa weye. Akamwambia: mimi ni na maana nikamwoa; na wewe nilipokwambia kana nimemwona na mwaname anambusu hukuniuliza: mwanamume gani? Akamwambia: mwanamume gani uliomwona naye akimbusu? Akamwambia: baba yake.

II.

Safari moja aliondoka Mutanebbi kwenda kuposa mke akienda hatta akafika akawakuta wachumba wengi wamekaa barazani na yeye akaenda akakaa; na yeye mzee naye a na chongo na wale wachumba wengine vijana naye anamtaka mwanamke yule. Akafanya mashauri katika roho yake bassi; hatta khalafu akaja mjumbe wa yule mwanamke akamwambia wale wachumba wakae mlangoni wote apate kusema nao yule binti. Bassi wakakaa wale wote. Mutanebbi akamwuliza yule mchumba mwenziwe akamwambia: wewe ukioa mke wako humfanzaje? Yule kijana akasema: mimi huzuwia vyakula nikampa kidogo kidogo na funguo za nyumba yote nikazuia, nikimpimia kulla kitu nikiesha nikamzuia na mwanamke asipate nafasi hatta kidogo ya kuchungulia nje. Na maneno yale yule mwanamke akasikia. Bassi Mutanebbi akasema: Mimi la, mimi nikioa vitu vyote humwachia mwanamke na funguo zangu nikamwachia yeye na amri yote ya nyumba ikawa juu yake yeye. Bassi yule kijana akamwambia: mimi la. Na mwanamke tokea hapo roho yake ilitaka aolewe na yule kijana, walakin aliposikia maneno ya yule kijana akaghairi kuolewa na yule kijana akakubali huolewa na yule mzee. Na yule kijana akakosa. Na yale maneno aliosema yule mzee Mutanebbi yote amesema ili asikataliwe kwa uzee wake. Na yale aliosema yote hapana hatta moja aliofanza. Tamat.

Maneno matatu kwa reale elfu tatu.*)

(Drei Worte für 3000 Thaler.)

Aliondokea mtu mmoja a na akili sana, amesema ndani ya roho yake: afadhali mimi nisafiri katika mji huu, bassi. Akafanya safari akasafiri akenda hatta akafika Mekrani akashuka katika mji akenda kwa sultani akamwamkia, bassi. Hatta alipokwisha akaondoka akenda zake kutafuta nyumba kupanga akaipata akapanga, bassi.

Hatta khatima akaondoka akenda kwa tajiri akamwambia tajiri: tafadhali, nataka unipatie kiwanja mahala nijenge nifanye duka, bassi. Yule tajiri akamwambia: inshallah, nitakupatia, bassi. Akamutafutia kiwanja akamupatia akenda akajenga duka lake, bassi. Hatta lilipokwisha akaondoka akaweka kiti mlangoni akakaa, bassi. Kwa kulla mtu anayepita humwona yule mjini amekaa mlangoni.

Akawa kazi yake hiyo kwa kulla siku. Khatima akaja kijana mmoja akamwuliza akamwambia: wewe ulisema kama unajenga duka hapa, duka lenyewe liko wapi unalouza? Yule mgeni akamujibu akamwambia: naam, mimi nimejenga duka hapa, walakini siuzi vitu mimi nauza maneno ya maana. Yule kijana akamwambia: neno mmoja kiasi gani? Akamwambia: kwa kulla neno thamani yake reale elfu. Yule kijana akamwambia: nambie mimi neno moja, nitakupa reale elfu.

Akamwambia: na kama unataka wewe kununua neno moja, tuandikiane mkataba tukisha andikiana nitakwambia neno moja. Yule kijana akakubali akenda akaleta reale elfu akenda akaleta na mkataba, bassi. Yule mgeni akapokea akamwambia neno moja. Akasema: ukiona neno usinene neno, ukinena neno litakupata neno, tamat.

---

*) Ich bringe hier noch eine zweite Darstellung von der Geschichte, welche schon Seite 97 ff. gebracht ist. Der Inhalt ist wesentlich derselbe, aber die Erzählung vielfach anders gewendet. Beide Redactionen sind von einander unabhängig. Sie mögen als Beispiel dafür dienen, wie dieselbe Geschichte von verschiedenen Erzählern verschieden erzählt wird.

Akaondoka yule kijana akenda zake na neno lake moja hatta siku ya pili akarudi akamwambia: nambie na la pili nitakupa reale elfu nyingine. Akamwambia vilevile, tukatibiane. Yule kijana akakubali wanakatibiana mukataba wa pili. Akamwambia neno la pili. Akamwambia: Ukienda njiani katika safari jua likichwa njiani lala hatta kunakokwenda unakoona, wa salaam.

Akaondoka yule kijana akenda zake na maneno yake mawili, bassi. Hatta siku ya tatu akarudi akamwambia yule mgeni: mimi ras mali yangu elfu tatu niliorithi kwa baba yangu, elfu mbili nimenunua maneno mawili, nimebaki na elfu moja, na sasa nambie na la tatu umalize elfu ya tatu. Akamwambia: tukatibiane. Akakubali yule kijana wakakatibiana. Akamwambia neno la tatu akasema: ukienda njiani ukiona mtu anayekujua akikuambia: karibu kwangu, tafadhal nenda, wa salaam.

Akaondoka yule kijana akaenda zake na maneno yake matatu. Ikawa hana hatta chakula, fedha yake yote aliokuwa nayo amenunua maneno, bassi.

Akafanya kazi hatta akapata reale mia akasema: Fedha hiyo niliyoipata nitanunua bidhaa nende bara nikatafute biashara nifanye, labuda nitapata fayida, bassi. Akaondoka akenda kwa Wahindi akanunua bidhaa akafunga akapata na mwenzi we wa kufuatana. Wakaondoka wakafanya safari yao, wakaenda hatta wakafika njiani wakaona mji mdogo. Wakafanya mashauri ya kwenda katika mji ule kununua ngamia. Wakaingia katika mji wakanunua ngamia wawili kwa kulla mtu na wake. Wakapanda wakapakia na bidhaa zao wakenda zao mwendo wa kutwa, hatta wakapata karibu na mji, wanakotaka. Na jua likatua.

Bassi, yule kijana aliyenunua maneno akamwambia yule rafiki yake: tafadhali, rafiki yangu, tulale hapa na kesho tukijaaliwa tutaingia katika mji. Yule rafiki yake akamujibu akamwambia: la ya akhi, mji ule tunaoona, tulale hapa; la, mimi silali hapa na kama wewe utalala, haya, lala.

Bassi, yule akamwambia: mimi nitalala bassi. Akaondoka

yule rafiki yake akaenda zake, na yule aliyenunua maneno akamfunga ngamia wake akalala hatta assubui. Akaondoka akafungua ngamia wake akampanda akashika njia akaenda zake.

Hatta alipofika katikati ya njia akaona rafiki yake amekufa na ngamia wa rafiki yake amekufa. Akasema: alhamdu lillah rabb ilalamina, neno niliolinunua kwa reale elfu si ghali, sasa reale elfu nimeziona fayida reale elfu mbili.

Akaenda akaingia ndani ya mji ule akatafuta nyumba ya kupanga akaipata akapanga, bassi. Hatta khatima akaondoka akenda kwa sultani wa mji ule akamwamkia sultani. Na sultani akamwuliza anakotoka. Akamwambia khabari yote ya mji wao, bassi. Sultani alipomwona yule kijana akamtamani ili akae kwake kwa mshahara akamwambia: Tafadhali, si afdhali ukakaa hapa pangu kwa mshahara, bassi. Yule kijana akamwambia: naam, nitakaa nawe hapa, sayidina.

Akakaa na sultani akapata nyumba akapata na watu wa kutumika, ikawa sultani akampenda sana yule kijana akamwamini sana tokea mali hatta ndani ya nyumba yake sultani akiingia ginsi alivyoaminiwa na yule sultani, bassi.

Na yule sultani alikuwa na wake wawili na masuria talatha mia, bassi. Ikawa siku moja sultani akatamani kwenda kutembea kuwinda nyama. Akamwambia yule kijana: tafadhal tuende kesho tuwinde nyama uwaambie na watu wanaojua kusaka nyama tufuatane nao, bassi. Yule kijana akasema: heiwallah sultani.

Wakalala hatta assubuhi akaondoka yule kijana akawaambia wasakaji nyama wote akafanya shughuli ya safari yote akaenda akamwambia sultani: shughuli yote imekwisha. Sultani akaondoka akasema: nimesahau saa yangu ya mkono chumbani kwa mke wangu mdogo panapo shibaka, bassi, tafadhali ewe kijana rudi nyumbani uingie ndani kwa mke wangu mdogo utazame shibakani utaona saa yangu; tafadhali, ilete kwa upesi, bassi. Yule kijana akasema: heiwallah sayidina. Akaondoka akarudi nyuma hatta akafika nyumbani akaingia ndani kule alikoambiwa akamwona mke wa sultani na waziri wamelala juu ya kitanda cha sultani, bassi.

Yule kijana alipoona vile asiseme neno akachukua ile saa aliotumwa akarudi kule aliko sultani akampa, bassi.

Na huku nyuma yule waziri alipomwona yule kijana amemgundua akathani: yule kijana atamwambia sultani, bassi. Akasema katika moyo wake, haifai illa kumwua kijana yule, nitafanya hila hatta nimwue maana akisikia sultani khabari hii nitauawa mimi, bassi.

Na yule sultani akaenda akasaka nyama hatta alipokwisha akarudi mjini akakaa na yule waziri. Ikawa kufanya wasiwasi kwa kulla siku maana alithani yule kijana atasema. Na yule kijana asiseme neno liwalo lote maana anatezama fayida ya fedha yake alionunua maneno.

Bassi, yule waziri akawaambia watumwa wake: Nendeni shamba kwa *) sultani mkachimbe handaki kubwa sana, mkiisha chimba mkae kitako mungoje mtu atakayekuja awayo yote mkamateni mtie ndani ya handaki, Allah Allah, hatta ajapokuwa mama yangu mimi, na kama nimekuja auwali nikamateni mnitie. Wale watumwa wakasema: heiwallah bwana. Wakaondoka wakaenda shamba kwa sultani wakashimba handaki kubwa sana. Walipokwisha kuchimba wakakaa kitako, bassi. Na huku nyuma waziri akamwambia yule kijana: tafadhal nataka nikutume shamba kwa sultani. Yule kijana akasema: heiwallah waziri. Akamwambia: ondoka magharibu wende ukanichukulie bunduki ya sultani shamba. Yule kijana akasema: heiwallah.

Bassi, akaondoka yule kijana akaenda hatta akafika katikati ya njia akamwona mtu anayemjua hayati baba yake akamwambia: je fullani uko huku sasa? Yule kijana akajibu akamwambia: naam, mimi niko kwa sultani wa mji hunakaa **)

---

*) Hier ist shamba, obwohl es nicht noch besonders in den Locativ gesetzt ist, als Ortsbezeichnung behandelt, der die Genitivpartikel kwa folgt.

**) Man beachte die Form, die die Dauer eines gewohnheitsmässig bestehenden Verhältnisses ausdrückt.

naye. Ikawa kujizumgumza muda wa saa mbili wakiulizana hali hatta akasahau anakokwenda alikotumwa na waziri, bassi.

Huku nyuma waziri akathani akasema ndani ya moyo wake, sasa yule kijana amekwisha kutiwa ndani ya handaki, nitakwenda kutazama. Akaondoka waziri akaenda hatta akafika, marra alipofika wale watumwa wakamkamata yule waziri wakamtia ndani ya handaki wakafukia, bassi.

Na yule kijana pale alipokaa na yule mtu anayemjua baba yake akakumbukia kama mimi nimetumwa na waziri shamba nitakwenda maana hapa nimekaa sana nimekawia, bassi. Wakaagana na yule mtu akaondoka akenda zake hatta katika shamba. Akawakuta wale watumwa wanafukia handaki akawauliza: nini mnafukia hapa? Wale watumwa wakamwambia: tunafukia handaki na ndani ya handaki yumo waziri, maana alituambia jana, tuje tuchimbe handaki na kulla atakayekuja auwali tumtie ndani ya handaki, bassi; hakuja mtu illa yeye mwenyewe na sisi tumemkamata tumemtia, wa salaam. Hiyo ndiyo khabari yetu. Tamat.

Bassi yule kijana aliposikia khabari ile akashukuru Muungu akasema: ilhamdu lillah rabb ilalamina, handaki hili nimefanyiwa mimi, walakini Muungu ameninusuru, ameingia mwenyewe aliyefanya, bassi.

Yule kijana akarudi mjini kwa sultani akaenda akamuaridhia khabari ile yote tokea auwali hatta akheri. Sultani akamwambia: kwa nini usinambie tokea kwanza. Yule kijana akamujibu sultani akamwambia sultani: mimi nalirithi kwa baba yangu elfu tatu na fedha hiyo yote nalinunua maneno matatu. Sultani akamwambia: maneno gani ulionunua? Akamwambia: la kwanza, nalinunua: ukiona neno usinene neno, ukinena neno litakupata neno; thamani yake elfu reale; na la pili nikanunua: ukienda njia jua likichwa katika njia na wewe uko njiani usiende, lala hapahapa njiani, thamani yake elfu reale; na la tatu nikanunua: ukipita mahala ukiona mtu akikukaribisha kaa hatta kama una shughuli elfu, acha shughuli ukae kidogo; thamani yake na lo elfu reale; na mimi

nimeona fayida yake yote maneno matatu, ilhamdu lillahi ilalamina.

Aliposikia khabari yake yule kijana akazidi kumsh akampa na mali elfu sabaa zayidi kuliko mali yake. salaam. Tamat.

Mazehebi ya watu wa Unguja.

(Sitten der Sansibarleute.)

Bism illah irrahman irrahim!

Alhamdu lillahi rabb ilalamina. Alhamdu, maana yake tutahimidi; lillahi, maana yake mwenyi ezi Muungu. Rabbi maana yake alio bwana. Ilalamina maana yake kwamba watu wote.

Na lugha ya kisawahili hunena mtu akiwa anataka kula, auwala hunena: bism illah irrahman irrahim. Na kiisha kula hushukuru hunena: Alhamdu lillahi rabb ilalamina. Hiyo ndiyo tabia ya kiswahili na Waarabu kazalika hunena vilevile. WAllahu aalam, maana yake Mungu ndiye ajuaye, sisi viumbe hatujui neno. Na katika lugha ya kisawahili ikiwa mtu amekuuliza neno na wewe hulijui lile neno, hujibu yule aliouliza: WAllahu aalam. Maana yake: mimi sijui. Na katika lugha ya kiarabu kazalika, hunena WAllahu aalam. Ndivyo tulivyoambiwa na waalimu wetu. Nasi hatuna budi kusema kama tulivyoambiwa na waalimu wetu.

Maana kwa mazehebu yetu mtu anayemkhalifu mwalimu wake kwa neno kwetu mtu huyu si mtu wa kusuhubiana naye. Maana kwetu radhi za mwalimu kubwa sana kwa mazehebu ya kisawahili na Waarabu kazalika.

Bassi, na watu wanaozama katika bahari ya maneno sharti mjue mazehebu ya maneno kwanza, ndipo mseme haya; ndio tulivyofundishwa na waalimu wetu.

Bassi ndio tunaingia katika mazehebu ya mambo. Auwal zalika (maana yake: la kwanza) ikiwa mtu anataka kwenda

njiani kwa mazehebu ya kisawahili hunena: A'úzu billahi min eshsheitān irrajīm, bism illahi irrahman irrahim. Na Waarabu kazalika. Bassi maana yake: ni kumlaani shaitani njiani usione mambo mabaya; na maana ya bism illah irrahman irrahim ni kutawakali Muungu wako kwa njiani lake. Ndivyo tulivyo ambiwa na waalimu wetu hatta na wazee wetu. Bassi. Na mtu atakaye kusema kisawahili shurti ajue haya kwanza. Bassi.

Tena tunakuja katika mazehebi ya kwenda kwa watu wambao wakubwa. Ikiwa umekwenda kwa mtu mkubwa kuliko wewe, ukifika mlangoni sharti ubishe: hodi, marra ya kwanza na marra ya pili na marra ya tatu, kama hukuitikiwa kwa mazehebu ya kisawahili hurudi mtu uliokwenda. Na Waarabu kazalika hurudi. Ama ukibisha marra ya kwanza ukiitikiwa, huuliza mtu uliokwenda: bwana yuko; hukujibu yule mtu aliyoitikia hodi: yuko, ama: hayuko. Na kiwa yuko wewe husema: mwambie fulani bin fulani amekuja, anataka kuonana na weye. Huenda yule mtu kumwambia: amekuja fulani bin fulani, yuko nje. Hunena yule uliomwendea: mkaribishe. Huja yule mtu akakuambia: karibu, pita. Wewe uliokwenda huingia ndani.

Ukimwona yule mtu uliomwendea humwambia: subalkheiri kama usubuhi; na kama alasiri, humwambia msalkheiri. Ukiisha mwambia msalkheiri, yeye hukujibu: labulkheiri. Walakin siku hizi Unguja hakuna kawaida hii; siku hizi kawaida yao: wewe husema: sabahaka labulkheiri; na yule mtu unayemwambia hukujibu: Allahi sabahaki bulkheiri, kēfu halaki? Wewe hujibu: taiyib. Khabari ya siku nyingi? Wewe hujibu: jema. Watoto hawa jambo? Wewe hujibu: hawa jambo. Onaje hali yako? Wewe hujibu: sijambo.

Ukiisha ukakaa mahali pa kadiri yako, usikae mahala pa watu wambao wakubwa kuliko wewe. Kaa mahala pa kadiri yako. Na watu wakubwa wakisema wewe usijibu illa waseme nawe ndipo uwajibu.

Na pale mahali pakihudhuria chakula usinawe wewe mdogo kabla ya watu wakubwa hawajanawa. Sharti wanawe watu wakubwa kwanza wote, khalafu unawe wewe.

Na mkikaa sahanini mnakula usinyoshe mkono wako kabla ya watu wakubwa hawajatia mkono. Sharte watie watu kwanza. Ndio utie wewe mdogo. Na kitoweo usitwae wewe mdogo, sharti utileo na wakubwa wako hatta mwishe kula. Na mkiisha kula huja maji ya kunawa wewe mdogo usinawe kabla ya watu wakubwa hawajanawa. Sharti wanawe watu wakubwa kwanza, ndipo unawe wewe mdogo. Na ukiisha nawa useme: Alhamdu lillah rabb ilālamina, ahsanta, jazak Allahu elfu kheir.

Ukiisha kusema hivyo ukae kitako, maana itakuja kahawa. Atakuja mtu mtwaaje kahawa atakupa kikombe cha kahawa, usipokee hatta waishe wakubwa kuliko wewe wote; khalafu upokee wewe.

Mkiisha kunywa kahawa na kama wataka kwenda zako, sharti uage kwa yule mtu mwenyi nyumba. Umwambie: kwa kheri nakwenda zangu. Yeye atakujibu: marra unakwenda zako hatta hatujazumgumza. Wewe hujibu: nna shughuli leo sana, sipati kuzumgunza sana, walakini ntakuja siku nyingine insha Allah tutazumgumza, walakin leo nisamehe, leo si na wasaa, nimepita kukujilia hali, maana si wajibu wangu kupita hapa nisije kukutazama.

Yeye yule mtu atakujibu: ahsanta. Wewe tena mwambie: kwa kheri. Yeye atakujibu: haya kwa kheri. Tena wewe sharti uwaambie wale watu pale mahala: Allahi mesiku bulkheiri, kama wakati wa lasiri; na kama wakati wa assubui sharti useme: sabahakum bulkheiri. Wao watakujibu: Allahu sabahaki bulkheir. Utakwenda zako unakotaka kwenda. Haya ndio mazehebu ya kisawahili na Waarabu kazalika, walakin Waarabu kwa lugha yao. Haya ndiyo tulioambiwa na waalimu wetu nasi hatuna budi kufuasa kauli za waalimu wetu.

Tamati. Maana yake: tamati imekwisha, bassi.

Sasa tena tunakuja katika mazehebi ya mtu na mzee wake. Ukiwa umekaa na baba yako usiseme neno hatta aseme na weye, wala akisema neno usimkaidi wala simwambie, sivyo, si adabu ya mtu na mzee wake kumkaidi maneno. Na ikiwa umefuatana wewe na baba yako mtoto hatangulii mbele, hutangulia mbele baba yako, si adabu mtoto kutangulia. Kawaida

ya mtoto huwa nyuma ya baba yake. Na ikiwa mnakula chakula sharti wewe mtoto hutwai kitoweo illa akupe baba yako. Mtoto hana rukhsa yakutoa kitu mbele ya baba yake illa apewe. Na kama hakupewa huwa ni bassi; walakin haya hayawi illa mtoto mwenyi adabu.

Walakini mtoto asiyekuwa na adabu hufanya kama anavyotaka nafsi yake. Walakini mwenyi adabu harithiki, maana hakubali kufanya mambo yasiofaa kufanyiza illa watoto wakianzali. Maana yake anzali yaani mtu asiyokuwa na adabu na hii maana ya anzali; huleta fasiri nyingi sana: mtu asiokuwa na adabu kwetu huitwa anzali; na mtu zalili, maana yake zalili nayo huleta fasiri nyingi; mtu maskini kwetu huitwa zalili na anzali mtu mujibu dhaifu, hajui mazehebi ya watu wala hajui heshima za watu wala hajui kiasi cha watu wala hajui kukisi watu yeye kwake. Killa mtu anayemwona humfanyiza sawasawa, naye hajui mkubwa kuliko yeye wala hajui mdogo kuliko yeye wala hajui bora kuliko yeye wala hajui dhaifu kuliko yeye. Wala hajui kutazama akili zake kwa kuwa nifanyize neno fulani: linalikhalisi mimi, halinikhalisi. Maana yake linalikhalisi linanifaa au halinifaa neno hili kulifanyiza.

Hajui kukisi mambo, hujifanyizia lile atakalo. Mtu yule huitwa jina lake anzali, maana hajui neno. Na kwa lugha ya kiarabu huitwa bughamu na kwa lugha ya kisawahili huitwa mjinga bardhuli na kwa lugha ya kiunguja kazalika huitwa bardhuli mjinga. Walakin kwa lugha fasihi hunena anzali na kwa lugha ya kipemba huitwa mpumbafu; na kazalika watu wa kiunguja hunena mpumbafu; walakin si mno, maana kwetu Unguja mpumbafu: mtu asioweza kufanyiza kazi ya nafsi yake huitwa mpumbafu. Walakin lugha fasihi huitwa bardhuli. Bardhuli na mpumbafu maana moja kwa lugha ya kisawahili.

Na maana ya mjinga: mtu asiojua maneno wala hajui mtu wala hajui mambo ya watu wala hajui kawaida za watu wala huuliza watu wajuao kawaida ya watu; akawa kama buzi, illa kasoro, buzi a na mkia yeye hana. Ndio kasoro yake kuliko buzi. Mtu yule kwetu huitwa mjinga. Na kwa lugha ya

maulamau huitwa maamuma, hajui mbele wala nyuma. (Maana yake maulamau: watu waalimu wanaojua mambo kuwailimu.) WAllahu aalam. Tamat. Yamekwisha mazehebi ya mtu na baba yake.

Sasa tena tunakuja katika mazehebi ya mtu na mzee wake mwanamke. Auwali zalika, la kwanza; mtu akiwa na mama yake sharti amjue kwa killa namna ya kumjua mtu mzee wake. Na ikiwa umekwenda nyumbani kwa mama yake, usiingie ndani illa kwa rukhsa yake.

Na watu wa kiunguja hunena kwa maana nyingi rukhsa, na lugha ya kisawahili hunena: usiingie ndani illa kwa izini ya mama yako. Na zote lugha mbili watu hunena, ili apendayo hunena hunena. Bassi.

Tena tumeacha haya maneno. Tunakumbusha khabari yetu ya adabu. Akikupa mama yako rukhsa kuingia ndani, wewe sema: bism Illah irrahman irrahimi. Uingie ndani ukimwona mama yako umwambie kwanza: shikamoo. Yeye ataitikia: marahaba, hujambo? Wewe utasema: sijambo. Atakwambia: khabari ya kwako? Wewe utasema: jema. Kama wa na mke, atakuuliza: mkwe wangu hajambo? Wewe utasema: hajambo min fadhili lillahi taala; walakin wewe waonaje hali yako. Yeye atakujibu: hali yangu mzima na afia zangu alhamdu lillahi rabb ilalamina. Wewe tena useme: ndivyo tuombavyo.

Haya ndio maneno ya kisawahili zamani na zalika kiunguja zamani hunena hivi, na hatta sasa watu wa shamba hunena na watu wasiojua lafudhi ya maneno hunena kama hivi. Walakin siku hizi watu wa kiunguja hawaneni. Maana siku hizi killa mtu hunena kwa fasaha (yaani ufasaha kama una ufasaha wa maneno sharti ujue harufu kwa killa neno unaonena ulinene kwa harufu). Ndipo wanapoambiwa na watu wajua: wa ama fulani bin fulani fasihi wa kusema.

Walakin ukisema bila harufu huambiwa fulani hajui kusema, bassi. Yahitaji mtu sharti ajue kusema ajue na harufu, ndipo yanayokuwa mambo yake sawasawa. Walakin mtu akijua kusema asijue harufu kwa lugha ya kiarabu hunena: kalkandili bila zaiti; maana yake: kama taa isio mafuta, hai-

waki, hainafayida, ndio maana yake kalkandili bila zaiti. Na kwa lugha ya kiarabu hunena: ka shajara bila thamer; maana yake kama mti usiozaa. Na baathi ya watu hunena: kama mti usio matunda, na hizi lugha zimekhitilifiana, walakin watu wa kiunguja hunena kwa zote lugha mbili. Bassi.

Tena sasa tunakuja katika maneno yetu ya auwali ya ufasihi. Ama fasihi akienda nyumbani kwa mama yake akifika mlangoni hubisha hodi akaitikiwa hodi akataka rukhsa ya kuingia ndani kwa mama yake akapewa rukhsa akaambiwa: pita, fasihi husema kwanza: bism Illahi waala millati rasulu Allahi salla Allahu aleihi wa salam. Tena akasema: bism Illah irrahman irrahim, akaingia ndani.

Akimwona mama yake kumwambia: subalkheir, kama ule wakati uliokwenda asubuhi, na kama wakati wa alasiri mtu hunena: mesalkheir, umeshindaje leo? Mama yako hukujibu: sijambo alhamdu lillah rabb ilalamina. Tena yeye hukuuliza: wewe je? wewe hujambo. Wewe husema: sijambo. Tena hukuuliza kama u na watoto na kama u na mke, mama yako hukuambia: watoto hawajambo? Wewe husema: hawajambo. Tena hukuambia: mkwe wangu hajambo? Wewe hunena: hawajambo wote min fadhili lillahi taala. Yeye hunena ndivyo tuombavyo. Bassi.

Sasa tunalifasiri neno la mkwe. Maana yake mkwe yaani mke wa mwana we. Kwa lugha ya kisawahili mke wo mama yake humwita mkwe na ndugu yo mwanamke mke o kumwita wifi, na nduguyo mwaname mke o huita shemegi; maana kwa lugha ya kiswahili hunena shemegi yake; na baba yake kazalika mke o huita mkwe. Bassi.

Na wewe mama yake mke o sharti umwite mkwe; na kazalika na baba yake wewe humwita mkwe. Maana kwa lugha ya kisawahili hunena wakwe o baba yake mke o na mama yake na ndugu ze huita shemegi; maana kwa lugha ya kisawahili hunena ndugu zake mke o ikiwa mwaname ikiwa mwanamke wewe hunena shemegi. Maana kwa lugha ya kisawahili hunena ndugu ze mke o shemegi zako. Na kwa lugha ya kiarabu hawaneni mke wa mwana we baba ye haneni mkwe, maana

kwa lugha ya kiarabu neno la mkwe kwao hakuna, hunena shemegi ikiwa mama yake mke o ikiwa ndugu ye mke o ikiwa jamaa zake mke o wewe wote huwita shemegi. Na wazee wake mke o kazalika wewe hukwita shemegi. Hivyo ndivyo tulivyoona. Bassi.

Tena tunakuja katika maneno yetu ya auwali, tumeacha fasiri ya maneno, tunarudi katika khabari zetu za mtu kwenda kwa mama yake, bassi.

Mkiisha kuonana na mama yako mkaulizana khabari, mkiisha, wewe mtoto hukaa mbali na mama yako, usikae karibu na mama yako wala mshingu sana na mama yako, wala usiingie chooni kwa mama yako, wala usiingie chumbani kwa mama yako. Maana mambo haya kwa mazehebi ya kisawahili makeruhu. Maana yake makeruhu mabaya, yamekatazwa, bassi. Mambo haya hayamwaliki mtoto mwaname kufanyiza nyumbani kwa mama yake. Maana yake hayamwaliki kwa lugha ya kisawahili hunena haifai, na karah hunena vibaya walakin kwa lugha ya kiunguja hunena kwa zote lugha mbili: haimwaliki fulani kufanyiza hivi, na baathi ya watu hunena haifai fulani kufanyiza hivi, bassi. Tena twalifasiri hili neno baathi ya watu, maana yake baathi ya watu yaani na watu wengine, ndio maana yake, bassi.

Tena tumeyaisha. Tunakuja katika khabari ya auwali. Tumenena auwali wala usiingie chooni wala chumbani kwa mama yako, karah, illa akiwa mgonjwa. Pale anapokuwa mgonjwa maazuri mtu huingia kumtazama mama yake. Maana watu wamenena mtu mama yake akiwa mgonjwa maazuri kuingia kumtazama. Na maana yake maazuri yaani rukhsa kwa lugha ya kisawahili, na kwa lugha ya kiunguja hunena kwa zote lugha mbili.

Na ndugu yo kazalika haifai kumgusa wala kuingia chumbani kwake ila kuuzuru maana makeruhu kwa mazehebi ya kisawahili na watu wa kiunguja kazalika. Walakin Waarabu hunena yafaa mtu kuingia kwa mama yake na kwa ndugu yake na mazehebu yamekhtalifiana, killa mtu hunena kwa mazehebi yake na tabia yake, na hapana mtu ajuaye mazehebi

sahihi illa Mngu, ndiye ajuaye. Na mtu arifu hunena: Allahu aalam bisawabu.

Bassi, sasa tunaingia katika anwani ya vitu na vyakula na matunda na nyama, jumla ya vitu yalivyoharimishwa. Maana vitu vingi wameharimisha na vingi wamehalalisha.

Auwali zalika la kwanza, shekh illbadhi na shekh ilmuslemina amenena: zi na haramu. Maana ameona kauli ya Mngu katika kitabu chake yaani katika korān ilathīm wa lfurkān il majīd kanena Mwenyiezi Mngu: azzaniata wazani fa jildati kulla wahedi minhum māata jaldaha. Maana yake mtu anayezini na yule anayezinwa hokumu yao, watu wawili wale wanaofanyiza mambo yale mwanamke na mwaname killa moja hajalidiwa jelidi mia. Maana yake jelidi, yaani jelidi hunena killa moja hupigwa fimbo mia.

Hio ndio kauli ya Mngu na masheikha wakafuata. Bassi. Sheikhi wa Ibadhi amenena: zi na haramu. Na shekh ishShafei kanena: haramu zi na. Na kazalika shekh ilHanefi kanena: zi na haramu. Na kazalika shekhi Maleki kanena: zi na haramu. Na kazalika shekh ilHambali kanena: zi na haramu. Maana Mngu kaharimisha. Bassi. Na kwa kulla mtu anayejidai kwamba yeye katika muslemina sharti ajue haya. Nasiyojua haya sisi hunena bahaim. Maana yake bahaim mjinga; yeye anajidai muslemina na maana ya muslemina hajui, huitwa bahaim.

Tumeisha tafsiri ya maneno, tunakuja katika khabari zetu za auwali. Akanena la pili walioharamisha ilmuslemina, amenena sheikha lIbadi: mali ya yatima kula haramu, na kushika mali ya atima haramu illa mtu iliyoambiwa na sultani kwamba wewe shika mali ya watoto wa fulani bin fulani hatta wakue, wewe watoto uwakabidhe mali yao. Mtu yule anayeambiwa na sultani kushika halali, kula haramu. Maana yake mali ya yatima yaani mali ya watoto wadogo na baba zao wamekufa; yale mali anayowakhalifu baba yao kwa lugha ya kisawahili hunena mali ya yatima.

Na sheikha wa Ibadhi kanena mali ya yatima haramu, maana ye asingenena illa kaona kauli ya Mngu katika lkorani. Maana Mwenyiezimngu kanena kauli yake ya haki: Wa amma

litima fala takihira wa amma sailan wala tanhira wa amma bi neemati rabbuka na haddithi. Bassi.

Na sheikha wa Ibadhi kwa sababu kuona aiya hii katika masihafu naye akanena kwa kuwa mali ya atima haramu. Na shekha lHanefi kazalika kanena haramu. Na kazalika sheikha Maleki kanena haramu. Na kazalika sheikha lHambali kanena haramu. WAllahi aalam bisawāb.

Bassi tena tunakuja katika khabari ya vinyu yaani khabari ya ulevi vinyu na tembo na pombe na kasumba na madadi na bangi na tumbako. Amenena isheikha ilām katika sheikha wa Ibadi vinyu na tembo na pombe na madadi na tumbako na afiuni haramu, na kwa killa kitu ambachoota chakula kichwa kikizunguka yaani ukalewa kwa mazehebu ya Ibadhi haramu hatta ukila sana hatta chembe ikakulevya haramu kwa kauli ya shekha lIbadi.

Maana amenena: nimeona katika lkorāni kauli ya Mngu, kanena: harramnakum ilkhomer wa lmaisari wa lazlām. Maana yake lkhomer vinyu, na maana yake lmaisār wa lazlām ni ulevi wote. Bassi. Shekha wa Ibadhi kanena haramu alipoona aya hii, bassi. Na sheikha ilimam Shafei amenena vinyu haramu kwa mtu anayejidai kwa kuwa yeye muslim na tembo kazalika na pombe kazalika na bangi kazalika na afiuni kazalika na madadi kazalika haramu, walakin tumbako si haramu. Na sheikha lHanefi kazalika kanena kama Shafei na sheikha Maliki kazalika na Hanbali kazalika. Maana mashekha wane hawa wote wanaabudu dini moja mazehebi mamoja, wote wane suni.

Walakin killa mtu hunena neno lake, walakin wawili furka wamefarikiana wawili mbali na wawili mbali. IshShafei na Hanefi kauli moja, na Maliki na Hanbali kauli moja. Maana kuna kauli ya Shafei na Hanefi kwa Maliki na Hanbali. Maneno yao Shafei na Hanefi yako baathi ya maneno, Maliki na Hanbali hunena kwamba haramu. Na yako baathi ya maneno ya Maliki na Hanbali yaani kwa Shafei na Hanefi hunena haramu. Bassi. Wamekhitilifiana watu wane, walakin wote suni, mazehebi moja. Na yako maneno ya suni Ibadhi hunena haramu. WAllahi aalam.

sahihi illa Mngu, ndiye ajuaye. Na mtu arifu hunena: Allahu aalam bisawabu.

Bassi, sasa tunaingia katika anwani ya vitu na vyakula na matunda na nyama, jumla ya vitu yalivyoharimishwa. Maana vitu vingi wameharimisha na vingi wamehalalisha.

Auwali zalika la kwanza, shekh illbadhi na shekh ilmuslemina amenena: zi na haramu. Maana ameona kauli ya Mngu katika kitabu chake yaani katika korān ilathīm wa lfurkān il majīd kanena Mwenyiezi Mngu: azzaniata wazani fa jildati kulla wahedi minhum māata jaldaha. Maana yake mtu anayezini na yule anayezinwa hokumu yao, watu wawili wale wanaofanyiza mambo yale mwanamke na mwaname killa moja hajalidiwa jelidi mia. Maana yake jelidi, yaani jelidi hunena killa moja hupigwa fimbo mia.

Hio ndio kauli ya Mngu na masheikha wakafuata. Bassi. Sheikhi wa Ibadhi amenena: zi na haramu. Na shekh ishShafei kanena: haramu zi na. Na kazalika shekh ilHanefi kanena: zi na haramu. Na kazalika shekhi Maleki kanena: zi na haramu. Na kazalika shekh ilHambali kanena: zi na haramu. Maana Mngu kaharimisha. Bassi. Na kwa kulla mtu anayejidai kwamba yeye katika muslemina sharti ajue haya. Nasiyojua haya sisi hunena bahaim. Maana yake bahaim mjinga; yeye anajidai muslemina na maana ya muslemina hajui, huitwa bahaim.

Tumeisha tafsiri ya maneno, tunakuja katika khabari zetu za auwali. Akanena la pili walioharamisha ilmuslemina, amenena sheikha lIbadi: mali ya yatima kula haramu, na kushika mali ya atima haramu illa mtu iliyoambiwa na sultani kwamba wewe shika mali ya watoto wa fulani bin fulani hatta wakue, wewe watoto uwakabidhe mali yao. Mtu yule anayeambiwa na sultani kushika halali, kula haramu. Maana yake mali ya yatima yaani mali ya watoto wadogo na baba zao wamekufa; yale mali anayowakhalifu baba yao kwa lugha ya kisawahili hunena mali ya yatima.

Na sheikha wa Ibadhi kanena mali ya yatima haramu, maana ye asingenena illa kaona kauli ya Mngu katika lkorani. Maana Mwenyiezimngu kanena kauli yake ya haki: Wa amma

litima fala takihira wa amma sailan wala tanhira wa amma bi neemati rabbuka na haddithi. Bassi.

Na sheikha wa Ibadhi kwa sababu kuona aiya hii katika masihafu naye akanena kwa kuwa mali ya atima haramu. Na shekha lHanefi kazalika kanena haramu. Na kazalika sheikha Maleki kanena haramu. Na kazalika sheikha lHambali kanena haramu. WAllahi aalam bisawāb.

Bassi tena tunakuja katika khabari ya vinyu yaani khabari ya ulevi vinyu na tembo na pombe na kasumba na madadi na bangi na tumbako. Amenena isheikha ilām katika sheikha wa Ibadi vinyu na tembo na pombe na madadi na tumbako na afiuni haramu, na kwa killa kitu ambachoota chakula kichwa kikizunguka yaani ukalewa kwa mazehebu ya Ibadhi haramu hatta ukila sana hatta chembe ikakulevya haramu kwa kauli ya shekha lIbadi.

Maana amenena: nimeona katika lkorāni kauli ya Mngu, kanena: harramnakum ilkhomer wa lmaisari wa lazlām. Maana yake lkhomer vinyu, na maana yake lmaisār wa lazlām ni ulevi wote. Bassi. Shekha wa Ibadhi kanena haramu alipoona aya hii, bassi. Na sheikha ilimam Shafei amenena vinyu haramu kwa mtu anayejidai kwa kuwa yeye muslim na tembo kazalika na pombe kazalika na bangi kazalika na afiuni kazalika na madadi kazalika haramu, walakin tumbako si haramu. Na sheikha lHanefi kazalika kanena kama Shafei na sheikha Maliki kazalika na Hanbali kazalika. Maana mashekha wane hawa wote wanaabudu dini moja mazehebi mamoja, wote wane suni.

Walakin killa mtu hunena neno lake, walakin wawili furka wamefarikiana wawili mbali na wawili mbali. IshShafei na Hanefi kauli moja, na Maliki na Hanbali kauli moja. Maana kuna kauli ya Shafei na Hanefi kwa Maliki na Hanbali. Maneno yao Shafei na Hanefi yako baathi ya maneno, Maliki na Hanbali hunena kwamba haramu. Na yako baathi ya maneno ya Maliki na Hanbali yaani kwa Shafei na Hanefi hunena haramu. Bassi. Wamekhitilifiana watu wane, walakin wote suni, mazehebi moja. Na yako maneno ya suni Ibadhi hunena haramu. WAllahi aalam.

Na kazalika khabari za nyama. Ilmuslemina hunena mbuzi na kondoo na ngombe na ngamia na paa na kuku na bata na njiwa halali kula muslemina. Na nguruwe na mbwa na punda na farasi na simba na tembo na chui haramu kula mtu anayejidai ye muslemina. Maana muslemina wamenena hawo mashekha ilmuslemina wamenena nyama wa barra baadhi halali na baadhi haramu. Na nyama wa bahari maana samaki wote halali. Maana killa kitu kinachoishi baharini halali. Walakin wako nyama wengine mtu hawezi kula, huna uchafu kula. Walakin kwa mazehebu ya muslemina halali. WAllahu aalam bisawāb.

Ama muslemina hatta wakanena killa kitu kinachotoka baharini halali; wasingalinena illa kwa maana wameona katika mistari ndani ya kitabu cha Mngu, amenena neno lake lilio bora, yaani sisi hunena: kauluhu taala; na wangine hunena: kauluhu jalla wa ala; na wengine hunena: kauluhu ilazizi; na wengine hunena: kauluhu ilathimu; na wengine hunena: kauluhu ilmannān; na wengine hunena: kauluhu rabb ilalamina, kauluhu ilhakki. Walakini haneni mtu mjinga maneno haya. Hunena mtu fasihi na mtu ālim.

Ama wakimwambia mjinga maneno kama haya, hayajui. Maana haya si maneno ya watu anzali, maneno haya maneno ya watu fasihi illisani na watu maalimu. Walakin ukinena na mtu mjinga inataka sharti nawe unene kijinga kama yeye. Maana apate kusikia maneno yako. Amma ukinena na mtu ambao fasihi arifu, sharti inataka unene kwa ufasihi, maana asikucheke. Maana kwa baathi ya watu mafasihi ukinena neno ukipotea, watu hukucheka sana, hukuambia: amma fulani bin fulani mjinga, hajui kusema, ulimi wake sifasihi, bassi.

Inataka killa mtu anayezama katika bahari ya maneno ajitahidi kuhafithi harufu. Maana mtu hawi fasihi illa ajue harufu; maana ajue neno la ze, na sini, na sodi, na dhe, na ṭe, na re, na ghaini, na kofu, na kiafu, na he, na ḥe, na the, na dhodi. Maana harufu hizi ngumu katika maneno. Bassi. Yahitaji mtu ajitahidi kuzijua hatta azihafithi.

Maana mtu akiwa anajua kusema kwa lugha fasihi kwa

mazehebu yetu husifiwa sana na watu humpenda sana kwa ufasihi wake. Bassi yataka mtu sharti ajue kusema, ajifundishe harufu hatta ajue. Bassi.

Tena tunamaliza maneno yetu ya auwali, amma muslemina hatta wakanena kitu chote cha baharini halali, kwa maana wameona kauluhu ilazizi maana kauli ya Mngu katika ilkurāni athimi: kāl Allahu taala, kanena Mwenyiezimgu: harramnakum said ilbarri wa hallalnakum said ilbahr. Na kauli nyingine kanena: wa jaalna ilmaya kulla sheiin haiyan; amma kauli ya: haṛramnakum ilbarri, maana yake: nimekuharimisheni nyama wa barra. Amma kauli ya: hallalnakum said ilbahri, maana yake nimekuhalalisheni nyama wa bahari. Wa amma kauli ya: wajaalna ilmaya kulla shaiin haiyan, maana yake: nimejaalia maji killa kitu cha ndani yake kizima. Bassi.

Na sisi hatu na budi kufuasa maneno yake, na kwa killa mtu ambaye anayejidai yeye muslemina hana budi illa atafuasa maneno haya. WAllahi aalam bisawāb.

Sasa tunaingia khabari ya wezi: amma katika hokumu ya muslemina; ada ya wezi: hukatwa mkono; akiiba marra ya pili hukatwa mkono wa pili. Amma mkono unaotangulia kukatwa mkono wa kulia: yaani hukatwa beina ya kighasha na mkono. Akiiba marra mbili hukatwa katikati. Akiiba marra ya tatu hukatwa begani. Akiiba marra ya ne hukatwa mkono wa pili wa kushoto beina ya kighasha na mkono. Akiiba marra ya tano hukatwa katikati ya mkono vivi hivi hatta ishi mikono. Ila kwa kauli ya Mngu, maana kanena: Assariku wa ssarikati fa kota'u aidiyahuma. Bassi. Mahakimu ya muslemina yaani wafalume wa muslemina walipoona mistari katika ilkorāni kauli ya Mngu imesabiki na wao wakafuata.

Walakin sharti inataka mfalme ambaye ádil hokumu yake ya ádil. Basi. Adil namna gani? Sharti inataka mfalme anayehokumu kwa hakki akatoa hakki kwa tajiri akampa maskini; akatoa hakki kwa nduguye akampa mtu mbali; akatoa hakki kwa thalim akampa mathulūm; akawa hapendelei mtu yaani yeye killa mtu mwenyi hakki yake kwa mtu yeye akamtwalia; akawa a na hokumu kwa hakki, hapendelei mtu yeye

kwake killa mathulumu bora na killa thalim kwake dhaifu na kwa killa alim kwake mwema na kwa killa fasiki kwake muovu, akawa mtu mujibu mcha Mngu sana, akawa mtawa sana, akawa hapendi raha ya dunia sana, akawa yeye mtu mjibu hana makosana, bassi, sisi hunena mfalume adil. Walakin lugha fasihi hunena sultani adil. Maana hokumu yake ya adil ya amru bilmaarufu wa yanha bilmunkahi. Maana anapenda hakki achukia bātil, bassi.

Yaani kwa mazehebi yetu hujuno sultani akiwa adil mwezi hukatwa mkono na mlevi hupigwa jildi themanini na zani hupigwa fimbo mia. Maana kaula ya Mngu kanena: azaniyata wa zani fa jaldati kulla wahedi minhuma mayata jaldaha wa sāriki wa sarikāti fa kotau aidiyahuma wa sakarani fa dhorubu thamanina jaldata. Na mtu akiua mtu bila hakki naye huuawa. Na mtu akimpiga mwenziwe fimbo naye hupigwa fimbo vilevile, ikiwa fimbo moja naye hupigwa fimbo moja, ikiwa fimbo mbili, ikiwa fimbo tatu, ikiwa kumi, ikiwa asherini, naye hupigwa vilevile. Ikawa mtu amempiga mtu selaha hupimwa jaraha akapigwa yule mtu aliyempiga vilevile.

Maana kauli ya Mngu imesabiki kanena: man katala kutila wa ljeraha kisasi. Maana yake: anayeua huuawa na anayepiga mtu naye hupigwa, ndio maana yake: man katala kutila wa ljeraha kisasi. Walakin sharti inataka sultani adil ajijue náfusi yake kwamba yeye ni adili na watu wote wamjue kwamba sultani adili hapendelei mtu, anahokumu kwa hakki, bassi. Akifanyiza mambo haya, watu wataridhika. Illa akiwa sultani jairi naye akataka kufanyiza mambo haya watu wa mji hawaradhiki; maana yake sultani jair, sultani asiyohokumu kwa hakki, hokumu yake anapendelea watu, maskini kwake dhaifu, tajiri kwake bora, naye si mtawanya. Akawa hupenda mambo ya dunia sana, hafikiri akhera, bassi, kwetu hunena sultani jair.

Na aidha mtu akazini kama ha na mke hupigwa fimbo mia. Na mtu mwenyi mke akizini hurujumiwa. Maana yake rijma: huchimbua shimo kubwa sana, urefu wake ziraa arbaini na upana wake ziraa arbaini, akitiwa yule mtu aliyezini

ndani ya shimo akapigwa kwa mawe hatta likajaa shimo. Ndio ada yake. Na mwanamke akiwa a na mume kazalika hurujumiwa.

Hii ndio sharia ya muslemina. WAllahu aalam bissawāb. Walakin siku hizi hakuna hokumu hizi kwa sultani. Maana siku hizi killa sultani jairi na hokumu zimeharibika. WAllahu aalam bilkhatima, maana yake: Mwenyiezimngu anajua khatima yake.

Auwali ya kisa hiki źama zakuzaliwa
mimi na umri wangu mimi wote
nimeandika humo.
Tamat.

*Alla*hum salla ala saiyidina wa maulana Muhammed
wa ala ali wa sahibihi wa sallam. Tamat.

Hekaya ilmezkur abd rasul Allahi
Amur bin Nāsur ilOmeiri.
Bijedihi. Berlin.

(Leben des Herrn Amur.)

Khabari ya wazee wangu.

(Geschichte meiner Eltern.)

Khabari ya kuzaliwa mimi.

Aliondokea baba yangu kutoka Maskati akasafiri hatta akafika Unguja; akaingia kwa ndugu yake Hamudi bin Amur akakaa siku kaza wa kaza, hatta khatima ilamri akatamani kuoa mke. Akamwambia ndugu yake: ndugu yangu, ya akhi, mimi nataka kuoa mke, walakin na mimi si na kitu katika mkono wangu, bassi.

Na yule ndugu yake akamwambia: bassi, na kama huna kitu utaoaje mke? Akamujibu: nataka unikopeshe fedha ijapokuwa ndogo, walakin lazima ila mimi kuoa mke. Maana yake: ndugu yangu, mimi ni mwanamume na mimi kijana mzima, hapa nilipo siwezi kukaa bila mke. Na yule ndugu yake akamjibu akamwambia: mke gani unayemtaka, ndugu yangu? Akamwambia: awaye yoyote yule, mimi namtaka. Akamwambia: wataka shamba au mjini? Akamwambia: mahala pawa popote pale panapo mwanamke. Akamwambia: Insha Allah taala, bassi.

Walipokwisha kufanya mashauri yao wakakaa hatta walipo kuichuma wakashukia mjini yeye na ndugu yake wakaenda hatta wakafika kwa mzee wao said Sud Muhindi wakamuaridhia khabari zao zote walizo nazo za posa. Bassi yule mzee wao akasema: insha Allah tutatafuta mwanamke anaye chochote tukaoze, bassi. Wakaulizauliza hatta wakapata mtu mmoja. Akawambia: mimi namjua mwanamke mmoja, ame-

fiwa na mume wake naye a na watoto watatu, wawili wanaume, mmoja mwanamke; mmoja jina lake Maseudi bin Rashid na mmoja Ali bin Rashid, na mwanamke Ghasha binti Hasan, naye ndiye mdogo wao huyu mwanamke; athani*) mwanamke huyu atakufaa, naye a na kitu kidogo, a na shamba moja Kikaanguni na moja Buibui, a na na watumwa, athani, wanapata kumi na sita, na waana we wa na mali, wamerithi kwa baba yao, labuda atakufaa mwanamke huyu, bassi.

Baba yangu akasema: naam, nataka kumposa, utakwenda wewe kuniposea. Yule mtu akasema: kwa ni mimi siendi? Ukinituma nitakwenda kuposa, maana kuposa ni thawabu, bassi. Wakafanya mashauri wakamtuma yule mtu akaenda akaposa akakubaliwa baba yangu akaoa. Naye hana hatta pesa moja, yaani mama yangu akakubali, bassi.

Khabari yangu mtoto.

(Geschichte meiner Kindheit.)

Hatta khatima wakahamia shamba Buibui wakakaa; hatta khatima wakarudi mjini wakakaa siku kaza wa kaza; hatta khatima baba yangu akasema: afdhali mke wangu tuhamie shamba Buibui wakahamia shamba Buibui wakakaa muda wa miezi sita. Nikazaliwa mimi nikaitwa jina langu mzee. Nikazaliwa katika mwezi wa ilhaji siku ya jumaa a tatu mwezi kumi na tatu kwa saa ya sita athuuri sene 1285, na mulki wa said Majid bin Saīd bin Sultan.

Baba yangu akafurahi sana na mama yangu akafurahi sana na yule ndugu ya baba yangu akaja akanitazama akaja na mke wake akanitazama, bassi. Hatta baada ya mwezi kupita akaja ndugu wa baba yangu Hamudi bin Amur akanichukua kwake Kwarara nikakaa kwa mke wake na jina lake Zafarani binti Abdallah Habeshia. Naye alikuwa akinipenda mimi sana zaidi kuliko ndugu ya baba yangu, bassi.

---

*) athani ist eine arabische Form, 1. pers. Imp.

Hatta khatima yule mke wa ndugu ya baba yangu akafa, bassi, akawa mimi kuchukuliwa kwa mama yangu nikarudishwa mjini kwa mama yangu, bassi. Mama yangu akanunua vijakazi viwili wa kunilea mimi. Wakakaa muda wa ijummaa moja wale vijakazi wakafariki wote wawili siku moja, bassi. Ikawa mimi sina yaya, ikawa ndugu yangu Ghasha binti Hasani ndiye yaya wangu akinilea mimi hatta nikapata kijana wa miaka miwili. Akaja mama yake baba yangu kutoka Maskati ikawa mimi kukaa kwa bibi yangu siku kaza wa kaza. Hatta khatima yule bibi yangu akafa. Akabaki shangazi langu aliyekuja naye bibi yangu; naye jina lake Zuwina binti Amur ilOmeiriya na binti wake Aza binti Muhammed.

Ikawa mimi kuhamisha kwa mama yangu, bassi. Nikakaa kwa mama yangu. Hatta khatima baba yangu akasema: afdhali tuhamie shamba. Mama yangu akasema: haya mume wangu, bassi. Wakahamia shamba wakakaa, bassi. Na yule ndugu yake baba yangu Hamudi alikuwa mtu mkubwa sana kwa said Majid, a na heshima sana, bassi. Hatta khatima tokea muda waliohamia shamba wazee wangu hawakupata mwezi mmoja illa walisikia said Majid amefariki. Na mimi kijana wa miaka mitano, bassi.

Wazee wangu wakarudi mjini wakakaa. Akatawala said Bargashi akasema: nataka watu Waarabu au Wangazija au Watwana au Waswahili au watu waliwowote niwapeleke Unyamwezi wakampige Mirambo, bassi. Said Bargash aliposema vile marra haukupata mwaka marra kikaja kimbunga, kikaangusha minazi kikaangusha na majumba yote, watu waliokuwa matajiri wakawa maskini, maana mashamba yao yote yameteketea minazi na migarafuu yote, bassi.

Baba yangu akasema akamwambia mama akamwambia: mimi, mke wangu, nitakwenda kwa Unyamwezi, maana yake sasa hatu na kitu, minazi yote imeanguka na migarafuu yote imeanguka na sisi hatu na shauri ya kufanya, afadhali mimi nitasafiri, bassi. Wakafanya mashauri ya kusafiri na yule ndugu yangu Ali akasema: na mimi kazalika nataka kusafiri pamoja na baba, bassi.

Wakaondoka wakasafiri baba yangu na ndugu yangu Ali na ndugu yangu Khalidi, mtoto wa shangazi langu, na mtoto wa shangazi langu mungine jina lake Sleman bin Salim. Na mama yangu akatoa mtumwa wake, jina lake Akilimali. Wakaondoka wakasafiri watu kaza wa kaza. Na huko nyuma mimi na mama yangu na ndugu zangu Maseudi na ndugu yangu mwanamke binti Hasan na ndugu ya baba yangu Hamud bin Amur.

Na wao waliambiwa: twaeni sasa reale 20 na mkirudi mutapata fedha yenu yote ya miezi mtakaokaa Unyamwezi. Wakasema: Heiwallah saidina. Wakaondoka wakaenda zao, bassi. Na huko nyuma mimi nikapata ugonjwa wa ndui mimi na ndugu yangu mwanamke na watu wote nyumbani. Mama yangu akamwambia ndugu ya baba yangu: tafadhali bwana nataka unipatie kiwacho chote nipate kula na huyu kijana, maana yake huyu kijana hawezi na mimi si na kitu na baba yake amesafiri naye hakuniachia kitu; au mchukue mtoto wenu, maana mwana wa ndugu yako bassi.

Yule ndugu ya baba yangu akamjibu: mimi si na kitu wala simchukui, aende akanitilie wanangu shamba, la, siwezi, bassi. Mama yangu akanyamaza asiseme neno la pili akajua: sasa nikasema ataleta maneno mengi huyu; akasubiri, bassi. Hatta khatima mama yangu alikuwa na mtwana wake, jina lake Sumail, naye mtwana huyu huenda kazini akileta mapesa, ndio tunayokula mimi na mama yangu; ikawa vivyohivyo hatta mimi na ndugu yangu tukapona ndui, na mimi kijana wa miaka sabaa.

Nilitiwa chuoni.

(Schulzeit.)

Mama yangu akasema kumwambia ndugu yangu Maseudi akamwambia: huyu kijana amepata miaka sabaa sasa na baba yake hayuko na mimi nataka atiwe chuoni akasome, bassi. Yule ndugu yangu akasema: naam afadhali nitampeleka akasome, bassi. Akafanya mashauri wakafanya na sadaka. Nika—

tiwa chuoni kwa maalimu Abdallah ilMadadi Kiponda. Nikakaa ili kusoma siku kaza wa kaza hatta baba yangu akaja. Naye mgonjwa sana wa tumbo akafanya dawa hatta akapata afya.

Wakaulizana khabari za safiri wakaelezana khabari yote ya walikokwenda. Na huku mama akamweleza khabari yote ya nyuma wanachotoka, bassi.

Hatta khatima baba yangu akamwambia mama yangu: huyu kijana tokea alipoingia chuoni hatta sasa tunaona hajui kitu, afadhali tutamtoa tutamtia katika chuo cha serkali, wanakosoma watoto wa said Bargash, bassi. Mama yangu akasema: haya chema unavyoona, ndivyo bassi. Wakanitoa wakanipeleka chuo cha serkali, na mimi kijana wa miaka minane. Nikasoma muda wa miezi sita nikatoroka nikaenda kwa ndugu yake baba yangu shamba Fuoni. Nikakaa hatta khatima akaja baba yangu akanikamata akanirudisha bassi.

Hatta khatima nikatolewa katika chuo cha serkali nikatiwa chuo cha maalimu Shekhi bin Fakihi ilMalindi. Nikakaa muda wa mwezi. Baba yangu akasafiri. Huku nyuma mama yangu akafanya mashauri na ndugu zangu ili kutia mimi katika jando bassi. Nikatiwa mimi katika jando na mimi kijana wa miaka tisaa. Nikakaa hatta baba yangu akarudi alikosafiri. Nami mule katika jando mimi na mtumwa wangu Kheiri na Abdulkheir, bassi. Hatta khatima tukatolewa tukapata zawadi kaza wa kaza, bassi. Hatta khatima nikarudi chuoni kusoma, ikawa mimi kulla siku utoro, baba yangu akafanya pingu akanitia hatta nikakhitimu nikatolewa chuoni. Na mimi kijana wa miaka kumi na moja, bassi.

Hatta khatima baba yangu na mama yangu wakagombana. Na sababu: baba alisema: mimi nataka kuoa mke khadimu ya ndugu yangu. Akamwambia: ukioa, mimi utaniacha, bassi. Hatta khatima wakafanya ugomvi wakaachana. Na baba yangu akaoa mke khadimu ya ndugu yake, na jina lake Tatu binti Sumaili, bassi. Na mama yangu akaacha kwa kuwa mali yake yote hatta na jumba yake ya njia kuu akanyanganywa na yule mtwana aliyekuwa akifanya kazi wakati nilipokuwa mimi na ndui naye alinyanganywa na jina lake fundi Sumaili. Na

[illegible]

[illegible] yangu na yaya [illegible]
[illegible] na yule ndugu yangu akafa [illegible]
[illegible] yangu mtoto wake mimi, bassi.

kakaa na mama yangu. Hatta khatima saidi Bargash akafa akatawali saidi Khalifa bin Said.

Ikawa mimi katika kazi ya askari nikatoka nikakaa mimi ikawa kazi yangu kukata vitambaa nikashona. Nikaona haifai ikawa kusafiri nikafanya biashara ya kulla kitu katika Mrima wa Pangani, bassi. Hatta khatima ikawa vivi siku kaza wa kaza. Na yule ndugu wa baba yangu akafa, yule Hamudi bin Amur, ikawa baba yangu kule Mrima peke yake na huku Unguja yule shangazi langu akafa na yule binti wake akafa. Ikiwa mimi Unguja mgeni, wasalaam.

Hiki kisa cha wazee wangu na mimi tokea sene 1285 hatta sasa sene 1310. Na sasa khabari ya safari yangu nilipo kuwa askari. Nalisafiri kwenda katika vita alipouawa Mdachi daktari walakini jina lake silijui katika Kismayu. Tukafanya mambo kaza wa kaza na mimi sikupata kitu cha heshima, na khalafu tukasafiri Pemba katika vita aliowawa nakhoza katika London Muingreza, sikupata heshima wa salaam.

Na katika khabari ya mwanamke niliyooa binti Saidi bin Khalfani, alipoona mimi si na kitu na mimi nimeoa mwanamke mungine akanambia: niache. Mimi nikamuliza: kwa nini? Akanambia: sababu umeoa mke mungine na tena hu na kitu. Na mimi nikamwambia: na kama sababu ndio hiyo, sikuachi. Akasema: utaniacha. Akaenda kunishitaki kwa jenerali wangu Matthews asipate haki akaenda nishitaki kwa kadhi Nasur asipate haki akaenda akanishitaki kwa kadhi Abdulazizi asipate haki ikawa kunishitaki kwa kulla siku naye hapati haki. Ikaendelea hatta na mama yake kuyaingia maneno yeye tu naye akafanya wazimu ikawa naye kunishitaki na kujitwika nguo mbovu kwenda nazo kwa kadhi usiku akawa hatta na ndugu yake naye akafanya wazimu ikawa na majirani zake wote kufanya wazimu, mchana hunyamaza na usiku hutanga nguo kwa makadhi, kwa kulla siku ikawa ndio kazi yao hiyo na vilio daima kama amekufa mtu nakudwiwa.

Hii ndio khabari ilionipata mimi tokea mimi kijana wa mwaka moja hatta sasa tokea sene 1285 hatta 1309, sijui khatima na ngine ya mbele; ya nyuma ni haya; na ya mbele ayajua Muungu na mtume we Muhammed. Wa salaam. Tamat.

Safari ya Berlin.

(Reise nach Berlin.)

Na hiki kisa cha safari yangu ya Berlin, nitaanza kueleza hapa katika kartasi hii.

Auwali nazukuru mimi Amur bin Nasur bin Amur ilOmeiri katika khabari ya safari ya Berlin Ulaya wa Majermani. Auwali naliondoka Unguja nikamwambia mama yangu: Mama, mimi nikijaaliwa nitasafiri Ulaya. Mama yangu akanambia: unakwenda kutafuta nini, mwanangu? Nikamwambia: nakwenda kutafuta kujuikana na watu na kutafuta riziki. Mama akanambia: haya mwanangu, walakin usitusahau kwa chochote huku nyuma. Nikasema: la, insh Allah taala, bassi.

Nikaondoka nikaaga mke wangu binti Rashidi nikaaga na mama yangu, wala sikuaga majirani wala watu wangine illa watu hawa. Nikaingia katika marikebu usiku. Na aliyenipeleka pwani yaya yangu Siyenu na ndugu yangu Khalid bin Muhammed; nikalala hatta asubuhi tukasafiri hatta tulipopata saa tisaa tukapata Tanga tukalala hatta kulipopambazuka asubuhi. Tukaondoka tukasafiri hatta kwa siku ya sita tukaona Adeni. Hatta alasiri tukaingia Adeni nikashuka katika Adeni nikapanda gari nikaingia katika Adeni. Na mimi nimeona katika Adeni mji wa Adeni nikaona na soko ya Adeni na katika bandari nikaona Wasomali ndio askari wa fordha. Na mji wa Adeni kama mji wa Pangani na milima kama Pangani na majebali makubwa. Sasa nimeona na mizinga katika majebali na watu wakapita chini ya majebali, bassi. Hatta khatima kwa siku ya sabaa tukasafiri tukaenda muda wa siku tano tukapata Suesikanali nikashuka katika mji wa Suesi nikaona gari la moshi nikaona na farasi nikaona na nyumba ya pasha nikaona yote niliyoona, bassi.

Hatta siku ya sabaa tukasafiri muda wa siku moja u nusu tukaingia katika mto mwembamba sana na mto huu umechimbiwa na Wafransa tokea Suesi hatta Port Said, bassi. Hatta kwa siku ya pili tukapata Port Said nikashuka katika Port Said nikatezama mji wa Port Said nikaona nguruwe wanatembea

katika mji usiku nikaingia madukani nikanunua kofia bassi. Nikarudi markebuni nikalala hatta asubuhi tukasafiri tukaenda mwendo wa siku tatu katika bahari ya Stambuli hatta tukaisha kwa siku ya sita tukapata Ulaya wa Mataliani. Nikashuka ndani ya mji nikatembea katika mji wa Mataliani. Nikaona mnara mkubwa nikaona na kilima kubwa sana na ndani ya kilima kinatoka moshi. Nikauliza ndio nini vile nikaambiwa: moto ule hatujui wapi unatoka tunaona na sisi vilevile, bassi.

Tukaondoka kwa siku ya pili tukasafiri hatta kwa siku ya tano tukapata mji nikauliza: hapa wapi? Watu wakaniambia: hapa ndio mji wa Wareno na jina lake Luzboa ndio Ulaya wa Ureno huu. Nikashuka nikaona ngome katika bahari na katika bandari. Nikaona na magari, bassi. Hatta khatima nikapanda marikebuni nikalala hatta asubuhi. Tukasafiri tukaenda mwendo wa siku tano tukaona mji nikauliza: huu mji gani? Nikaambiwa: mji huu ndio Ulaya wa Waholandi. Nikauliza: wanasema lugha gani watu hawa? Nikaambiwa: wanasema kama lugha ya Madachi; walakin si Madachi watu hawa, bassi. Tukaingia katika mji ule nikashuka nikaenda ndani ya mji nikaona mji wote wameenea mito nikaona na daraja za chuma, chini hupita marikebu na juu hupita gari la moshi; nikastaajabu sana khabari ile, maana yake tokea kuzaliwa kwangu sikuona khabari kama ile, bassi. Nikazunguka katika mji nikaona wanawake ndani yake wakikamata wanaume nikawaza: mji huu ndio mji wa wazimwi khasa, hii ndio akheri dunya na huku ndiko kupotea mimi Amur, bassi. Nikarudi markebuni nikalala. Hatta asubuhi tukashinda muda wa siku mbili; hatta siku ya tatu tukasafiri tukaenda hatta tulipopata usiku tukaona kandili zinawaka. Mimi nikauliza: wapi kule kunakowaka kandili. Watu wakanambia: kule ndiko Londoni Ulaya wa Wangreza, bassi. Nikatezama sana hatta kulipokucha asubuhi tukaona na majumba, walakin hatukushuka ndani ya mji. Nikaona na marikebu moja imetota, bassi.

Tukaenda hatta tukapata mji nikauliza: wapi hapa? Nikaambiwa: hapa ndipo Hamburg mji wa Madachi, ndio Ulaya

wetu ulio katika bandari. Nikauliza: ndio tumefika au bado. Nikaambiwa: sisi tumefika, walakin wewe bado, bassi. Mara nikaona mtu moja akaja akanambia: wewe ndio Amur bin Nasur ilOmeiri. Nikamwambia: naam, mimi ndiye Amur bin Nasur. Akanambia: haya, shuka katika marikebu, bassi. Hatta khatima nikashuka nikatiwa ndani ya gari wa farasi nikaenda hatta tukafika kunako bandari ya gari la moshi nikaambiwa: leo ndio utakwenda Berlin katika mji mkubwa sana nao ndio mji anaokaa sultani wetu na jina lake Kaiza Wilhelmu, bassi.

Hatta khatima nikaingia katika gari la moshi, markebu ya nchi kavu, na tokea Hamburg bandarini hatta Berlin na kama mtu anakwenda kwa miguu atakwenda kwa siku sabaa, walakin marikebu ya bara anakwenda kwa saa tano, bassi. Tukaondoka tukaenda hatta tukafika Berlin. Mara nikaambiwa: tumefika sasa katika Berlin, nikashuka ndani ya gari la moshi. Mara nikaona mbwana mkubwa daktari Büttner akanambia: wewe ndiye Amur bin Nasur? Nikamwambia: naam, ndiye mimi Amur bin Nasur. Na neno lake la kwanza akanambia: umekuja salamu salemina. Nikamwambia: naam. Akaniambia: ngalawa juu na wimbi chini. Nikamwambia: naam, ilhamdu lillahi rab ilalamina, bassi.

Hatta khatima akaniambia: sasa umefika hapa ndipo Berlini na sasa tuende jumbani, bassi. Tukaondoka tukaenda hatta nyumbani nikafanyiwa chakula nikala nikalala. Hatta assubui akaja daktari bwana mkubwa akanitazama akaniuliza hali yangu. Nikamwambia: hali yangu jema, bassi.

Hatta khatima akaniambia: tafadhali nataka wende kwangu ukatutazame. Tukaondoka tukaenda kwake nikamwona mama yake na mke wake na watoto wake wote akanambia: hawa ndio watu wangu. Wakafurahi sana wazee wake na mke wake na waana we kuwakuniona mimi na mimi nikafurahi sana nao nikala chakula hatta nikashiba. Hatta khatima nikarudi nyumbani kwangu nikakaa yeye kwa kulla siku huja kwangu akinitazama akaenda akanionyesha nyumba ya darasa akanionyesha na nyumba ya mizinga na nyumba hii sikupata kuona mimi tokea kuzaliwa kwangu hatta sasa wala mizinga

kama hiyo. Ikawa mimi naye akinifundisha namna ya mji, adabu ya watu wa huku akaninunulia mbau wa kujifunza kusoma na kitabu akanipa kwa muda wa siku hamse waasherini, bassi.

Hatta khatima tukaenda kufanya shauri mimi naye hatta khalafu akaja rafiki yangu naye ndiye maalimu wangu jina lake Hans Tsakhe akaja tukaenda tukafuatana kwa fundi kufanya nguo nikalinga nguo, bassi. Hatta khatima ikawa mimi kwenda kulla siku kwa bwana B. na kulla siku nikaenda mimi, yeye huona kama ndio leo siku kuu, bassi. Hatta khatima ikawa vilevile hatta sasa. Wa salaam.

Khabari ya katika Berlin.

(Sehenswürdigkeiten von Berlin.)

Hii ndio khabari ya katika Berlin niliyoona yote. Tamat.

Auwali ya kuja kwangu Amur bin Nasur katika Berlin. Auwali nimeona mji wa Berlin nikauliza mji huu watu wangapi ndani yake, nikaambiwa malyoni wa nussu malyoni watu walio katika mji huu, bassi.

Nikaona na majumba ya matabaka katika mji na kulla nyumba ghorfa tatu na ghorfa inne na kulla ghorfa yamejaa watu ndani. Na mimi katika siku nilizokaa zote nimeuliza: watu wenyewe majumba wako wapi? Sikuwajua, bassi.

Hatta khatima akaja rafiki yangu naye ndiye maalimu wangu jina lake Hans akanichukua kwake akanikerimu, bassi. Akanionyesha njia za mji kidogo akanionyesha na khabari za Berlin akanifundisha kuandika kidogo na kusoma hatta nikajua, bassi. Hatta khatima tukafanya darasa yetu. Ikawa mimi kupata wanafunzi kufundisha. Na mimi ikawa kazi yangu kuwafundisha lugha ya kisawahili na kuandika na wao kujifunza, bassi.

Hatta khatima akaja mwanafunzi wangu rafiki yangu jina lake Velten akanambia: tafadhali shekh Amur nataka tufanye usuhuba tufuatane pamoja. Nikamwambia: haya, bassi. Akawa mimi naye kufuatana na huku akinifunza namna ya kidachi.

fiwa na mume wake naye a na watoto watatu, wawili wanaume, mmoja mwanamke; mmoja jina lake Maseudi bin Rashid na mmoja Ali bin Rashid, na mwanamke Ghasha binti Hasan, naye ndiye mdogo wao huyu mwanamke; athani*) mwanamke huyu atakufaa, naye a na kitu kidogo, a na shamba moja Kikaanguni na moja Buibui, a na na watumwa, athani, wanapata kumi na sita, na waana we wa na mali, wamerithi kwa baba yao, labuda atakufaa mwanamke huyu, bassi.

Baba yangu akasema: naam, nataka kumposa, utakwenda wewe kuniposea. Yule mtu akasema: kwa ni mimi siendi? Ukinituma nitakwenda kuposa, maana kuposa ni thawabu, bassi. Wakafanya mashauri wakamtuma yule mtu akaenda akaposa akakubaliwa baba yangu akaoa. Naye hana hatta pesa moja, yaani mama yangu akakubali, bassi.

Khabari yangu mtoto.

(Geschichte meiner Kindheit.)

Hatta khatima wakahamia shamba Buibui wakakaa; hatta khatima wakarudi mjini wakakaa siku kaza wa kaza; hatta khatima baba yangu akasema: afdhali mke wangu tuhamie shamba Buibui wakahamia shamba Buibui wakakaa muda wa miezi sita. Nikazaliwa mimi nikaitwa jina langu mzee. Nikazaliwa katika mwezi wa ilhaji siku ya jumaa a tatu mwezi kumi na tatu kwa saa ya sita athuuri sene 1285, na mulki wa said Majid bin Saïd bin Sultan.

Baba yangu akafurahi sana na mama yangu akafurahi sana na yule ndugu ya baba yangu akaja akanitazama akaja na mke wake akanitazama, bassi. Hatta baada ya mwezi kupita akaja ndugu wa baba yangu Hamudi bin Amur akanichukua kwake Kwarara nikakaa kwa mke wake na jina lake Zafarani binti Abdallah Habeshia. Naye alikuwa akinipenda mimi sana zaidi kuliko ndugu ya baba yangu, bassi.

*) athani ist eine arabische Form, 1. pers. Imp.

Hatta khatima yule mke wa ndugu ya baba yangu akafa, bassi, akawa mimi kuchukuliwa kwa mama yangu nikarudishwa mjini kwa mama yangu, bassi. Mama yangu akanunua vijakazi viwili wa kunilea mimi. Wakakaa muda wa ijummaa moja wale vijakazi wakafariki wote wawili siku moja, bassi. Ikawa mimi sina yaya, ikawa ndugu yangu Ghasha binti Hasani ndiye yaya wangu akinilea mimi hatta nikapata kijana wa miaka miwili. Akaja mama yake baba yangu kutoka Maskati ikawa mimi kukaa kwa bibi yangu siku kaza wa kaza. Hatta khatima yule bibi yangu akafa. Akabaki shangazi langu aliyekuja naye bibi yangu; naye jina lake Zuwina binti Amur ilOmeiriya na binti wake Aza binti Muhammed.

Ikawa mimi kuhamisha kwa mama yangu, bassi. Nikakaa kwa mama yangu. Hatta khatima baba yangu akasema: afdhali tuhamie shamba. Mama yangu akasema: haya mume wangu, bassi. Wakahamia shamba wakakaa, bassi. Na yule ndugu yake baba yangu Hamudi alikuwa mtu mkubwa sana kwa said Majid, a na heshima sana, bassi. Hatta khatima tokea muda waliohamia shamba wazee wangu hawakupata mwezi mmoja illa walisikia said Majid amefariki. Na mimi kijana wa miaka mitano, bassi.

Wazee wangu wakarudi mjini wakakaa. Akatawala said Bargashi akasema: nataka watu Waarabu au Wangazija au Watwana au Waswahili au watu waliwowote niwapeleke Unyamwezi wakampige Mirambo, bassi. Said Bargash aliposema vile marra haukupata mwaka marra kikaja kimbunga, kikaangusha minazi kikaangusha na majumba yote, watu waliokuwa matajiri wakawa maskini, maana mashamba yao yote yameteketea minazi na migarafuu yote, bassi.

Baba yangu akasema akamwambia mama akamwambia: mimi, mke wangu, nitakwenda kwa Unyamwezi, maana yake sasa hatu na kitu, minazi yote imeanguka na migarafuu yote imeanguka na sisi hatu na shauri ya kufanya, afadhali mimi nitasafiri, bassi. Wakafanya mashauri ya kusafiri na yule ndugu yangu Ali akasema: na mimi kazalika nataka kusafiri pamoja na baba, bassi.

Wakaondoka wakasafiri baba yangu na ndugu yangu Ali na ndugu yangu Khalidi, mtoto wa shangazi langu, na mtoto wa shangazi langu mungine jina lake Sleman bin Salim. Na mama yangu akatoa mtumwa wake, jina lake Akilimali. Wakaondoka wakasafiri watu kaza wa kaza. Na huko nyuma mimi na mama yangu na ndugu zangu Maseudi na ndugu yangu mwanamke binti Hasan na ndugu ya baba yangu Hamud bin Amur.

Na wao waliambiwa: twaeni sasa reale 20 na mkirudi mutapata fedha yenu yote ya miezi mtakaokaa Unyamwezi. Wakasema: Heiwallah saidina. Wakaondoka wakaenda zao, bassi. Na huko nyuma mimi nikapata ugonjwa wa ndui mimi na ndugu yangu mwanamke na watu wote nyumbani. Mama yangu akamwambia ndugu ya baba yangu: tafadhali bwana nataka unipatie kiwacho chote nipate kula na huyu kijana, maana yake huyu kijana hawezi na mimi si na kitu na baba yake amesafiri naye hakuniachia kitu; au mchukue mtoto wenu, maana mwana wa ndugu yako bassi.

Yule ndugu ya baba yangu akamjibu: mimi si na kitu wala simchukui, aende akanitilie wanangu shamba, la, siwezi, bassi. Mama yangu akanyamaza asiseme neno la pili akajua: sasa nikasema ataleta maneno mengi huyu; akasubiri, bassi. Hatta khatima mama yangu alikuwa na mtwana wake, jina lake Sumail, naye mtwana huyu huenda kazini akileta mapesa, ndio tunayokula mimi na mama yangu; ikawa vivyohivyo hatta mimi na ndugu yangu tukapona ndui, na mimi kijana wa miaka sabaa.

Nilitiwa chuoni.

(Schulzeit.)

Mama yangu akasema kumwambia ndugu yangu Maseudi akamwambia: huyu kijana amepata miaka sabaa sasa na baba yake hayuko na mimi nataka atiwe chuoni akasome, bassi. Yule ndugu yangu akasema: naam afadhali nitampeleka akasome, bassi. Akafanya mashauri wakafanya na sadaka. Nika-

tiwa chuoni kwa maalimu Abdallah ilMadadi Kiponda. Nikakaa ili kusoma siku kaza wa kaza hatta baba yangu akaja. Naye mgonjwa sana wa tumbo akafanya dawa hatta akapata afya.

Wakaulizana khabari za safiri wakaelezana khabari yote ya walikokwenda. Na huku mama akamweleza khabari yote ya nyuma wanachotoka, bassi.

Hatta khatima baba yangu akamwambia mama yangu: huyu kijana tokea alipoingia chuoni hatta sasa tunaona hajui kitu, afadhali tutamtoa tutamtia katika chuo cha serkali, wanakosoma watoto wa said Bargash, bassi. Mama yangu akasema: haya chema unavyoona, ndivyo bassi. Wakanitoa wakanipeleka chuo cha serkali, na mimi kijana wa miaka minane. Nikasoma muda wa miezi sita nikatoroka nikaenda kwa ndugu yake baba yangu shamba Fuoni. Nikakaa hatta khatima akaja baba yangu akanikamata akanirudisha bassi.

Hatta khatima nikatolewa katika chuo cha serkali nikatiwa chuo cha maalimu Shekhi bin Fakihi ilMalindi. Nikakaa muda wa mwezi. Baba yangu akasafiri. Huku nyuma mama yangu akafanya mashauri na ndugu zangu ili kutia mimi katika jando bassi. Nikatiwa mimi katika jando na mimi kijana wa miaka tisaa. Nikakaa hatta baba yangu akarudi alikosafiri. Nami mule katika jando mimi na mtumwa wangu Kheiri na Abdulkheir, bassi. Hatta khatima tukatolewa tukapata zawadi kaza wa kaza, bassi. Hatta khatima nikarudi chuoni kusoma, ikawa mimi kulla siku utoro, baba yangu akafanya pingu akanitia hatta nikakhitimu nikatolewa chuoni. Na mimi kijana wa miaka kumi na moja, bassi.

Hatta khatima baba yangu na mama yangu wakagombana. Na sababu: baba alisema: mimi nataka kuoa mke khadimu ya ndugu yangu. Akamwambia: ukioa, mimi utaniacha, bassi. Hatta khatima wakafanya ugomvi wakaachana. Na baba yangu akaoa mke khadimu ya ndugu yake, na jina lake Tatu binti Sumaili, bassi. Na mama yangu akaacha kwa kuwa mali yake yote hatta na jumba yake ya njia kuu akanyanganywa na yule mtwana aliyekuwa akifanya kazi wakati nilipokuwa mimi na ndui naye alinyanganywa na jina lake fundi Sumaili. Na

mama alimnunua sababu ile yangu mimi baba akachukua, bassi. Ikawa mimi kukaa kwa mama na baba. Hatta khatima akaja ndugu yake baba yangu Hamudi bin Amur akamwambia: afdhali ndugu yangu, sasa tuhame hapa Unguja, maana yake hapa tufanye kitu hapa sasa, bassi. Wakafanya mashauri wakahama yeye na ndugu yake wakahamisha Mrima Pangani wakafanya mashamba wakakaa. Na mimi nikawa na mama yangu Unguja, bassi.

Hatta khatima akaja baba yangu akasema kwa mama yangu: nataka mwanangu nimchukue Pangani. Mama yangu akasema: mimi sikukatazi, walakin huyu kijana unasoma na wewe unataka kumchukua, haifai. Akasema: amekhitimu sasa, haithuru. Mama yangu akasema: la, humchukui mwanangu Mrima, bassi. Baba yangu akanyamaza asiseme neno akangoja akafanya taratibu zake, hatta akaniiba akanichukua Pangani; nikakaa muda wa mwaka. Akanisafirisha Maskati kwa ndugu yake mwanamke nikakaa muda wa miaka miwili.

Mimi kijana.

(Meine Jugendzeit.)

Hatta khatima nikarudi kwa baba yangu akanioza mke binti Saidi bin Salum ilLemkiye. Nikakaa naye Pangani nikatoroka naye tukaja Unguja kwa mama yangu nikakaa. Hatta khatima nikaingia katika kazi ya askari katika garde, bassi. Hatta khatima nikafanya kazi muda wa miaka mine. Nikaoa mwanamke mungine jina lake binti Raya binti Saidi bin Khalfani ilAdwaniye. Hatta khatima yule mke aliyenioza baba yangu nikamwacha na yule ndugu yangu binti Hasani akashikwa na maradhi akafariki, bassi. Hatta khatima na yule ndugu yangu Maseudi akafariki. Na mimi ni na wake wawili binti Saidi na binti Rashidi na watumwa wa mama yangu wote wakafa. Nikabaki mimi na mama yangu na yaya yangu na Mnyasa. Hatta khatima na yule ndugu yangu akafariki, yule Ali. Ikawa mama yangu mtoto wake mimi, bassi. Ni-

kakaa na mama yangu. Hatta khatima saidi Bargash akafa akatawali saidi Khalifa bin Said.

Ikawa mimi katika kazi ya askari nikatoka nikakaa mimi ikawa kazi yangu kukata vitambaa nikashona. Nikaona haifai ikawa kusafiri nikafanya biashara ya kulla kitu katika Mrima wa Pangani, bassi. Hatta khatima ikawa vivi siku kaza wa kaza. Na yule ndugu wa baba yangu akafa, yule Hamudi bin Amur, ikawa baba yangu kule Mrima peke yake na huku Unguja yule shangazi langu akafa na yule binti wake akafa. Ikiwa mimi Unguja mgeni, wasalaam.

Hiki kisa cha wazee wangu na mimi tokea sene 1285 hatta sasa sene 1310. Na sasa khabari ya safari yangu nilipo kuwa askari. Nalisafiri kwenda katika vita alipouawa Mdachi daktari walakini jina lake silijui katika Kismayu. Tukafanya mambo kaza wa kaza na mimi sikupata kitu cha heshima, na khalafu tukasafiri Pemba katika vita aliowawa nakhoza katika London Muingreza, sikupata heshima wa salaam.

Na katika khabari ya mwanamke niliyooa binti Saidi bin Khalfani, alipoona mimi si na kitu na mimi nimeoa mwanamke mungine akanambia: niache. Mimi nikamuliza: kwa nini? Akanambia: sababu umeoa mke mungine na tena hu na kitu. Na mimi nikamwambia: na kama sababu ndio hiyo, sikuachi. Akasema: utaniacha. Akaenda kunishitaki kwa jenerali wangu Matthews asipate haki akaenda nishitaki kwa kadhi Nasur asipate haki akaenda akanishitaki kwa kadhi Abdulazizi asipate haki ikawa kunishitaki kwa kulla siku naye hapati haki. Ikaendelea hatta na mama yake kuyaingia maneno yeye tu naye akafanya wazimu ikawa naye kunishitaki na kujitwika nguo mbovu kwenda nazo kwa kadhi usiku akawa hatta na ndugu yake naye akafanya wazimu ikawa na majirani zake wote kufanya wazimu, mchana hunyamaza na usiku hutanga nguo kwa makadhi, kwa kulla siku ikawa ndio kazi yao hiyo na vilio daima kama amekufa mtu nakudwiwa.

Hii ndio khabari ilionipata mimi tokea mimi kijana wa mwaka moja hatta sasa tokea sene 1285 hatta 1309, sijui khatima na ngine ya mbele; ya nyuma ni haya; na ya mbele ayajua Muungu na mtume we Muhammed. Wa salaam. Tamat.

Safari ya Berlin.
(Reise nach Berlin.)

Na hiki kisa cha safari yangu ya Berlin, nitaanza kueleza hapa katika kartasi hii.

Auwali nazukuru mimi Amur bin Nasur bin Amur ilOmeiri katika khabari ya safari ya Berlin Ulaya wa Majermani. Auwali naliondoka Unguja nikamwambia mama yangu: Mama, mimi nikijaaliwa nitasafiri Ulaya. Mama yangu akanambia: unakwenda kutafuta nini, mwanangu? Nikamwambia: nakwenda kutafuta kujuikana na watu na kutafuta riziki. Mama akanambia: haya mwanangu, walakin usitusahau kwa chochote huku nyuma. Nikasema: la, insh Allah taala, bassi.

Nikaondoka nikaaga mke wangu binti Rashidi nikaaga na mama yangu, wala sikuaga majirani wala watu wangine illa watu hawa. Nikaingia katika marikebu usiku. Na aliyenipeleka pwani yaya yangu Siyenu na ndugu yangu Khalid bin Muhammed; nikalala hatta asubuhi tukasafiri hatta tulipopata saa tisaa tukapata Tanga tukalala hatta kulipopambazuka asubuhi. Tukaondoka tukasafiri hatta kwa siku ya sita tukaona Adeni. Hatta alasiri tukaingia Adeni nikashuka katika Adeni nikapanda gari nikaingia katika Adeni. Na mimi nimeona katika Adeni mji wa Adeni nikaona na soko ya Adeni na katika bandari nikaona Wasomali ndio askari wa fordha. Na mji wa Adeni kama mji wa Pangani na milima kama Pangani na majebali makubwa. Sasa nimeona na mizinga katika majebali na watu wakapita chini ya majebali, bassi. Hatta khatima kwa siku ya sabaa tukasafiri tukaenda muda wa siku tano tukapata Suesikanali nikashuka katika mji wa Suesi nikaona gari la moshi nikaona na farasi nikaona na nyumba ya pasha nikaona yote niliyoona, bassi.

Hatta siku ya sabaa tukasafiri muda wa siku moja u nusu tukaingia katika mto mwembamba sana na mto huu umechimbiwa na Wafransa tokea Suesi hatta Port Said, bassi. Hatta kwa siku ya pili tukapata Port Said nikashuka katika Port Said nikatezama mji wa Port Said nikaona nguruwe wanatembea

katika mji usiku nikaingia madukani nikanunua kofia bassi. Nikarudi markebuni nikalala hatta asubuhi tukasafiri tukaenda mwendo wa siku tatu katika bahari ya Stambuli hatta tukaisha kwa siku ya sita tukapata Ulaya wa Mataliani. Nikashuka ndani ya mji nikatembea katika mji wa Mataliani. Nikaona mnara mkubwa nikaona na kilima kubwa sana na ndani ya kilima kinatoka moshi. Nikauliza ndio nini vile nikaambiwa: moto ule hatujui wapi unatoka tunaona na sisi vilevile, bassi.

Tukaondoka kwa siku ya pili tukasafiri hatta kwa siku ya tano tukapata mji nikauliza: hapa wapi? Watu wakaniambia: hapa ndio mji wa Wareno na jina lake Luzboa ndio Ulaya wa Ureno huu. Nikashuka nikaona ngome katika bahari na katika bandari. Nikaona na magari, bassi. Hatta khatima nikapanda marikebuni nikalala hatta asubuhi. Tukasafiri tukaenda mwendo wa siku tano tukaona mji nikauliza: huu mji gani? Nikaambiwa: mji huu ndio Ulaya wa Waholandi. Nikauliza: wanasema lugha gani watu hawa? Nikaambiwa: wanasema kama lugha ya Madachi; walakin si Madachi watu hawa, bassi. Tukaingia katika mji ule nikashuka nikaenda ndani ya mji nikaona mji wote wameenea mito nikaona na daraja za chuma, chini hupita marikebu na juu hupita gari la moshi; nikastaajabu sana khabari ile, maana yake tokea kuzaliwa kwangu sikuona khabari kama ile, bassi. Nikazunguka katika mji nikaona wanawake ndani yake wakikamata wanaume nikawaza: mji huu ndio mji wa wazimwi khasa, hii ndio akheri dunya na huku ndiko kupotea mimi Amur, bassi. Nikarudi markebuni nikalala. Hatta asubuhi tukashinda muda wa siku mbili; hatta siku ya tatu tukasafiri tukaenda hatta tulipopata usiku tukaona kandili zinawaka. Mimi nikauliza: wapi kule kunakowaka kandili. Watu wakanambia: kule ndiko Londoni Ulaya wa Wangreza, bassi. Nikatezama sana hatta kulipokucha asubuhi tukaona na majumba, walakin hatukushuka ndani ya mji. Nikaona na marikebu moja imetota, bassi.

Tukaenda hatta tukapata mji nikauliza: wapi hapa? Nikaambiwa: hapa ndipo Hamburg mji wa Madachi, ndio Ulaya

wetu ulio katika bandari. Nikauliza: ndio tumefika au bado. Nikaambiwa: sisi tumefika, walakin wewe bado, bassi. Mara nikaona mtu moja akaja akanambia: wewe ndio Amur bin Nasur ilOmeiri. Nikamwambia: naam, mimi ndiye Amur bin Nasur. Akanambia: haya, shuka katika marikebu, bassi. Hatta khatima nikashuka nikatiwa ndani ya gari wa farasi nikaenda hatta tukafika kunako bandari ya gari la moshi nikaambiwa: leo ndio utakwenda Berlin katika mji mkubwa sana nao ndio mji anaokaa sultani wetu na jina lake Kaiza Wilhelmu, bassi.

Hatta khatima nikaingia katika gari la moshi, markebu ya nchi kavu, na tokea Hamburg bandarini hatta Berlin na kama mtu anakwenda kwa miguu atakwenda kwa siku sabaa, walakin marikebu ya bara anakwenda kwa saa tano, bassi. Tukaondoka tukaenda hatta tukafika Berlin. Mara nikaambiwa: tumefika sasa katika Berlin, nikashuka ndani ya gari la moshi. Mara nikaona mbwana mkubwa daktari Büttner akanambia: wewe ndiye Amur bin Nasur? Nikamwambia: naam, ndiye mimi Amur bin Nasur. Na neno lake la kwanza akanambia: umekuja salamu salemina. Nikamwambia: naam. Akaniambia: ngalawa juu na wimbi chini. Nikamwambia: naam, ilhamdu lillahi rab ilalamina, bassi.

Hatta khatima akaniambia: sasa umefika hapa ndipo Berlini na sasa tuende jumbani, bassi. Tukaondoka tukaenda hatta nyumbani nikafanyiwa chakula nikala nikalala. Hatta assubui akaja daktari bwana mkubwa akanitazama akaniuliza hali yangu. Nikamwambia: hali yangu jema, bassi.

Hatta khatima akaniambia: tafadhali nataka wende kwangu ukatutazame. Tukaondoka tukaenda kwake nikamwona mama yake na mke wake na watoto wake wote akanambia: hawa ndio watu wangu. Wakafurahi sana wazee wake na mke wake na waana we kuwakuniona mimi na mimi nikafurahi sana nao nikala chakula hatta nikashiba. Hatta khatima nikarudi nyumbani kwangu nikakaa yeye kwa kulla siku huja kwangu akinitazama akaenda akanionyesha nyumba ya darasa akanionyesha na nyumba ya mizinga na nyumba hii sikupata kuona mimi tokea kuzaliwa kwangu hatta sasa wala mizinga

kama hiyo. Ikawa mimi naye akinifundisha namna ya mji, adabu ya watu wa huku akaninunulia mbau wa kujifunza kusoma na kitabu akanipa kwa muda wa siku hamse waasherini, bassi.

Hatta khatima tukaenda kufanya shauri mimi naye hatta khalafu akaja rafiki yangu naye ndiye maalimu wangu jina lake Hans Tsakhe akaja tukaenda tukafuatana kwa fundi kufanya nguo nikalinga nguo, bassi. Hatta khatima ikawa mimi kwenda kulla siku kwa bwana B. na kulla siku nikaenda mimi, yeye huona kama ndio leo siku kuu, bassi. Hatta khatima ikawa vilevile hatta sasa. Wa salaam.

Khabari ya katika Berlin.

(Sehenswürdigkeiten von Berlin.)

Hii ndio khabari ya katika Berlin niliyoona yote. Tamat.

Auwali ya kuja kwangu Amur bin Nasur katika Berlin. Auwali nimeona mji wa Berlin nikauliza mji huu watu wangapi ndani yake, nikaambiwa malyoni wa nussu malyoni watu walio katika mji huu, bassi.

Nikaona na majumba ya matabaka katika mji na kulla nyumba ghorfa tatu na ghorfa inne na kulla ghorfa yamejaa watu ndani. Na mimi katika siku nilizokaa zote nimeuliza: watu wenyewe majumba wako wapi? Sikuwajua, bassi.

Hatta khatima akaja rafiki yangu naye ndiye maalimu wangu jina lake Hans akanichukua kwake akanikerimu, bassi. Akanionyesha njia za mji kidogo akanionyesha na khabari za Berlin akanifundisha kuandika kidogo na kusoma hatta nikajua, bassi. Hatta khatima tukafanya darasa yetu. Ikawa mimi kupata wanafunzi kufundisha. Na mimi ikawa kazi yangu kuwafundisha lugha ya kisawahili na kuandika na wao kujifunza, bassi.

Hatta khatima akaja mwanafunzi wangu rafiki yangu jina lake Velten akanambia: tafadhali shekh Amur nataka tufanye usuhuba tufuatane pamoja. Nikamwambia: haya, bassi. Akawa mimi naye kufuatana na huku akinifunza namna ya kidachi.

Akanambia: Amur, umeona farasi kucheza ngoma? umeona farasi kuambiwa maneno akasikia? umeona farasi charaza? Nikamwambia: la, sikuona. Nikathani ni uwongo nikamwambia: unafanya thihaki sasa na mimi. Akanambia: la, na kama husadiki utaona. Nikamwambia: lini? Akanambia: kesho usiku insh Allah taala utaona. Bassi. Nikalala hatta ussubuhi tukakaa hatta usiku. Akanambia: haya tuende ukatezame leo. Nikaondoka nikaenda nikatazama nikaona watu ndani ya nyumba wamejaa tele, na nyumba hiyo ni ya chuma yote na ukubwa wake kama nyumba tatu ja Shaksi *), bassi. Tukakaa. Mara wakaja farasi wamepandwa na wanawake wakacheza. Hatta khatima wale waanawake wakashuka wakaachiwa wale farasi peke yao wakicheza wakiamurishwa na mwanamke na wao wanafuata. Nikastaajabu sana khabari ile, bassi.

Na siku nyingine akanipeleka katika nyumba ya nyama nayo bustani nikaona simba na paa nikaona na chui nikaona na kiboko nikaona na bweha nikaona na tembo wa pembe nikaona na twiga nikaona na punda milia nikaona nyama wote wa bara tokea wa bara hatta wa bahari, tokea wakubwa hatta wadogo, tokea panya hatta nyoka, tokea samaki hatta uronda. Nilipoona vile nikastaajabu sana khabari ile nikaona tokea kuku hatta ndege na kulla nyama ndani ya nyumba yake na kulla chumba kama nyumba ya saidi Ali, baiti ilajaib. Nikasema huko ndiko wapi, huku akhera au huku dunyani nisiseme neno nikanyamaza kimya. Na rafiki yangu huniuliza: vitu hivi viko Unguja. Na mimi hamwambia: naam, viko. Na katika roho yangu mimi naogopa, walakin nafanya roho yake na mume, nataka kutoka nende zangu, walakin nistahamili asinambie rafiki yangu: nyama unaogopa? Bassi. Maana yake manyama yale mimi sikupata kuona tokea udogo wangu hatta sasa, bassi.

Hatta khatima akanipeleka mahala kungine. Kuna nyumba kubwa na ndani muna vitu vya washenzi vyote vitu vya bara na vitu vya watu waliopigana na Wadachi nikaona, bassi.

---

*) Shaksi ist der Name eines reichen Mannes, Muhammed bin Abdallah, in Sansibar.

Tukatoka tukakaa hatta siku nyingine akanambia: leo tuende tukatazama teata. Nikaenda nikaona watu kupanda juu ya uzi wakaenda, nikastaajabu sana khabari ile. Hatta khatima nikaona wakafanya mahala nikaona majumba na bustani mara nisione kitu. Hatta khatima nikaona bahari na mawimbi na watu wanavua na watu wanapita ndani ya mashua na majabali. Nikathani kweli, hapa pana bahari, bassi. Hatta khatima nikaona na jua linatua nikafanya khofu sanasana. Nikathani kweli khabari hii nikamwuliza rafiki yangu: hapa Berlin au hapa katika marikebu sisi. Akaniambia: Berlini, kwa nini unauliza, Amur? Nikamwambia: la, nauliza, bassi; walakin ndani ya moyo wangu naogopa sana, walakin yeye hajui, na mimi nakhofu khabari ile, bassi. Hatta khatima tukatoka nikaenda nyumbani nikafikiri kucha, hatta assubuhi nisilale, bassi.

Hatta siku nyingine akanambia: tuende tukatezame muujiza mangine. Nikamwambia: muzuri? Akamwambia: naam, leo utaona simba anapanda farasi. Nikathani uwongo nikamwambia: haya tuende, bassi. Tukaondoka jioni tukaenda tukakaa hatta khatima nikaona tundu lake simba akaingia mtu ndani; na mara akaja kijana mwanamke na mara akaja simba akaja na farasi akaja na mbwa wakacheza sana; simba hupanda juu ya farasi ya nyuma, na mke humuamurisha; na yule simba hufanya kama anaoyataka yule mwanamke, bassi. Hatta khatima walipokwisha wakatoka. Bassi. Akaja na mtu mmoja mwaname akaingia ndani yake tundu la simba nyingine, na ndani yake tundu mu na simba sabaa akacheza nao akashindilia basitula akamushirikisha simba akapiga. Nikastaajabu sana. Bassi. Hatta khatima tukatoka tukarudi na huku nawaza khabari ile, bassi.

Hatta khatima siku nyingine tukaenda katika nyumba na ndani ya nyum bahiyo mu na mafupa ya watu, mu na na sanamu ya watu nikaona na sarufu yao nikaona na viungu vyao. Nikauliza: watu hawa wa lini? Nikaambiwa: miaka elfu wa themania mia. Nikastaajabu sana. Nikaona na watu waliyokauka wamegeuka mawe ya matumbawe. Nikauliza: watu gani hawa? Nikaambiwa: watu hawa ndio watu waliyoingiliwa na

bahari katika mji wao na sisi tukienda kuzamia tukaona vitu hivi tukaumbuwa. Nikastaajabu sana khabari ile, bassi.

Hatta khatima tukatoka tukaenda zetu, hatta siku nyingine akanambia: leo tuende tukatezame nyumba nyingine. Nikamwambia: haya twende. Tukaondoka tukaenda nikaona ndani ya nyumba hiyo mu na sanamu ya sultani yote ya ulimwenguni. Nikathani wazima nikauliza: hawa wazima au wamekufa. Akanambia: wazima walakin haya masanamu yao, bassi kwani unathani nini wewe Amur? Nikamwambia: mimi nathani labuda wazima. Akanambia: la, haya masanamu, bassi. Hatta khatima tukatoka tukaingia katika nyumba nyingine nikaona nyoka wazima na nondo. Na nyoka hawa wa kulla inchi tokea wa bara hatta Wahindi wamo ndani nikastaajabu sana khabari ile, bassi. Hatta khatima tukatoka tukaenda zetu nyumbani, bassi.

Hatta kwa siku nyingine akanambia: na leo, twende ukatezama khabari nyingine. Tukaondoka tukaenda nikaona nyumba kubwa sana na ndani yake mu na vitu vya Hindi vimekusanywa ndani tele nikatazama nikastaajabu sana khabari ile, bassi. Tukaingia katika nyumba nyingine nikaona masanamu ya kihindi na ya kiparisi na ya China na watu wanatikisa shingo. Nikauliza: watu hawa wazima? Akanambia: la, watu hawa masanamu, hawa si watu. Nikastaajabu sana miujiza ile na khabari ile, bassi. Hatta khatima tukatoka tukaenda zetu nyumbani.

Hatta siku nyingine akaja kwangu akaniambia: leo twende ukatezame mambo mengine. Nikamwambia: haya, twende. Nikaondoka tukaenda katika nyumba na ndani ya nyumba hiyo mu na macheza ya tembo. Nikakaa na yeye akakaa kitako. Mara akaja mtu na tembo watatu wakacheza hatta khalafu wakapewa kitambaa wakavaa wakacharaza kama watu. Hatta khatima wakaondoka akaja mtu mungine akapanda juu ya uzi akaenda, nikawaza labuda mtu huyu ataanguka. Hakuanguka, nikastaajabu sana kwa khabari ile ya tembo kucharaza na mtu kupita juu ya kamba, bassi. Hatta khatima tukatoka tukaenda zetu.

Hatta siku nyingine tukaenda katika nyumba nyingine na ndani ya nyumba hiyo mu na mizinga na bendera na mikombora

na sura ja watu nikaona na sura za miji na vitu vingine vyote vya Wafransa vilivyotekwa wakati wa vita Dachi na Mfransa. Nikaona mizinga sijapata kuiona na makombora sijapata kuyaona nikawaza khabari hiyo katika roho yangu, bassi. Hatta khatima tukatoka tukaenda zetu nyumbani.

Hatta kwa siku ya pili akanambia: leo twende tukatezame machezo mangine. Tukaondoka tukaenda katika mahala pakubwa sana, na siku hiyo ndio siku ilikuwa siku yake ya kuzaliwa sultani kaiza. Nikaona usiku umegeuka mchana, zimetapakaa taa katika mji, nikastaajabu sana khabari hiyo. Nikaona watu sijapata kuona waliko wengi nikaona na mambo kazawakaza, bassi. Hatta khatima tukarudi nyumbani.

Hatta siku nyingine akaja maalimu wangu Hans Tsakhe akanambia: tafadhali Amur wewe umeona askari wa kidachi hapa? Nikamwambia: naona njiani, bassi. Akanambia: bassi, tafadhali, nataka kesho kutwa uje kwangu tufuatane ukatazame askari wanavyocheza kiungani, na sultani atakwenda, bassi, tafadhali twende. Bassi. Hatta ikawa ile siku yetu ya miadi ikaja nikaondoka nikaenda kwake tukafuatana tukaenda hatta tukafika kiungani wakaja askari wote. Nikauliza: hawa ndio watu wa mji wote au askari, bassi. Akanambia: hawa askari nao si wote, hawa katika mafungu kumi yetu, hili ndilo fungu moja; ametamani sultani kuwatazama. Nikastaajabu sana. Nikauliza: hawa watu wangapi wote. Nikaambiwa: hawa elfu mia waliyopanda farasi na hawa wanaokwenda kwa miguu elfu mia. Nikasema: ilhamdu lillah rabb ilalamina dunia iko maskini Bushiri bin Salim amethulumu roho yake burre, watu kama hawa yeye alitaka kupigana nao, bassi. Mara alhasil akaja sultani na mkewe ndani la gari. Nikamwona. Nikaona na dude kama yayi yamepanda juu na ndani yake mu na watu. Nikauliza: ndio nini kitu kile? Nikaambiwa: Dude lile ndani yake mu na watu wamepaa juu wanatezama maadui atoka wapi, wakiona adui mara washuka walete khabari chini. Nikataajabu khabari hiyo, bassi. Hatta khatima tukarudi nyumbani nikamwona na sultani mwanamke wa Hollandi katika machezo hayo, bassi. Akawa mimi kutaajabu sana kwa kulla siku, bassi. Hatta

khatima tukaona mashangwi ya watu kazawakaza wanaotezama khabari ya machezo. Na mimi nikathani labuda katika mji hapana watu; watu ni hawa, bassi, kumbe ndani ya mji kama hakuondoka mtu. Nikatikisa kichwa changu na huku nikafikiri, bassi.

Hatta khatima kwa siku nyingine nikaona watu wanasema: leo sultani wa mji mgine atakuja hapa kumtazama sultani wetu, bassi. Naye sultani mwenyewe wa katika mji wa Italia, bassi. Mimi nikangoja hatta nikasikia: leo atakuja; nikaondoka nikaenda katika njia atayopita sultani nikakaa. Hatta mara nikaona wakaja watu wakajipanga safu na watu hao askari wa mji na majina yao mapolisai na kulla moja a na nguvu kama simba, wangine juu ya nyama na wangine wanakwenda chini. Na kulla asiyekuwapo siku hiye hakufaidi, na kulla asiyekuja au asiyekwenda katika Berlin hakujaaliwa wala hajazaliwa wala hana jina ndani ya dunia, bassi. Mara wakaja wafalume wawili, kaiza na mfalume wa Italia ndani la gari. Nikawaona nikafanya salamu. Mara nikaona na mke wake na mke wa kaiza wameingia katika gari moja. Wakaondoka watu wote wakafanya salamu wakamtupia maua na wao wakiitikia salamu na wakipokea maua, bassi. Hatta khatima tukaondoka na mimi nikaenda zangu hatta kwangu na huku nafikiri ufalme nasema katika roho yangu: ama ufalme ni kama huu asemaye vingine muongo, bassi.

Hatta khatima nikakaa kitako siku kazawakaza, bassi. Hatta siku moja akaja rafiki yangu Velten akanambia: leo tafadhal, Amur, nataka tukatembee katika nyumba ya pombe. Nikamwambia: haya, walakin wapi? Akaniambia: karibu, si mbali, bassi. Tukaondoka tukaenda katika nyumba ya pombe nikaona vioo vidogo sawasawa na kuta nikaona na kandile kwa kulla namna nikamwambia rafiki yangu: nyumba hii ya nani? Akanambia: nyumba hii ya tembo, bassi. Nikaona viti sijapata kuviona tukakaa kitako, bassi. Hatta khatima tukaona watu na vinanda na matarumpeta na ngoma. Nikauliza: watu hawa wanakwenda wapi? Akanambia: watu hawa watapiga ngoma hizi na matarumpeta haya kwa ajili yetu sisi tunaokunywa pombe kwa ajili kutuanis.

Nikawaza mimi ndani ya roho yangu: ikiisha kuwa nyumba ya pombe kama hii, chumba anayolala mwenyewe kama nini? Nikamwambia rafiki yangu: nyumba kama hii tokea kuzaliwani kwangu sikuona, nikisema nyumba hii kama ya sultani Unguja, la hii zaidi. Nikasema: alhamdu lillahi rabb ilalamina. Nikamwambia rafiki yangu: mimi nikienda Unguja nikahadithi khabari hii, watu hawatanisadiki watanambia wewe unapenda Madaehi ndio maana unasema hivi, bassi. Hatta khatima tukaondoka tukaenda nyumba nyingine nikaona zaidi kuliko ile, bassi. Ikawa kwenda nyumba baada ya nyumba hatta zikatimia nyumba sabaa na kulla nyumba zaidi kuliko ya pili, bassi. Akanambia: nyumba zilizo kama hivi katika mji huu jumla yake zote nikipunguza uwongo Ja baba 8000, na kulla nyumba zaidi kuliko ya pili. Nikasema: Allahu akbar. Bassi. Hatta khatima tukaondoka tukaenda zetu, bassi.

Siku nyingine tukaondoka tukaenda hatta tukafika mahala. Na mahala hapa pa na watu wengi. Nikauliza: watu hawa wani? Akanambia: watu hawa wamewekwa, kwa sababu pakizaliwa mtu au pakifa mtu au akija mgeni na watu hawa watu elfu sabaa, kazi yao hii, akija mgeni huuliza: umezaliwa wewe, hunena unatoka nchi gani, hunena umezaliwa siku gani na mwezi gani na hapa utakaa siku gani au miezi mingapi, na wewe kazi yako nini, bassi. Na wewe useme yote. Na ukisema: mimi si na kazi hapa, nimekuja tembea utasafirishwa mara au kama hawajui siku yako uliyozaliwa utasafirishwa mara hii. Ndio khabari yao watu hawa waliokalia hapa, bassi. Tukatoka tukaenda zetu, bassi.

Hatta siku nyingine tukaondoka tukaenda mahala nikaona nyumba na ndani ya nyumba hii mu na masanamu mengi sana nikaona na magari ya posta ya kulla inchi nikaona na marikebu za kulla inchi nikaona na mitambo inalia nikasikia na watu wanakuimba nikauliza: nini hivi? Nikaambiwa: mitambo hii unayosikia hao si watu wanaokwimba, nikastaajabu sana umuri ule, bassi. Hatta khatima nikatoka na yeye akatoka tukaenda zetu hatta tukafika nyumbani. Nikakaa.

Siku moja nikasikia: leo anakuja Bismark katika Berlini,

walakin atapita, hatakaa sana, bassi. Nikaondoka nikaend kunako nyumba ya gari la moshi. Mara nikaona wakaja wat wakaja na askari wakakaa safu. Mara nikaona gari linakuj na ndani yake yumo Bismark, wakaja watu wakafanya salam kwake. Mara akatoa kichwa chake ndani ya gari akaitiki salamu. Na mimi nikasogea hatta nikapata karibu yake ni kamwambia akaitikia akatoa ua kwa mkono wake akanip akanambia: tafadhal shwakhsa*). Nikamwambia: ahsanta Nikamutazama sana nikamwona mwana we na mke wake n ahali zake wote, na yeye a na mvi hatta kope, nikafurahi san kumwona kwangu Bismark, bassi. Hatta khatima akaondok akaenda zake na mimi nikaenda zangu nyumbani na huk ningali na furaha na kunusa lile ua aliyonipa, nikakaa nal siku kazawakaza hatta khatima nikalitupa, bassi. Tamat.

Wa salaam. Hiki kisa na khabari ya Berlin. Tamat.

Khabari nyingine ya Berlin.

(Sonstiges aus Berlin.)

Sasa nataka kuandika khabari yake ya magari ya moshi ya magari yanaokwenda katika njia za chuma na magar mengine yalio ghali na minara na saa na khabari ya majumb na maposta ninaoyaona, vidogo na vikubwa vilivyo katika nji na desturi ya Berlin niliyoijua na niliyoiona mimi, bassi.

Khabari ya njia, mapana yake pima tano na urefu wak upeo wa macho ya mtu. Na njia wanaopita watu mbali n njia inayopita magari mbali. Na njia hizo kwa kulla sik utaziona kama kioo, zi na watu kasid wa kufagia, kwa kull usiku hufagiliwa, na katika njia hizo sikupata kuona njia iliy namna nyingine, kwa kulla njia hali moja. Na katika nji hizo mu na taa na kulla taa inawaka zaidi kuliko ya pili. N njia hizo si za mawe wala kokoto. Njia hizo zimetiwa n vipande na khalafu lami na khalafu rangi uliziona kama hariri wala mimi sijapata kuona njia kama za Berlini, bassi.

---

*) So hat Amur das deutsche Wort gehört und geschrieben.

Na katika khabari ya taa za Berlin kulla siku huziona zinawaka, walakin sioni mafuta wala mwasha taa, huziona zinawaka; na kulla nyumba zimeenea taa zaidi kuliko khamsini; na mji wa Berlini wote unawaka taa na ikitoka baamwezi huijui kwa ajili ya taa.

Na majumba ya Berlini makubwa sana nayo ya na nguvu kana majabali nayo ni meupe nayo mazuri, wala sikupata kuona nyumba nzuri kama Berlini nayo na dhifu sana nayo kwa kulla nyumba ghorfa tatu hatta nne; hapana nyumba iliyo ghorfa moja wala mbili. Na nyumba hizo zi na mashimo chini na ndani ya mashimo wanakaa watu waliyo maskini na mashimo hayo kwa kulla shimo kana nyumba ya Taria. Na katika khabari ya matajiri wanaouza vyombo, utaona ndani ya maduka kwa kulla kitu tokea lulu na zahabu na fedha na shaba na chuma hatta mavi ya chuma wameweka na nguo, na kulla kitu wameandika na thamani yake juu ya mali na vitu na pete na saa ya fedha na zahabu kazalika. Wala hapana mwivi na kama atakwiba, bassi.

Na khabari ya njia za chuma. Mu na magari na magari hayo ukitaka kuingia themani yake nauli yake tokea pesa kumi na pili hatta pesa nne. Nayo yamefanywa na kochi ndani na vibao na vibaa na kulla anasa imo ndani ya gari, bassi. Na magari hayo ndiyo ghali ukitaka kwenda mahala tokea rupia tatu hatta esherini, bassi. Na mimi nikakaa hatta nimechoka sikuona nyama awayo yote wala nyama yake. Watu wamechukua ndani ya magari kwa kulla nyama tokea ngombe hatta nguruwe na hatta bidhaa nazo zitiwa ndani ya magari, bassi.

Na khabari ya magari ya moshi: Ukitaka kusafiri tokea mji hatta mji, yamefanywa na njia zake za chuma pale na magari hayo yaliyo ndani ya mji mbali na yaliyo mbali yako mbali. Na magari hayo kama majumba, ya na vyakula ndani, ya na maji ndani, ya na maduka ndani ya na vyoo ndani ya na kulla kitu ndani. Na ukitaka kusafiri mji wote unaotaka utaingia. Nayo ya na mahala pazuri na pabaya, ya na ghali na rakhisi. Mahala pa ghali pana matandiko ya makhmil ndani ya mahala rakhisi muna bao ndani. Na ukitaka kwenda

hatta nchi ya sultani Rum utakwenda ndani ya gari. Na hatta Ulaya yote ukitaka utakwenda, walakin i ghali sana nauli yake magari hayo. Na magari hayo si moja wala si arbain mia, nayo mengi sana hatta mtu hajui idadi yao. Na majumba yake magari yamejengwa kwa chuma, na kuti yake vyoo na kulla panda la magari urefu wake pima arbaini na mapana yake pima kumi. Hii ndio khabari ya magari ya moshi. Bassi.

Na khabari ya njia sikumaliza yote. Katika njia mame-fanywa vyoo vidogo na vikubwa na ukitaka kwenda chooni utaingia ukatabawali; na ikiwa usiku utaona kandili ndani inawaka ndani; na ukitaka kwenda kwa kikubwa utaingia ndani, walakini utatoa pesa nne, ndipo utapata kwenda chooni, bassi.

Na katika njia mu na miti na miti hiyo i na watu huingoja; na wakati wa bardi hukauka majani yote na wakati wa hari huchimbuka majani; na miti hiyo urefu wake *) kama miembe na unene wake *) kama mifinesi, nayo haina maana iwayo yote, imekaa zana, bassi.

Na ndani ya njia mu na ndege; na ndege hawo wengi sana, hawana idadi, nao wala hawakimbii mtu wakimwona; na wewe ukiwaona usiwapige, ukiwapiga utapata khatia kwa serkali, bassi.

Na mimi nimekaa siku nilizokaa nikaona watu kama hawo walivyo wengi, walakin sikuona hatta mtu mmoja kugombana na mwenzi we, hatta siku moja, kulla nimwona humwona na kazi yake akafanya na idha. Wala sikumwona mtu kijana anayepata miaka sita umri wake ikawa hana kazi katika mkono wake, kwa kulla umwonaye, utamwona ameshughulika na kazi; na mtu hana kazi husafirishwa mara, na kama hasafirishwi atakufa kwa njaa. Na watu wa huku hujifunza mambo kaza wa kaza ya dunia ya kulla kazi na ya kulla muhaji na kulla namna ya kusoma, watu wa huku wanajua.

---

*) Man beachte den Singular des Pronomens, wo wir den Plural erwarten.

Na katika khabari ya kupanga majumba, ukitaka kupanga nyumba kwa kulla namna ya upangaji utapata. Ukitaka nyumba tupu au ukitaka nyumba na vyombo ndani utapata. Ukipanga nyumba tupu utapata nyumba rakhisi, na ukitaka na vyombo utapata ghali, walakin utapata mtu akutumike, utapata kitanda na kochi na viti vizuri, utapata na zulia ndani na maji na mahala pa kutawabali, na mtumishi usubuhi atatandika atazoa uchafu wote atafuta matandiko atafanya vizuri asubuhi, na ukija utaona yote tayari amefanya, na wewe utatoa koodi kwa kulla mwezi tokea marka arbaini hatta eshrini. Utapata na kahawa asubuhi na mkate, bassi.

Na ukitaka nyumba tupu nayo utapata, walakin rakhisi inavunja mpishi, utapata nyumba haina hatta mtu ndani, nayo utanunua kwa kulla kitu wewe mwenyewe utatia.

Na katika khabari ya koodi ya nyumba, mtu huanza kutoa kabla hajalala ndani ya nyumba, ndipo unapotoa koodi. Na ukitaka kuhama, sharti useme katika mwezi khamstashara kati ya mwezi. Na ukisema akheri hutaweza kuhama, sharia haitakukubalisha kuhama, na wewe wala huwezi kuondoka kwenda mahala pangine, atatunzwa lasim. Na ukitaka kwenda kupanga nyumba au kitu kiwacho chote ukipatana naye mwenyi mali ukisema: naam nimekubali nitakuja, na wewe kama hutakwenda akikushitaki atapata haki. Wa salaam.

Na katika khabari ya makadhi hapana kadhi anayetoa rushwa kwa kulla mtu mwenyi haki yake, akishitaki atapata hatta nakama. Unamshitaki kwa sultani atatunzwa upewe haki yako. Na sultani hana hatta amri ya kuua mtu wala hana amri ya kufunga mtu. Sultani kazi yake hungoja mshahara wake, bassi, akapewa. Na mshahara huu wanatoa watu katika mji, kulla mtu anayekula mshahara hutoa fedha kidogo kwa kulla muda wa miezi mitatu na jina lake staia, koodi ya mji. Na kulla mtu mwenyi nyumba au mwenyi kiwanja au mwenyi shamba hutoa koodi hiyo lazimu, illa mtu kijana anayekuwa kwa mama yake na baba yake hatoi. Na fedha hiyo ndiyo anayopata sultani na inayofanywa kazi yote ya mji, bassi.

Na katika Berlini kuna bardi sana; muda wa miezi sita bardi na miezi sita jasho. Na jasho hili, afdhali ya bardi kuliko jasho hilo, maana yake utaona jasho sana, na ukiona jasho sana usitamani kuvua nguo zako utapata bardi inaingia ndani ya kifua na khatima utapata maradhi.

Na katika Berlin mu na daraja za chuma, mu na na mito, mu na na madau, mu na na mbwa wangi sana nako Berlini barra si kisiwa nayo nzuri sana wala si mbaya. Walakin khabari yake ni kama hii ya bardi yake maji huganda kama mawe, na ikija mvua huanguka mvua kama kokoto. Na mvua nyingine kama machicha ya nazi, bassi.

Hii ndio khabari ya Unguja.

Mtu atakaye kusafiri kwenda Unguja kwanza atashuka pwani. Ataona watu wanaokula nyama ya watu. Walakin si nyama, hawo wanakula fedha wake kuona hujui lugha yake Unguja. Watakujia watakuambia: unataka kwenda wapi, bwana? Nao watasema nawe kwa lugha ya kiingreza watakuchukua hatta nyumba unayotaka; atafanya shauri yako hatta ulichoshughulika; atakuja atakuambia: sasa unataka kwenda wapi, bwana? Utamwambia atakupeleka, na ukitaka kununua kitu atakupeleka kwa Wahindi wao. Maana watu hawo wa na Wahindi wao maalumu, kitu kwa reale utanunua kwa reale mbili na kitu cha pesa utanunua kwa pesa kumi. Hiyo ndiyo khabari ya watu hawo.

Pa na na wangine ndani ya mashua na wangine katika maduka na watu hawa watwaua na Wangazija na Washeheri, hawo ndio watu dhaifu walio katika kisiwa cha Unguja, bassi.

Na Unguja ndogo si kubwa walakin kwa mtu atakaye kukaa nzuri. Nayo i na biashara nyingi ya pembe na ya ngozi na ya sandarusi na ya garafuu na ya mihogo na mtama na kunde na nazi na makumbi na vifuo na kulla kitu.

Walakini na ukitaka kupanga nyumba Unguja utakwenda kwa mwenyi nyumba utapatana naye kama vile mtavyoafikana wewe ma mwenyi nyumba ikawa reale au mbili, maana

hapana kawaida hiyo kwetu. Nako ku na majumba ya mawe na majumba ya udongo nayo ya makuti. Ndio yaliyo rakhisi, themani yake tokea reale khamse mia hatta reale ishirini, utapata kununua; ukitaka kupanga tokea reale sita hatta robo utapata. Na nyumba za mawe ukitaka kupanga tokea reale miteen hatta reale tatu mwezi utapata. Walakin na nyumba hizo lazim kwa kulla kitu ununue mwenyewe tokea meko hatta fagio hatta mtumishi wa kufagia ndani ya nyumba.

Na katika khabari ya koodi hutoa akheri ya mwezi ikiandama mara utatoa, bassi.

Na Unguja kuna mifeleji katika njia, walakin ndani ya majumba hapana, illa mtumishi aende apeleke maji. Na Unguja ku na maduka na Wahindi na Waarabu na Washeheri na Wangazija na Watwana na Wasawahili na watu wa Mrima na Washenzi na Wazaliwa.

Na Unguja kuna mitaa: wa kwanza Fordhani na Malindi na Shangani na Mnazimoja na Kidotani na Kibunguni na Gogoni na Fungoni na Mtakuja na Sokoni na Baghani na Vuga na Mkunazini na Malindi na Kiponda funguni. Na mitaa hii yote mjini na mpaka wake daraja. Na upande wa pili: kwanza Vikokotoni na Kisiwani na Vikokotoni kwa wabuki na Mchangani na njia kuu na Miembeni na kwa Machoro na Kikwajuni na kwa said Hamud Kiungani na huku pia jina lake Ngambo. Na maana yake Ngambo kwa sababu ngambo ya mto. Na watu wanaokaa katika mji watu walio Waarabu na Wazungu na watu wangine kidogo Wangazija, walakin ndani ya Ngambo nyumba za makuti na watu wanaokaa Ngambo Waarabu na Watwana na Wangazija kazalika na watu walio maskini kama mimi Amur. Na mimi nakaa Vikokotoni. Na Ngambo hapana nyumba ya mawe; zipo kidogo, walakini si kama mjini. Nako ku na mabokhari mengi na watwana wa Kiangazija wauza nyama ndani ya mabokhari ya makuti.

Na katika khabari ya mashamba ya Unguja nayo kana mitaa, kwa kulla mahala pana mashamba: auwali Donge na Kinduni na Mwera na Zingwezingwe na Nyanyale na Uzini na Fuoni na Kwarara na Kikaangoni na Mwanyanya na

Buibui na Mwera na Pwani mchanga na Uzi na Mzizima na Bandamaji Mwanda na Chechele na Kisongoni na Uzi ndogo na Langoni na Mtoni na Bububu na Mbuzini na Kitumba na Fuoni na mangine siyajui.

Walakini mashamba haya yote ya Waarabu na Wahindi walionyanganya kwa Waarabu. Na mashamba ya saiyidi Chukuani na Chweni na mangine mengi sana, walakini hayo mawili ndio mashamba mashuhuri yanayojuikana nayo ndiyo anayokwenda mwenyewe, kwa kulla anapotaka kwenda shamba huenda yeye mashamba haya mawili. Na baathi ya mashamba nimeyasahau kuyataja, bassi.

Na Unguja kulla katika mashamba yalio mbali ku na watu, na watu hawo wakhadimu, nao hawana kazi illa uchawi na kulima na kuruka: na watu wenyewe aghlabu wanakaa katika Maweni na Mwanda na Donge na Muyuni na Pwani Kiwengwa na Uzini. Walakin Uzini uchawi wao punyu na asli ya punyu moyo wa nyoka na moyo wa guruguru na dawa nyingine ya miti na dawa nyingine katika makaburi ya watu. Na khalafu wanasaga mwituni hatta ikawa kama unga, bassi. Na wakisaga sharti upande juu ya mti na wao wawe na mti mrefu wakukaangia hiyo punyu, hatta khatima wakaipua wakaitia ndani ya mahala wanapotaka, basi. Na wakiwa na mtu hawamupendi hutolewa hiyo dawa kidogo ikatiwa ndani ya chakula akapewa yule mtu, bassi. Hatta akaisha kula hapati siku kumi atakufa, na ugonjwa wake hukohoa na ikanyaga mtu yale makohoo yake naye atakufa. Na mambo haya yako Uzini. Wa ama khabari ya Donge nako kasalika ku na uchawi. Walakin namna nyingine. Watu wa Donge uchawi wao wakiona mtu a na mali au amevuna mpunga sana humwangia wakamwua kwa sababu kutaka wote kula nyama ya ngombe. Naye akiisha kufa watafanya khitima na katika khitimata watapata kula nyama. Hiyo ndiyo khabari ya mashamba na khabari ya Wahadimu.

Na mjini kuna wachawi wa vizuu. Na vizuu vimekaa kama panya na chakula chao bisi na watu wanaofuga vizuu sana khadimu za said Hamid bin Sultan, hawo ndiwo wanaofuga

vizuu sana katika mji. Na khabari ya vizuu: hutumwa, wakaambiwa: nendeni mukamle fulani. Na wale hujua huenda wakamla maini yake yule mtu aliyeazimiwa bassi. Hio ndio khabari ya wachawi walio katika mji wa Unguja. Nayo khabari hii sahihi wala mtu asihasibu nidhihaki, bassi.

Na mashamba mangine wako uchawi, walakin si kama kana mashamba haya; maana mashamba hayo ndio maarufu kwa mambo hayo. Na ithana Wangazija nao wa na uchawi wao na uchawi wao wa ramli na masihiri na mazuka. Na wao hawafanya illa kumwona mtu yuko katika hadhi kwa sultani au kwa balozi au kama a na mali au a na watoto wengi bassi, humfanyia ushihiri wakamwua mara au mtoto wake au mke wake au humtoa katika nyumba yake anayopata hadhi mara.

Na katika khabari ya watu wa Unguja Waangazija nao kamalika, hatta kama mtoto wa miaka kumi anajua kazi ya wazee wake ya uchawi ndio kazi yao Wangazija. Nao wa na vijicho*) sana na wao wanapendwa na Wazungu wote kwa sababu wanafanya uchawi sana. Nao ni waongo sana nao hawana fadhili; ujapo kumpa zahabu kwa kulla siku, wakiona adui yako watakuletea apate kukuthuru. Hio ndio khabari ya Waangazija.

Na khabari ya Wasawahili kazi yao yote jema, walakin wangi katika Wasawahili wanaosoma ilmu hii, ndio kazi yao. Na Waarabu kazi yao hununua watumwa; kwa kulla panapo mtumwa mwema, atakwenda kumnunua hatta kama a na rasi-mali yake, ndio thamani ya mtumwa lazim atamnunua.

Na Waarabu hupenda sana kulisha watu na kukaribisha watu na kuheshimu watu. Walakin si wote wanaofanya hivi, bassi. Nao hupenda sana chakula kizuri na wanawake wazuri na nyumba nzuri na kulla kitu kizuri. Hii ndiyo khabari ya Waarabu. Na libasi nzuri, hatta kama themani yake elfu reale lazimu atanunua. Na adabu yake Arabu na heshima yake Arabu nyingine kuliko Wasawahili. Mwarabu ukienda kwake atakukaribisha kwa heshima atakupa kahawa; na

---

*) vijicho eigentlich grosse Augen.

ukinywa kahawa lazim unywe vikombe vitatu; ukinywa zaidi atakuambia: wewe mjinga. Na akikuuliza kunywa tena kahawa, umwambie: naam, walakin mimi nimekunywa, bassi. Atanyamaza. Atakuuliza: tafadhali, leo ntalala pangu. Na wewe utamwambia: mimi sina amri, amri yote kwako. Maana mimi niko kwako hapa, bassi. Na yeye atafurahi sana, bassi.

Na desturi ya kiarabu hakuuliza kama unataka kula au la. Desturi hiyo kwake Arabu ni aibu sana. Na Wasawahili kazalika bassi. Hatta khatima yule Mwarabu ataingia ndani ataamurisha chakula kipikwe, hatta khatima kitatoka barazani mtakula. Na katika kula usile kama chakula hukitaki atakasirika, yahitaji ule sana na furaha. Hatta kama chakula hukipendi, bassi, yeye atafurahi sana, bassi. Na khalafu yatakuja maji ya mafukizwa na ubani, na khalafu mtakunywa kahawa, na khalafu ndio atakuuliza khabari na hali na yote unayotaka. Walakin kama hujala kwanza hakuulizi neno illa: tafadhali pumzika. Na ukiisha kula na kunywa utapata mazumgumzo yake yote aliyonayo, basi.

Na khabari ya majumbani wanawake wa kiarabu nao wanafanya kazalika sawasawa. Na desturi ya wanawake, hapana mtu anayemwita mtu kwa jina lake, illa unaita na „binti fulani“ bassi. Na wanawaume kazalika, hapana mtu anayemwita mtu kwa jina lake, kwa kulla mtu atakuita „shekhi fulani“. Hii ndio desturi ya Waarabu. Walakini Wamanga desturi yao nyingine, si kama waliyozaliwa Unguya. Wanawake wa Wamanga wanaitana kwa majina „fulani na fulani“, bassi. Walakin na wanaume heshima yao kama masuriama. Hii ndio khabari ya Waarabu wa Unguja na wa Maskati, atakayesema namna nyingine hiyo mwongo wala hapana atakayesadiki. Ukienda kwa Mngazija kwanza atakupapasa kipindo akutezame, na khalafu ndipo akuuliza khabari unayotaka; na kama akiona hamuna kitu katika kipindo chako hakuulizi kitu, atakuambia: unataka nini hapa? Hii ndiyo khabari ya Wangazija na Wasawahili la, hawafanyi. Walakin mgeni asikae sana; akikaa sana watamnena na kumgugunua na kumnyanasa na khalafu ataambiwa: toka. Hii ndio khabari ya Wasawahili.

Walakini Wangazija mgeni akikaa sana utaambiwa khalafu mgeni huu mwivi. Hii ndio khabari yao hatta ajapokuwa mwana wa ndugu yake, lazim watamfanya kama hivi. Wa salaam.

Hii ndio khabari yangu mimi ninayoijua. Walakin sikuimaliza yote; insh Allah taala nikijaaliwa mwakani nitaandika zaidi kuliko hii mara elfu, nitaandika tokea Unguja hatta Mrima nimpe shekh ilakbar baba yangu maalimu wangu mwombezi wangu muhebu wangu iddoktor B. Muungu amupe afia na hadhi ampe na kulla neno lilio njema na mudiri kazalika na kulla watu walio katika nyumba yake tokea mama yake hatta mke wake hatta wanawe hatta na jirani zake wote na mimi kazalika. Wakatabahu ilfakir Allahi taala abdi rasuli Muhammed Amur bin Nasur bin Amur ilOmeiri bijedihi. Na mimi nimeandika ili kwa ajili zawadi yangu mimi ya Berlini. Tamat bitarikh yom 15 September 1892 bitarikh yom muhammadiye sene 1310.
Berlin.

Mashairi madogo.

(Kleine Gedichte.)

Die neue Villa.

1. Ninunuzile kiwanda
kwa samani ilio ghali
kwa kubali ya kukupenda,
nisikuliwe na mali.
Penyi duro kapavunda
hatta kikawa saugali,
kaazimia kwa kweli
kasidi kujenga nyumba.

2. Wawashi kaweniendea
hatta kapatana nao,
tukēsha kuniwakia
na washi niyapendao.
Saa ngema kazengea
wakati ulingineo;
kata mzinje kwa zeo
kasidi kujenga nyumba.

3. Nikatia na milango
ya msaje ilio ngema
na tumbuu na magwango
na misomari ya chuma.
Waliokiamba mbwongo
kuonakwe imekuima,
hapo ambile kusema:
flani we upete nyumba.

4. Kafukua na kisima,
maji ye yakawa mema;
ninywapo kazizimia
kulla siku ya Jumaa.
Hejabuni kakitia
ilikinga kuwekea
. . . .
isikusudie nyumba.

---

3. 8. upete Perfect von pata.

5. **Hatta siku zikipita**
niwene mtu akija
ghafula, nisipomwita
papo akaningilia.
Nitashilepo kuteta;
akanambia: tulia,
hatu na la kutetea,
toa mali nipa nyumba.

Die Einführung der Steuern.

1. Risala, funga safari,
tanga ulitweke zima,
wasili Zingibari
kwa mashekha wemawema,
ukaeleze khabari
Shangani kwa Hema.
Killa mcheka kilema
naye humsikilia.

2. Mwambia Shekhi Humudi:
awete watu wazima,
aanze tangu biladi
Mwera hatta Matetema
awambie: zidi ya mzidi!
kulla lijaalo ni jema.
Killa mcheka kilema
naye humsikilia.

3. Mwalikuwa kisema
kwamba Pemba imezama
nasi tumeisha zoea
kunywa maji ya ngama;
mwerevu wa kogelea
si mjinga wa kuzama.
Killa mcheka kilema
naye humsikilia.

4. Mwenzio akianguka
wewe sema: yamekoma.
Umwombee Rabbuka.
Kulla ninalomsama
haiwi kukutanika;
jamii mkamuzoma.
Killa mcheka kilema
naye humsikilia.

5. Ajabu hatta siyadi
wa mishipi na madema;
shurti watoe ushuru,
ndipo soko kusimama.
Sasa kwenu yamezidi
mboni mwashika tama.
Killa mcheka kilema
naye humsikilia.

6. Wayonga mti wayonga
matawi yamekuinama,
garofuu na mkunde
hatta kunde na mutama;
sasa mtanoa unga
menoni uliokwama.
Killa mcheka kilema
naye humsikilia.

---

5. 5. nitashile Perfect von taka (nach Art des Yao gebildet).
2. 2. awete = awaite.

Antwort auf dieses Spottlied.

Risala umewasili;
rudi tena, wende Pemba
kwa watu wenyi akili
wambao wanaokwambwa;
usiende kwa watu kasiri
wasiokula wakashiba;
pita ukiwasaili
haya siyakuombwa.
Amzindwaye simba
hana buddi na kuliwa.

Verkracht.

1. Yalia ya Ngambo
wakopi twakhubiri
yameenea na yimba
deni na bei ikhiari;
ya kiturumo ni mambo
hapana tena saburi.
Killa siku ni khabari:
fulani kafilisika.

2. Nu waliokwenda kopa
biladi ya Zingibari
wakinunua mashapa
wakitanga na bahari;
sasa yamewapotea
watamani kuhagiri.
Killa siku ni khabari
fulani kafilisika.

3. Na walao biskiti
kwa maandazi ya ngano,
killa siku ni mkili
karatasi na wino;
mda ikiisha wasili,
haifai mnongono.
Killa siku ni khabari
fulani kafilisika.

4. Na wapandao farasi
kwa madegile ya zari,
wakienda killa ginsi
kutuonya utajiri,
sasa yamewapotea,
tena hawana shauri.
Killa siku ni khabari
fulani amefilisika.

---

3. mkili vom arabischen Worte qal rufen.

Spottgesang auf Hamadi Omar.

1. Msagure, Msagure na kifimbo cheza.
Bushiri wamchezea Jermani, hatamweza,
atageuka muhadimu mchokoa pweza.
Kweli? uwongo?

2. Bushiri amenena: Bagamoyo ntakwenda
tena Jermani kwa askari na mizinga kenda.
kaitezama Mrima alioyoitenda.
Kweli? uwongo?

3. Bushiri amenena: Ningali kijana
hivi vita vya Bagamoyo sivijui sana.
Kaniitieni Kimweri na mweleka mwana.
Twende zangu!

Der Sultanspalast.

Bet il ajaib imenipendeza,
imejengwa pale chini ya gereza;
imetiwa rangi juu imepambwa fedha,
na bwana Khalidi anachezacheza.

Die Himmelserben.

1. Hawa walimwengu
wana madagana;
warithi wa mbingu
taka kutangana.
Ni Hasani ndugu
hapendi kufana.

2. Mekwisha waganga
na wanazuoni.
Apendalo Mungu
kiumbe haoni.
Ya rabbi, salama
tuvuke mtoni.

---

3. s. weleka ein Kind auf dem Rücken tragen; von di
ist ubeleko abgeleitet.

Der Dieb.

Nimwoni mwizi wa ndani
kwetu akatuingilia;
hajituka kitandani,
muizi kanisimamia.
Nifikiri nifanyeni,
si kisu, si na jambia.
Kulla nikiangalia
shari ya mwenda machoni.

2. Ndyivi hilo ni ajabu
ni wakhubiri ndugu ya
lalikitaka sababu
kufa na mtu mmoja.
Ukiliona mpumbafu
huenda likijinamia;
halegamiki kwa mbavu
kwa kotama, ni uthia.
Kulla nikiangalia
shari ya mwenda machoni.

3. Lalingia taratibu
kwa hila na kundoweza;
na milango nimefunga,
sijui lilipopitia
Lateleza ja mkunga
kwa mafuta kumwenea.
Kulla nikilangalia
shari ya mwenda machoni.

4. Lalinifutia mfuto,
nyumba akaifagia,
Asinisazie kitu,
pesa ya kuyatumia.
Kulla nikilangalia
shari ya mwenda machoni.

5. Kad tamati, watama.
Mola na kumhimidia.
Umeniona salama
mimi na watoto pia.
Mwivi hakuja kwa kheiri
aliniazima baya.
Kulla nikilangalia
shari ya mwenda machoni.

---

1. 1. nimwoni = nimwonene.
2. 1. ndyivi von mwivi nach der li-Klasse hier auf den Dieb selbst übertragen; vergl. auch ukilione und likijinamia, wo ebenfalls das li auf einen Menschen, den Dieb geht; auch 3. 5. lateleza.
2. 2. ya = yangu.

Spottlied.

Alikuwa akichunga
mbwa nyumbani kwa Osfali;
sasa anapanda punda
kwa khamsini reale.
Ya Rabbi, utulipie
tuli hayi dunyani.

Lied der Kinder zu Neujahr, wenn sie mit ihren Fahnen zum Schulmeister kommen.

Si letu, si letu,
la mwalimu wetu.
Kalamu na mbau
mkononi mwetu.
Vidaua vya wino
viko chuoni kwetu.
Twaomba salama
ya mwalimu wetu
Mngu tupe afia
na wazee wetu.

Na baada wapigana sana.

Was verglichen werden kann.

Kifaa kifanana
tui na maziwa!
Mwalimu mkinena
„simba“ ni adui.
Simba ni mlizi
kushinda awi.

Wie man zu Ehren kommt.

Ukitaka utukufu
kwa ziyana za Kiamu
sharuti ujikalifu
upike zakula tamu.
Tengoni wangakusifu
na zingawa za haramu.
Alao chao ni sumu
hakimshuki kooni.

Der falsche Bruder.

1. Nalithani wewe ndugu yangu,
kinona changu saghiri;
lako wewe kuwa langu,
na mtu kutoa kadiri.

2. Umeninywesha machungu
maji pwani kwa subili,
kutoa kwuza khabari yangu;
moyo u na kaserani.

3. Si furahi, ungacheka;
deni i na muungwana,
hai buddi kulipika,
hatta moyo kusonona.

4. Labuda nikutoeka,
mimi nawe kwandama.
Wa katabahu lijahil,
kalu: salama salimina.

Der Herr Gustav.

1. Bwana Gustavu apenda mpumbao;
usiku huvua libasi za kwao,
sikumtambua kiona ujao.

2. Mevua makoshi, metia ziatu,
mevaa kikoi libasi ya kwetu;
mejua na lugha zayidi ya watu.

3. Mejua kunena, sote tumekiri,
na wasiomwona tawapa khabari:
mewashiri sana akina Hesilari.

4. Na yake thamani nimekukhubiri
towa ya zamani ya Skekhi Nasiri
naye wapo duni heshima na kheiri.

Der Maurer.

Ukimtaka mwashi usimfuase kwa yake
pishi tatu za mchele ataka na chungu chake.

Räthsel.

Baba a na watoto watatu. Mkubwa akampa reale mia, wa katikati akampa reale miteen, wa mwisho akampa reale thelatha mia, na wote watoto wanawaume, watoto gani? Wako katika dunya yenu.

Majibu: Elif, Be, Te, The.

---

1. s. sikumtambua ist Perf. statt Praesens.

Rechenaufgabe.

Akapita mtu mmoja akaona ndege ndani ya mti akawaambia: assalamu aleikum ndege mia. Wakajibu: sisi hatujatimia mia; tunataka kama sisi na nussu ya sisi na robo ya sisi nawe uingie; ndipo tutimie mia, wallahu.

Räthsel.

Kijamanda cha bibi kijaa mbwebwe tele.

Majibu: Kinwa na meno.

Wa na nguo wote, wa na kofia upande, asio kofia upande si mwanangu.

Majibu: Vidole na kucha zao.

Simba mmoja akilia hapa, killa mahali watu wasikia.

Majibu: Kunguru.

Shungi la bibi latetea.

Majibu: Taa.

Tumbwa wangu wangenda kakata mayayi kenda na huko akenenda.

Majibu: Maboga.

Nyumbangu kubwa nguzo moja.

Majibu: Uyoga.

Kinderspruch.

Wawili wanaona,
wawili wanasikia,
watano wamesimama,
watano wameshika,
thenᶦni tha thelathᶦn wanakula.

Schwierige Fragen.

1. Moji a na mtumbwi
moji a na mshipi,
moji a na mdwani,
moji kavua.
Mwenyi samaki nini?

2. Tako la bunduki.
Mtambo wa bunduki.
Kasiba ya bunduki.
Mdeki wa bunduki.
Bunduki nini bassi?

Zu Ehren des Koran.

Ki na madoadoa ya zahabu
wala si ya Mzungu, ya Mwarubu.

Maneno ya vidole.

1. Twende!
2. Wapi?!
3. Tukebe? (tukaibe)
4. Tukigunduliwa?
5. Miye simo.

Pierer'sche Hofbuchdruckerei. Stephan Geibel & Co. in Altenburg.

Anthologie

aus der

Suaheli-Litteratur

(Gedichte und Geschichten der Suaheli)

gesammelt und übersetzt

von

Dr. C. G. Büttner,

Lehrer am Seminar für orientalische Sprachen in Berlin.

Zweiter Theil.

Uebersetzung.

Berlin.

Verlag von Emil Felber.

1894.